

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA BUURI MASHARIKI**102/1****KISWAHILI****KARATASI YA 1****INSHA****MAAGIZO :**

- (a) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
- (b) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobaki.
- (c) Kila insha isipungue maneno 400.
- (d) Kila insha ina alama 20.
- (e) Kila insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

MASWALI

1. Wewe ni mwanahabari wa kituo cha runinga cha mwelekezi. Andika mahojiano kati yako na mtaalamu wa maadili kuhusu hali ya maadili katika jamii ya sasa.
2. Suala la utovu wa usalama ni changamoto kubwa katika jamii. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali .Mchumia juani hulia kivulini.
4. Tunga kisa kitakacho malizika kwa .Nilifurahi sana kwamba niliweza kupata ufanisi wa kiwango hicho.

**TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA BUURI MASHARIKI
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA.****102/2****KISWAHILI****KARATASI YA 2****LUGHA****JULAI/AGOSTI 2019****MUDA: SAA 2 ½****UFAHAMU*****Soma kifungu kasha ujibu maswali.***

Dawa za kulevya ni donda ndugu katika taifa letu. Ni zimwi linalotesa na kufisha wazee kwa vijana. Halichagui jinsia, tabaka, rangi wala umri. Uraibu wa dawa hizi hauna faida yoyote. Wanaotumia dawa za kulevya huzitia mwili kwa kunusa, kuvuta, kumeza na kujidunga sindano. Zinapoingia katika miili ya watu madhara huwa mengi .

Kuna wale wanaokosa hamu ya kula, wengine huambukizwa maradhi kama vile ukimwi wanapotumia sindano zilizotumiwa na watu wenye virusi vya maradhi hayo kujidunga sindano na kutia dawa mwilini.

Mihadarati pia inaweza kufanya mtu awe mwendawazimu. Vifo pia hutokea ikiwa uraibu utazidi na mtu akose kupata matibabu. Mtu anayetumia dawa za kulevya huathirika akili. Yeye huwa hana uamuzi wenye hekima katika maisha yake .wengi wao hushiriki katika vitendo vya uhayawani. Wao hukosa fikra za utu. Baadhi yao wamebaka kina mama na watoto wadogo na wengine wamezua vita katika familia na kusababisha madhara makubwa katika jamii zao kwa sababu ya ulevi.

Familia za wanaotumia miadarati hazina amani. Jamaa zao hutumia hala nyingi kuwalipia ada ya hospitali ili wapate matibabu baada ya kuzidiwa na uraibu. Mali hufujwa na watu wenye uraibu wa dawa hizo pale wanapohakikisha hawazikosi kila siku. Mzazi kwa mfano anaweza kutumia hela kununua dawa za kulevya badala ya kumlipia mwanawe karo. Kuna wale wanaowaibia majirani na marafiki ili wakidhi mahitaji yao.

Ajali barabarani pia husababishwa na malevi. Dereva yejote awe wa matatu au gari la kibinasi anapoedesa gari akiwa mlevi huwa anahatarisha maisha yake mwenyewe, abiria na wananchi wanaopiga miguu barabarani .Uchumi wa taifa huzorota baada ya wananchi kutumia miadarati. Watu wenye uraibu hukaa mbumbumbu bila

kufanya lolote hasa kutokana na kudhoofika kwa afya yao au ulegevu unaosababishwa na ulevi. Watu wa aina hiyo huwa wanamchango haba katika ukuzi wa uchumi wa taifa.

Dawa hizi zimesambaa kila mahali utapata zinazuwa masokoni, shulenii, njiani na hata pahali popote pale penye watu. Dawa za kulevyaa haziuzwi hadharani nchini Kenya kwa sababu serikali imepiga marufuku uuzaji wa bidhaa hiyo. Waja wanaoziuza hufanya hivyo kisiri. Walangazi wa miadarati aghalabu hutumia watu wengine kuuza kwa niaba yao. Kuna wale wanaotumia watoto, wanaorandaranda almaarufu chokoraa na wengine hutumia vijana katika shule za misingi, upili na vyuo vikuu kama mawakala.

Vijana hasa wamejipata katika mtego huu kwa kuwafanya walangazi biashara hii haramu hili waweze kupata hela za kukidhi matakwa yao ukweli ni kuwa pesa wanazo patiwa na waajiri wao ni chache mno na hatimaye wao hutumia daw zile na kuishia kuwa na uraibu unaosababisha wao wenyewe kuwa wateja wa mabwenyenye hao wasio na utu.

Watua maarufu kama vile wafanyabiashara, wanamuziki na wanasiwa wametuhumiwa kushiriki katika biashara hii. washukiwa hawa mara nyingi hukosa kufikishwa mahakamani kwa sababu jamii hukosa ushahidi wa kutosha dhidi ya tabia hiyo. Ni nani hasa muhusika katika kuingiza sumu hii katika nchi yetu? hakuna mtu anayeweza kusimama kadamnasi na kusema hiyo ndiyo kazi yake. Mbona tushiriki katika biashara tusiyoweza kujivunia?

Ni mwito wangu kwa kila mwananchi mzalendo kuungana na wenzake ili kipinga biashara hii haramu. Tuhubiri makanisani, shulenii misikitini, hekaluni na mahali popote pale. Tukemee adui huyu, wa afya na mali. Washauri nasaha washike usukani wawashauri wazee kwa vijana, wakubwa kwa wadogo, weusi kwa weupe tuizike miadarati katika kaburi la sahau.

Maswali (al.15)

1. ape makala haya anwani mwafaka. (al.1)
2. Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa dawa za kulevyaa ni dondandugu katika taifa letu. (al.2)
3. Taja namna ambavyo dawa za kulevyaa zinavyotumiwa. (al.4)
4. Eleza athari ya dawa za kulevyaa kwa familia za wanaotumia. (al.2)
5. Kuna changamoto gani katika kupiga vita matumizi ya miadararati. (al.1)
6. Eleza sera ya serikali kuhusu dawa za kulevyaa. (al.2)
7. Msamiati ufuatao umetumika kumaanisha nini kwa mijibu wa taarifa. (al.3)
 - (i) mawakala
 - (ii) kadamnasi
 - (iii) washauri nasaha

UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Kila msanii anacho kifaa chake ambacho anakitumia, ambacho kinakuwa alama ya usanii wake. Mchoraji anategemea sana kalamu au rangi zake na mchongaji anao ubao au mti wake.

Vivyo hivyo mwanafasihi naye anategemea lugha katika usanii wake. Matumizi ya lugha ni miomgoni mwa mambo muhimu yanayotofautisha kazi ya fasihi na kazi isiyo ya fasihi. Jinsi ambavyo mwandishi anavyoitumia lugha yake na kiwango cha usanii anachofuraia ndivyo alama muhimu inayomtofautisha na mwandishi mwingine wa fasihi.

Katika uhakiki wa kazi za fasihi za hivi karibuni, hasa katika Kiswahili, kumekuwa na msisitizo mkubwa katika maudhui ya kazi hizo au kwa lugha rahisi, ujumbe unaotolewa na mwandishi. Vivyo maswali yanayoulizwa ni kama kazi hii ina umuhimu gani katika jamii ya leo? Inajengaje tabia, mwenendo na mwelekeo wa jamii? Ina maadili gani?

Mara nyingi, wahakiki hawaulizi mwandishi alivyofaulu kisanaa isipokuwa kama jambo la ziada tu mwishoni uhakiki wa namna hii hasa umehusu kazi za fasihi zisizo za ushauri kwa sababu imekubalika kwa muda mrefu kuwa mshauri

lazima aitawale luga yake vizuri ndipo aweze kuleta ule mvuto maalum unaotakiwa na kufikia viwango vinavyokubalika katika fani hii.

Haiwezekani kutenganisha maudhui na usanii katika kazi yoyote ile ya fasihi ujumbe unaoletwa katika kazi ya fasihi unaweza kutolewa na mtu mwingine yeyote kwa njia nyingine. Ujumbe huo unaweza kutolewa kwa njia ya hotuba, vitabu au maongezi ya kawaida.

Katika isimu ya lugha , tunaposema ya kwamba mwanadamu anajua lugha yake, tuna maana kuwa “amemeza” mfumo wa lugha yake wa matamshi, muundo wa maneno, muundo wa sentensi na maana zinazokusudiwa. Ujuzi alio nao mwanadamu huyu ni sawa, na ujuzi walionao wanadamu wengine wa jamii yake wanaozungumza lugha moja. Hivyo tukisema kuwa mwanadamu aongee lugha hatuna maana tu ya kule kumeza mfumo wake wa lugha bali ni uwezo wake wa kuitumia katika mahusiano yake na wanajamii wengine. Katika lugha yoyote ile kuna mitindo mingi inayotumika kutegemea kile kinachozungumziwa.Hivyo, tunaweza kuwa na mtindo wa siasa, sheria dini na kadhalalika pia upo mtindo wa kawaida unaotumika.

Katika mawasiliano ya kila siku ya wanajamii moja Katika mtindo huu kuna matumizi ya aina mbalimbali kihusiana na nyanja tofauti za maisha. Matumizi haya yanaitwa rejestra kwa lugha ya kitaalam. Rejestra yoyote ile inategemea nani anazungumza nini na nani, wapi kuhusu nini na kwa sababu gani.

Mtu anayejua lugha yake vizuri tunategemea aweze kuitumia katika mitindo iliyobadilika na aweze kujua mazingira anayopaswa kutumia mtindo mmoja badala ya mwingine katika mahusiano ya kawaida, mtumiaji wa lugha anapaswa kujua ni rejestra gani anapaswa kutumia kila wakati. Mwandishi wa habari lazima awe “amefuzu” kuliko kuweka haya matumizi tofauti ya lugha.

Mwandishi huyu anatakiwa kuwa mtafiti ili ajue Yale matumizi ambayo ye ye hana haja nayo katika mahusiano yake ya kawaida na huyo aweze kuchora jamii yake inayostahili katika kazi yake. Sababu kubwa ya kumtaka mwanafasihii kuyajua kinaganaga matumizi tofauti ni ule ukweli kuwa kazi ya fasihi haina mpaka na utumizi wa lugha.

Maswali.

- (a) Eleza vipengele muhimu vya lugha katika uwaishilishaji wa fasihi (maneno 70-80) (al.8)
NAKALA CHAFU
NAKALA SAFI
- (b) Fupisha aya tatu za mwisho(maneno 75-85) (al.7)
NAKALA CHAFU
NAKALA SAFI
MATUMIZI YA LUGHA.
- (a) Andika sifa za sauti zifuatizo. (al.2)
 - (i) /o/
 - (ii) /i/
 - (iii) /m/
 - (iv) /gh/
- (b) Huku ukitoa mifano eleza maana ya silabi fungo na silabii wazi. (al.2)
- (c) Tunga sentensi kudhahirisha dhana tatu za kiimbo. (al.3)
- (d) Ainisha viambishi katika maneno yafuatayo. (al.2)
 - (i) Wimbo
 - (ii) Muundo
 - (iii) Pazuri
 - (iv) Darasani
- (e) Tunga sentensi kwa kutumia aina zifuatizo za maneno. (al.2)
 - i) Nomino ambatani
 - ii) Nomino ya kitenzi jina
- (f) Tumia kiwakilishi kiashiria cha mbali badala ya maneno yaliyopigiwa mstari (al.2)
- (g) Eleza matumizi ya viakifishi vifuatavyo (al.2)
 - i)Koma

- ii) Mshazari
- iii) Ritifaa
- iv) Vifungo
- (h) Onyesha muundo miwili ya nomino katika ngeli ya (KI- VI.) (al.2)
- (i) Kanusha sentensi zifuatazo
 - i) Angesoma kwa bidii angeenda chuo kikuu.
 - ii) Nimeenda Nairobi kununua gari.
- (j) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa kinyume. (al.2)
Mwendawazimu alitembea haraka alipokumbuka alipoteka.
- (k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo umoja. (al.2)
Ngoma hizo zao ziliibwa na wezi wale.
- (l) Andika katika usemi wa taarifa. (al.3)
“Jichunge, “ alimkemea Kamau, “Mienendo yako itakuonyesha cha mtema kuni”
- (m) Andika katika hali ya kufanya. (al.2)
Yesu alikufa kwa dhambi zetu.
- (n) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate vifuatavyo. (al.1)
Gesi/kesi
- (o) Changanua kwa kutumia visaduku. (al.4)
Baba yake amemnunulia balskeli aligomwahidi mwaka jana.
- (p) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi yafuatayo ya (ku)
 - i) Kikanushi cha wakati uliopita.
 - ii) Nafsi ya pili umoja.
- (q) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (al.2)
KN (W+RV) + KT (T+RE)
- (r) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (al.3)
Mgema aliyesifiwa kwa kuwagemea wakazi tembo nzuri kwa nazi amenaswa.

ISIMU JAMII (AL.10)***Soma makala haya kasha ujibu maswali.***

- Kwani mnauza salamu? Sina time ya kuwaste hapa. Am a busy person leta order yake haraka... Nimesema samaki wa kupaka. Mimi ng'ombe na chicken.
- (a) Tambua sajili hii. (al.1)
 - (b) Fafanua sifa tisa za sajili hii. (al.9)

**TATHMINI YA PAMOJA YA ~~KAUNTI~~ NDOGO YA BUURI MASHARIKI
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA.**

102/3**KISWAHILI****KARATASI YA 3****FASIHI****MAAGIZO**

- (a) Jibu maswali manne pekee.
 - (b) Swalii la kwanza ni la lazima.
 - (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki.
 - (d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
 - (e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
 - (f) Watahiniwa wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na maswali yote yamo.
Swali la lazima.
1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.
Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.
Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

Maswali

- (a) Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)
- (b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)
- (c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)
- (d) Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)
- (e) Eleza umuhimu wa fomyula:
 - (i) Kutanguliza (al.3)
 - (ii) Kuhitimisha (al.3)

TAMTHILIA ; KIGOGO NA TIMOTHY AREGE

2. Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!
 - (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (al.4)
 - (b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (al.4)
 - (c) Eleza matatizo yanayoikumba safari inayorejelewa. (al.12)
3. Eleza nafasi ya mwanamke katika jamii ya kigogo. (al.20)

RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASHUMTA K. MATEI

4. Matatizo mengi yanayowakumba wahusika wengi katika riwaya hii ni mwiba wa kujidunga. Jadili (al.20)
5. Kwa kurejelea riwaya hii, fafanua mbinu zifuatazo.
 - (i) Kinaya
 - (ii) Mbinu rejeshi
 - (iii) Sadfa
 - (iv) Jazanda
 - (v)

HADITHI FUPI : TUMBO LISILISHIBA.

6. Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifauroongo na shogakedada ana ndevu fafanua changamoto zinazowakumba vijana. (al.20)

7. Mame Bakari

“Una nini ? Umeshtuka mwanangu ! Unaogopa? Unaogopa nini?”

- (a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (al.4)
- (b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondo. (al.2)
- (c) Eleza sifa za mrejelewa. (al.6)
- (d) Eleza umuhimu wa mse maji. (al.4)
- (e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. (al.1)
- (f) Fafanua maudhui katika swalida (e) kwa kurejelea hadithi nzima. (al.3)

8. USHAURI.

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Sinusubuwe akili, nakusihi e mwandani
 Afiya yangu dhahili, mno nataka amani
 Nawe umenikabili, nenende sipitalini
 Sisi tokea azali, twende zetu mizimuni
 Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
 Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
 Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini
 Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
 Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
 Dawa yake ni subili, au zogo huauni
 Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalo ndani

Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini.
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Waambowi damu, kalili ndugu msaidieni
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wamajano na wa kijani
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi mlangoni?

Maswali.

1. Lipe shairi hii anwani mwafaka. (al.1)
2. Toa sababu zinazofanya mshairi kutokana kwenda hospitali. (al.3)
3. Andika ubeti wanne kwa lugha ya nathari/ tutumbi. (al.4)
4. Taja bahari mbili zilizotumika katika shairi hili. (al.2)
5. Tambua nafsineni katika shairi hili. (al.1)
6. Tambua toni ya shairi hili. (al.1)
7. Eleza muundo wa shairi hili. (al.4)
8. Fafanua uhuru wa mshairi unavyojoitokeza katika shairi hili. (al.2)
9. Andika maana ya maneno yafuatayo kama yaliyyotumika katika shairi hili. (al.2)
 - (i) Dhalili
 - (ii) Azali

MWONGOZO WA KUSAHISHA .

FASIHI 102/1

TATHMINI YA BUURI MASHARIKI

MWAKA 2019

MWONGOZO WA KUSAHISHA KARATASI YA KWANZA .

1. a) Haya ni mahojiano .
b) Azingatie mtindo wa tamthlia.
c) Ahusishe wahusika wawili na majina na majukumu yao yabainike wazi mwanahabari na mtaalam.

HOJA.

- i) Ufisadi
- ii) Ulevi
- iii) Ukahaba
- iv) Utapeli kanisani.
- v) Kuteleke za watoto.
- vi) Vavyaji wa mimba.
- vii) Ulaghai.

CEKENA I
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
102/1
KIDATO CHA NNE

KARATASI YA INSHA**Swali la kwanza (lazima)**

1. Wewe ni Gavana wa gatuzi mojawapo katika nchi ya Kongomano. Wakaazi wa mji wa Songambele wamekiuka sheria zilizowekwa na baraza la gatuzi hilo. Waandikie ilani
2. Jitihada za kumwinua mtoto wa kike zimepeleka kudhalilisha kwa mtoto wa kiume. Jadili.
3. Andika kisa kitachodhihirisha maana ya methali.
Ulimi huuma kuliko meno
4. Tunga kisa kitakapomalizika kwa kauli ifuatayo.
..... Nilijitazama na kujidharau. Kwani nini nilijiingiza katika hali hii? Nilijuta.

CEKENA I
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
102/2
KIDATO CHA NNE
KARATASI YA PILI
LUGHA

A. UFAHAMU (ALAMA 15)**Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali**

Ajali haina kinga. Watu wengi wanapotajiwa neno ajali, fikira zao hukimbilia moja kwa moja hadi barbarani. Mara chachemawazo yao huenda viwandani, mashambani au kwenye viwanja vya michezo. Ni nadra sana watu kufikiraia kuwa nyumbani ndiko ajali nyingi zinztoke.

Idadi kubwa ya ajali nyumbani hutokea kimchezo tu. Watu wengi wameteleza msalani na wanapata majeraha mabaya. Wengine wameteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni, kama vile mafuta, mabaki ya chakula au hata maganda ya ndizi. Ulemavu walio nao watoto na hata watu wazima hutokana na ajali kama hizi wasizofikiria wtu wengi.

Ajali vilevile hutokea watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba kuu ya kutenda. Katika hali hii, huweza kujiumiza au kuwaumiza wengine bila kujua.

Hapa tunazungumzia ~~watu~~ ambaeo hujaribu kubebe mizigo yenye uzani wasiokadiria. Madhara huwa kateguka viungo na kuchanika misuli. Aghalabu hulemewa na kubanwa. Mwandishi wa makala haya siku moja alipanda kibao kuangika picha ukutani. Ingawa alikuwa mfupi, ari ilimsukuma kuchuchumia. Matokeo ni kibao kilijisukuma nyuma. Mhusika alianguka akajigonga kidevu. Kitendo hiki kilisababisha yeye kujuma ulimi vibaya. Kuvunjika jino na hata kuzirai. Bahati ni kuwa alikuwepo mtu aliyempa huduma ya kwanza na kumkimbiza hospitalini.

Hat hivyo ajali nyingi hutokana na vifaa vya nyumbani. Zana hizi ni pamoja na visu, meko ya gesi, mashine zinazotumia umeme na kadhalika na huwa hatari sana, hasa kwa watoto. Kitu kidogo hata kama wembe huweza kusababisha madhara makubwa. Kwa hakika hakuna ye yeyote kati yetu, hata waliokulia katika makasri ya fahari asiye na kovu. Makovu haya ambayo tunayaficha katika mavazi yetu ni ishara ya majeraha kutokana na ajali nyumbani. Je una kovu lolote?

Unakumbuka ulivyolipata?

Ingawa ajali hizi haziepukiki, yawezekana kuzipunguza. Ni muhimu kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani. Kwa mfano, ni hatari kuepu chungu chenye maji yanayotokota mekonu kwa mikono mitupu. Aidha ni

kutowajibika kuchanganya kitu chochote chenye unyevu na mafuta moto mekon. Watu wengi wamebambuka ngozi na nyumba kuteketea kwa namna hii. Kwa hivyo ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhalikisha tunavirudisha ipasavyo.

Jambo la tatu na muhimu zaidi ni kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza. Inawezekana kuokoa maisha au kuounguza majeraha kwa kuchukua hatua za dharura.

Maswali

1. Eleza maana ya methali ‘Ajali haina kinga’ (alama 2)
2. Kwa nini mwandishi anasema ajali nyumbani hutokea kimchezo? (alama 3)
3. Ni mambo gani mengine yanayosababisha ajali nyumbani? (alama 3)
4. Onyesha vile invyowezekana kupunguza ajali nyumbani. (alama 3)
5. Eleza maana ya:
 - (i) Jazba
 - (ii) Makasri
 - (iii) Makovu
 - (iv) Kuepua

B. UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali

Ardhi ni mali ya taifa. Hivyo inampasa kila raia kuinafidhi. Hii ina maana kwamba hatuna budi kuwarithisa wana na wjukuu, vitukuu na vilembwe, vining’ina na wapwa zetu ardhi yenye rutuba. Ardhi ndiyo chanzo cha riziki zote. Fauka ya hayo, ardhi ni dafina kubwa.

Tangu asili ardhi hii imefunikwa na joho la miti na majani. Rutuba ilienea kila mahali. Lakini wakati ulifika ambapo wanadamu hawakuvumilia kukaa bila kuitumia johari hii. Walishika maparange na mashoka.

Wakafyeka majani na miti yote. Wakalima wakapanda na kuvuna.

Kisha walihama hapo. Waliendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka. Hali ya kufyeka sehemu mbalimbali za nchi, kuchoma mioto ovyo, kuwa na mifugo mingi na kutojua kuhifadhi ardhi vizuri kulileta mavuno hafifu kila mwaka.

Mvua iliponyesha matone ya mvua yaligonga ardhi. Maji yakajiri kwa nguvu na kutawanya chembe za udongo. Wakati wa kiangazi udongo ulipokauka, upopo mkali ulichukua tabaka la juu. Hivyo ikawa mazao hayawezi kustawi. Hatimaye nchi ikawa kama mkuranga. Mambo haya yakasababisha mmomonyoko wa juu juu halafu mwanzo wa michirizi na mwisho makorongo na maporomoko ya ardhi.

Walakini basi ya kale hayapo. Sasa wakuu wa serikali yetu ya Insafu wamekuhimizeni, ikiwa mu wakulima, mpande zaidi. Wamewashauri namna ya kuongeza mavuno katika mashamba yenu kwa maarifa bora ya zaraa, kama vile kuunafidhi udongo, kutumia mbolea, njia za kunyunyizia dawa makondeni ili kuua wadudud wanaoharibu mimea, na kutumia maarifa malihi katika kupanda mbegu. Kwa wale amba si wakulima, serikali yetu ya Insafu imeweka shule za mafundisho maalum na kumhimita kila mmoja wao aongeze maarifa yake na afanye kazi kwa tabasuri na bidii ili aongeze mapato yake na mapato ya serikali pia. Katika sehemu nyingine maelezo ya wakuu wa serikali yamefuatwa barabara, na kumetokea maongezeko malihi ya mazao.

Walakini pia katika sehemu hizo maongezeko yake hayakutosha sana. Katika sehemu nyingine kwa bahati mbaya watu wamepotezwa na watu wakaidi amba kwa kutaka ushaufu, wamewaambia watu kuwa njia rahisi na nyepesi ya kujipatia serikali ya kujitawala yenyewe, na wamewashawishi na kuwatisha baadhi ya watu waasi amri za serikali zihusozo zaraa. Wahaini hao wametibia mambo. Ni watu wa kuaili na ni afkani.

Maswali

- a. Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho.

Nakala Safi

- b. Eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno 60.
(alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho.**Nakala Safi****C. MATUMIZI YA LUGHA**

- (a) Taja sauti mbili ambazo huitwa likwidi (alama 1)
(b) Andika neno lililo na muundo wa silabi ufuatao (alama 1)
IKKI
(c) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo (al. 2)
Yafutikayo.....
(d) Tambua aina mbili za sentensi ukizingatia uamilifu na utoe mfano mmoja kwa kila moja (ala. 2)
(e) Ainisha vielezi vya namna katika sentensi hii (ala. 2)
Mzee huyu mkongwe alicheka kijinga huku akila haraka haraka
(f) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (ala. 2)
Kijana aliyezungumza na nyanyake ameingia katika darasa lililochafuliwa na wanafunzi
(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mostari (ala. 3)
Mwanafunzi mwerevu sana aliyekuwa mgonjwa jana amepelekwanyumbani
(h) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo (ala. 3)
Somo aliukata mti kwa kisu jana asubuhi
(i) Andika kwa usemi wa taarifa (ala. 3)
Karani: Njoo nikutume kwa babu yangu.
Karanja: Sitaki kupita njia ya kwa babu
(j) Eleza matumizi ya ‘ni’ katika sentensi hii (ala. 2)
Ingieni darasani mara moja ili niwape zoezi ambalo ni rahisi
(k) Eleza maana ya sentensi ifuatayo (ala. 2)
(i) Ningalisona kwa bidii ningalipita mtihani
(ii) Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani
(l) Andika katika udogo wingi (ala. 2)
Mti wa msonobari unatengeneza meza nzuri sana
(m) Tambua miundo yoyote mitatu ya ngeli ya LI-YA (ala. 3)
(n) Eleza maana tatu za sentensi ifuatayo (ala. 3)
Alisema angeenda kwao
(o) Andika upya sentensi ifuatayo katika hali sambavu (ala. 1)
Mwanafunzi anasoma darasani
(p) Tumia neno ‘hadi’ kuonyesha mahalina wakati katika sentensi (ala. 2)
(q) Yakinisha katika hali ya mazoea. (ala. 2)
Asiyeugua hahitaji daktari
(r) Tunga sentensi ukitumia neno ‘komaa’ kama (ala. 2)
(i) Kivumishi
(ii) Nomino
(s) Taja matumizi yoyote mawili ya kistari kirefu (ala. 2)

D. ISIMU JAMII

- (a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha Kiswahili? Toa sababu tano (ala. 5)
(b) Fafanua sifa za lugha ya kazi (ala. 5)

CEKENA I**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
(KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION)****102/3****KIDATO CHA NNE
KARATASI YA TATU
FASIH****SEHEMU A:****“Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine”****Swali la lazima**

1. “Akanyangapo chini ardhi inatetemeka.....
Amejitia hamnazo. Kabwela kama mimi nina faida gani?
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
 (b) Fafanua mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (ala. 6)
 (c) Eleza madhila kumi yaliyompata Kabwela
 (ala.10)

SEHEMU B:**Chozi la heri****Chagua swali la 2 au 3**

2. wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinavyowalisha.....
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
 (b) Taja maudhui yanavyo jitokeza katika dondoo hili na ueleze (ala. 2)
 (c) Kwa kutoa hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (2b) yanavyo jitokeza katika riwaya (ala.10)
 (d) Eleza sifa nne za msemaji (ala. 4)
3. (a) Migogoro ni maudhui muhimu katika riwaya hii. Fafanua (ala 10)
 (b) Uozo umetamalaki katika jamii ya Chozi la Heri. Tetea kauli hii kwa kutolea hija kumi zilizoelezwa
 (ala10)

SEHEMU C: TAMTHILIA**Kogogo****Jibu swali la 4 au 5**

4. “Na mwamba ngoma huvuta wapi?”
 (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
 (b) Tambua tamathali mbili za sauti zilizotumika katika muktadha huo (ala. 2)
 (c) Fafanua sifa za msemajwa wa maneno (ala. 6)
 (d) Thibitisha ukweli kuwa kila mwamba ngoma huvuta kwake ukirejelea Tamthilia nzima ya Kigogo (ala. 8)
5. “Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyokas”
 Jadili usemi huo kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo (ala.20)

SEHEMU D: USHAIRI**Jibu swali la 6 au la 7****6. Shairi**

La adhabu hili wingu, lataka kutunyeea
 Himahima kwalo vungu, pasi nako kuchelea,
 Kujikinga hili wingu, sije katunyeshea.

Wengineo hawajali, wasinayo wasiwasi,
 Tahadhari hawabali, wajiunge nasi
 Aidha watafakali, mengine yalo hasi.

Vua hili halibagui, jinsia wala umri,
 Na kama hawajui, tuwajuze vizuri,
 Kwani siso adui, kuwao msumari.

Tangazo haliwapiku, wahimizwa kujikinge,
 Wingu hili la usiku, ukicheza likuringe,
 Latutia usumaku, daima likunyonge.

Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba,
 Yavuma kwa machungu, bila lolote huba,
 Tunza chako kijungu, fungia kwalo juba.

Japo nafika tamati, nawaacha tafakari,
 Madhara linalo wananti, wingu hili sukari,
 Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari

Maswali

- | | |
|---|----------|
| 1. Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne | (ala. 2) |
| 2. Onyesha ufundi wa kimundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili | (ala. 4) |
| 3. Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu. | (ala. 2) |
| 4. Kwa kuzingatia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu | (ala. 1) |
| 5. Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi yaidhini ya kishairi | (ala. 3) |
| 6. Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti | (ala. 3) |
| 7. Andika ubeti wanne kwa lugha ya tutumbi | (ala. 4) |
| 8. Eleza sifa moja ya nafsi nenii katika shairi hili | (ala. 1) |

7. Ushairi

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata

1. Maendeleo ya umma
 - Sio vitu maghalani
 - Kama tele vimesaki
 - Lakini havishikiki
 - Ama havikamatiki
 - Ni kama jinga la moto
 - Bei juu

2. Maendeleo ya umma
 - Sio vitu gulioni
 - Kuviona madukani
 - Kuvishika mikononi
 - Na huku wavitamani
 - Kama tama ya fisi
 - Kuvipata ng'o

3. Maendeleo ya umma
 - Sio vitu shubakani
 - Dhiki ni kwa mafakiri
 - Nafuu kwa matajiri
 - Ni wao tu washitiri
 - Huo ni ustiimari
 - lo! Warudia

4. Maendeleo ya umma
 - Ni vitu kumilikiwa

Na wanyonge kupatiwa
 Kwa bei kuzingatiwa
 Bila ya kudhulumiwa
 Na hata kuhadaiwa
 Hiyo ni haki

5. Maendeleo ya umma
 Dola kudhibiti vitu
 Vijapo nchini mwetu
 Na kuwauzia watu
 Toka nguo na sapatu
 Pasibakishiwe na kitu
 Huo usawa
6. Maendeleo ya umma
 Watu kuwa na kauli
 Katika zao shughuli
 Vikaoni kujadili
 Na mwisho kuyakubali
 Maamuzi halali
 Udikteta la
7. Maendeleo ya umma
 Watu kuwa waungwana
 Vijakazi na watwana
 Nchini kuwa hakuna
 Wote kuheshimiana
 Wazee hata vijana

Maswali

- (a) Toa anwani mwafaka ya shairi hili (ala. 1)
- (b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako (ala. 2)
- (c) Eleza dhamira ya mwandishi kuandika shairi hili (ala. 3)
- (d) Toa mifano miwili ya urudiaji katika shairi hili, Je urudiaji huu una kazi/majukumu gani? (ala. 4)
- (e) Onyesha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili (ala. 4)
- (f) Eleza toni ya mshairi. Toa sababu (ala. 2)
- (g) Nafsi neni ni nani? (ala. 1)
- (h) Toa mfano mmoja wa twasira katika hili. Je, twasira hiyo inajengwa na nani? (ala. 3)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Fafanua sifa za matambiko katika jamii (ala. 4)
 (b) Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa (ala. 10)
 (c) Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya Ulumbi katika jamii ya kisasa (ala. 2)
 (d) Tofautisha dhana zifuatazo
 - (i) Miviga na maapizo (ala. 2)
 - (ii) Ngoma na ngomezi (ala. 2)

CEKENA II**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI
(KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION)****102/1****KIDATO CHA NNE
KARATASI YA KWANZA
INSHA****Swali la kwanza (lazima)**

1. Wewe ni mwenyekiti wa kamati ya kupigana na ujisadi nchini Kenya na umealikwa, kuhutubia kongamano la kitaifa kuhusu athari za ujisadi huku ukipendekeza hatua za kukabiliana na janga hili. Andika hotuba utakayoitoa. (Alama 20)
2. Nyimbo za kitamanduni zilikuwa na nafasi kubwa katika ufanisi wa jamii kwa jumla. Eleza. (Alama 20)
3. Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali isemayo; Bahati ni chudi (Alama 20)
4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo; Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote. (Alama 20)

CEKENA II**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019
(KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION)****102/2****KIDATO CHA NNE
KARATASI YA PILI
SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA****A. UFAHAMU (ALAMA 15)****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Hakuna dakika inayopita bila kisa cha kuchelewa. Mikutano karibu yote hucheleva kuanza kwa sababu wahusika hawafiki wakati ufaao. Ibada nazo hucheleweshwa kwa uzembe wa waumini. Na mazishi je? Taratibu hucheleweshwa vilevile. Ingawa hapa yaweza kufikiriwa kuwa pengine wampendao marehemu hawataki kuharakisha safari yake ya kwenda kuzimuni. Lakini hata arusi ambazo huwa na misururu ya mikutano ya maandalizi, siku itimiapo shughuli hucheleva. Si ajabu sherehe kuendelea mpaka usiku ambapo ratiba ilionyesha zingekomea masaa ya alasiri.

Uchunguzi unabainisha kuwa watu hucheleva kwa sababu mbalimbali. Sababu mojawapo ni kutowajibika; yaani, watu wengi hawaoni umuhimu wa kuzingatia saa. Wengine hufanya hivi kwa kisingizio kuwa ni kawaida ya mwaafrika kutozingatia muda. Huu ni upuuzi mtupu. Wazee wetu walizingatia muda ipasavyo tangu jadi ingawa hawakuwa na saa wala kalenda. Hii ndiyo sababu walipanda mimea walipohitajika, wakavuna na hatimaye wakapika na kuandaa ipasavyo. Wahenga hawa walituachia methali nyingi kama funzo, kwa mfano; ‘Chelewachelewa utakuta mwana si wako’, na hata wakasindikiza kuwa, ‘Ngoja ngoja humiza matumbo’.

Watu wengine hucheleva kwa sababu ya kutojiandaa kwa yale yatakayojiri. Watu wasiopanga shughuli zao na badala yake kuzifanya kwa kushtukia aghalabu hushindwa kuhudhuria hata mahojiano ya kuajiriwa kazi kwa wakati ufaao. Hawa huwa neema kwa washindani wao. Kujitayarisha si jambo gumu. Anachopasa kujua mhusika ni saa ya miadi na hali ya usafiri.

Hivi viwili vitamwezesha kujua muda wa safari na hivyo kukadiria wakati wa kuondoka. Ni wangapi wameiona milolongo ya watu nje ya milango ya benki wakiwasih mabawabu na pengine kuwashonga wawaruhusu kuingia? Hawa huwa si wageni. Ni wateja wanaojua ratiba ya kazi lakini hushindwa kupanga mwenendo wao barabara.

Mikutano, sherehe na shughuli nyingi huchelewa kuanza kwa masaa mengi kwa sababu eti mgeni mashuhuri amechelewa kufika. Muda wa kungoja huwa mrefu zaidi kutegemea ukubwa wa cheo cha mhusika. Watu hawa huchelewa makusudi kwa sababu pengine ya kiburi. Majivuno haya huwafanya wafurahi wanaposubiriwa na watu wadogo. Wakubwa hawa wanapofika badala ya kuomba msamaha, hujigamba kuhusu majukumu yao mengi na makubwa.

Aidha kuna watu ambao hupenda kutekeleza mambo mengi kwa wakati mmoja. Tujuavyo ni kuwa mambo mawili yalimshinda fisi. Pia watu wanaposhika mengi, mahudhurio yao katika baadhi ya mambo hutatizwa na hivyo huchelewa. Isitoshe, kuna watu wa aina hii hata wanapopewa ratiba mapema, hujikokota na hivyo kupitwa na wakati.

Ingawa sababu tulizozitaja hutokana na watu wenyewe, kuna zile zinazosababishwa na dharura nyingine. Hizi ni pamoja na misongamano ya magari, kuchelewa kwa vyombo vyaya usafiri na hata kuharibika kwa vyombo. Hii ndiyo sababu inashauriwa kuwa mtu anapoamua kutekeleza jambo, atenye muda takribani wa dakika 30 kwa ajili ya dharura fulani. Kwa hivyo hata anapopata tuseme pancha njiani bado atafika kwa wakati ufaao.

Kuchelewa hakuudhi tu watu wanaocheleweshwa bali huwa na matokeo mengine mengi. Mara nyingi watu waliochelewa huharakisha mambo ili kufidia muda walioupoteza. Kama wanaendesha gari, kwa mfano, basi huzidisha kasi matokeo huweza kuwa ajali ambayo mara nyingine huleta ulemavu au vifo.

Ratiba ya mambo ichelewapo watu waliofika mapema hypoteza muda kusubiri. Muda huu wangeutumia kwa harakati muhimu. Mfumo wa uchumi wa kisasi unahitaji mamilioni ya watu kukurubiana, kutagusana na kuendesha shughuli zao kwa ujima. Aidha, watu hawana budi kubadilishana bidhaa na huduma. Mambo haya yanapocheleweshwa basi gharama huwa kubwa.

Tatizo hili hubainika sana katika ofisi za umma.

Ni kwaida watu kufika kazini dakika nyingi baada ya wakati wa kufungua milango ya kazini.

Ajabu ni kuwa wafanyakazi wawa huwa wa kwanza kufunga kazi kabla ya kipindi rasmi.

Inakisiwa Kenya hypoteza shilingi bilioni 80 kila mwaka kupitia uzembe wa kutozingatia wakati.

Jambo la kwanza ni kuweka sera ya kitaifa inayolenga kuwaelimisha wananchi umuhimu wakizingatia saa. Halikadhalika kanuni iwekwe ya kuwafungia nje watu wanaochelewa kuhudhuriashughuli za mikutano au hafla. Wananchi nao wazinduliwe kuwa ni haki yao kufumkana muda washughuli unapowadia kabla mgeni wa heshima kufika. Nchi ya Ekwador (Ecuador) imefanikiwakutekeleza haya. Kenya pia haina budi kuandama mwelekeo huo. Hii ndiyo njia mojawapo ya kufufua uchumi na kuhakikisha taifa linapiga hatua kimaendeleo.

Maswali:

1. Kipe kifungu hiki anwani mwafaka (ala. 1)
2. Taja watu watatu walio na mazoea ya kuchelewa katika shughuli walizoalikwa (ala. 3)
3. Taja sababu zinazofanya watu kushindwa kutimiza miadi (ala. 4)
4. Taja na ueleze njia nne zinazoweza kuondoa tatizo la kuchelewa (ala. 4)
5. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa
 - a) Ujima
 - b) Miadi
 - c) Pancha

B. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yote

Takriban kila siku vyombo vya habari hueleza kuhusu mateso ya watoto; cha kusikitisha zaidi ni kwamba mbali na visa vinavyoripotiwa, kuna vingine chungu nzima ambavyo havijaripotiwa. Mateso kwa watoto hawa ni ya aina mbalimbali. Mwezi wa Julai, 2005 wavamizi walipowaua watu zaidi ya sabini Kaskazini mwa Kenya, walianza kwa kuwauwa watoto katika shule ya msingi ya Mabweni. Waliwauwa watoto ishirini na wawili huku mamia wakijehuriwa.

Kuna wazazi ambao huwapiga watoto wao mithili ya kumpiga nyoka. Utaona watoto wakiwa na majeraha yanayofanya malaika kusimama mwilini. Visa vingi vimeripotiwa ambapo wazazi au walevi

huwakata au kuwadhuru watoto sehemu fulani za mwili kama vile masikio, miguu au mikono. Vilevile, kumetokea visa vya kuwachoma watoto na wengine kuwachwa bila chakula.

Kenya ni mojawapo ya nchi zilizotia sahihi mkataba wa kulinda haki za watoto. Serikali yetu ina idara katika ofisi ya makamu wa rais inayoshughulikia maslahi ya watoto. Mwezi wa Julai 2005, Serikali ilianzisha kampeni kabambe za kukomesha mateso dhidi ya watoto. Ajabu ni kwamba watu wengi na hata watoto wenyewe hawajui haki zao. Sheria ya watoto ilipitishwa ili kutetea haki za watoto katika nchi ya Kenya.

Baadhi ya haki za watoto ni kama vile kulindwa kutokana na ubaguzi wowote, kutunzwa na wazazi na kupewa elimu. Watoto wana haki ya elimu ya kiakademia na dini. Vilevile wana haki ya kulindwa kiafya. Watoto hawatakikani kunyanyaswa kiuchumi au kwa njia nyinginezo kama vile kusajiliwa kupigana katika vita. Kila mtoto akiwemo mlemau, ana haki ya kuheshimiwa katika jamii.

Hata hivyo, sharti pia watoto wawajibike ipasavyo kwa wazazi, walezi na jamii kwa jumla. Mtoto anapaswa kuheshimu wakuu wake na kuwasaidia panapo haja. Watoto wana jukumu la kudumisha na kuimarisha umoja wa jamii na raia kuendeleza maadili mema katika jamii.

Maswali:

- (a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 60-80
Matayarisho
Jibu
- (b) Bainisha mambo muhimu aliyojadili mwandishi katika aya tatu za mwisho.
(Maneno 100 – 120)
Matayarisho

- C. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**
- (a) Taja vipasuo viwili vya ufizi
(alamu 2)
 - (b) Onyesha maumbo mawili ya silabi funge kwa kutolea mifano katika maneno
(alamu 2)
 - (c) Bainisha mofimu za neno ‘kilichonywewa’
(alamu 3)
 - (d) Unda nomino moja moja kutokana na nomino zifuatazo
 - (i) Madhara _____
 - (ii) Kitenzi _____
 - (e) Tambua virai vihusishi katika sentensi ifuatayo
Wengine wao waligesha kando ya barabara iliyokarabatiwa na kampuni ya Kichina
(alamu 2)
 - (f) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kutumia ‘po’
 - (i) Raia wakipatana maendeleo yataimariika
(alamu 2)
 - (ii) Mkiwatesa watoto wenu intashtakiwa
 - (g) Andika kwa ukubwa hali timilifi
Mtego ulimnasa ndovu huyo
(alamu 3)
 - (h) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kivumishi
Msichana amepigwa yibaya
(ala. 2)
 - (i) Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo
Wanafunzi walimwatikia mwalimu mkuu miche ya matunda nje ya nyumba yake kwa ustadi wakitumia vijiti.
(alamu 4)
 - (j) Andika visawe viwili vya neno ‘vurumai’
(alamu 2)
 - (k) Taja na utolee mifano matumizi mawili ya mshazari
(alamu 2)
 - (l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao kisha uichanganue kwa matawi
S – KN (N + V) + KT (T + E)
(alamu 4)
 - (m) Andika kwa usemi halisi
Kyalu alikiri kuwa kama wangefika mapema wangekamilisha shughuli zote
(alamu 2)
 - (n) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo
 - (i) Alipokelewa mgeni
(ii) Alipokezwa mgeni
 - (o) Andika kinyume
Vijana walivunja kambi baada ya macheo
(alamu 3)
 - (p) Kanusha
(alamu 3)

Asha aliwapelekea wageni chakula na akawanavya mikono

D. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

- | | |
|---|-----------|
| (a) Eleza sifa zozote tano za lugha ya itifaki | (alama 5) |
| (b) Hakiki sifa zozote tano za sajili ya kituo cha polisi | (alama 5) |

CEKENA II

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019

(KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

102/3

**KIDATO CHA NNE
KARATASI YA TATU
FASIHII**

SEHEMU A: Riwaya

1. LAZIMA

Assumpta K. Matei: Chozi la heri

“Hili lilitmia uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke.”

- | | |
|--|-----------|
| (a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake | (alama 4) |
| (b) Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili | (alama 1) |
| (c) Kwa kutumia hoja <u>kumi na tano</u> , eleza namna suala ulilolitaja hapo juu 1 (b) linalijitokeza | (ala. 15) |

SEHEMU B: Tamthilia

Kigogo (Pauline Kea)

Jibu swalii la pili au la tatu

- | | |
|--|------------|
| 2. “Kubali pendekizo letu la kufungwa kwa soko..... huoni hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi?” | (alama 4) |
| (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili | (alama 4) |
| (b) Kufungwa kwa soko ni ukatili. Mbali na ukatili huu, toa mifano mingine ya ukatili kwenye tamthilia. | (alama 9) |
| (c) Msemaji wa maneno haya ni mshauri mbaya. Thibitisha kutoka kwenye dondoo na kwingineko tamthilianii. | (alama 7) |
| 3. (a) Fafanua mbinu kumi anazotumia Majoka katika kuuendeleza uongozi wake | (alama 10) |
| (b) Eleza namna mbinu ya <u>ishara</u> ilivyotumiwa katika tamthilia ya <u>Kigogo</u> | (alama 10) |

SEHEMU C: Hadithi Fupi

Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (Alifa Chokochi na Dumu Kayanda)

Jibu swalii la 4 au la 5

- | | |
|--|------------|
| 4. “..... Ningendoka..... mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana.” | (alama 4) |
| (a) Eleza muktadha wa maneno haya | (alama 2) |
| (b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili | (alama 9) |
| (c) “Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja <u>tisa</u> | (alama 5) |
| (d) Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii | (alama 13) |
| 5. (a) Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya <u>Masharti ya Kisasa</u> | (alama 7) |
| (b) Kwa kurejelea hadithi ya <u>Shibe inatumaliza</u> , eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza | (alama 7) |

SEHEMU D: Fasihi Simulizi

6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

Heri ujue mapema

Nasaba yetu haina woga

Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.

Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisuu cha ngariba ni kikali ajabu.

Iwapo utatikisa kichwacho.

Uhamie kwa wasiotahiri,

Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

Maswali;

- (a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu (alama 4)
- (b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (alama 2)
- (c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)
- (d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume? Thibitisha kauli hii. (alama 2)
- (e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii (alama 6)
- (f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 4)

SEHEMU E: Ushairi (alama 20)

Jibu swali la 7 au la 8

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatishika, utahisi kama kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvurugika myamba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na *kutamba*,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni kubwa sana, mfanowe kama nyumba,
Yazuka na kugongana, wala hatuna la *kwamba*,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
 Inarusha vilevile, *seuze hiyi migomba*
 Viumbe tu hali gani!

Ni kipi kilotuliya, tuwazeni na kudumba,
 Mandovu kiangaliya, yagongana na masimba,
 Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
 Walioko mikondoni, kila mmoja *asamba*,
 Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
 Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
 Itokee afueni!

(Shairi la ‘Tufani’ la Haji Gora Haji, katika *Tamthilia ya Maisha*, uk 62)

Maswali:

- (a) Taja na ueleze mikondo ya shairi hili (alama 4)
- (b) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)
- (c) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
- (d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
- (e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. (alama 3)
- (f) Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi . (alama 3)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mjibu wa shairi hili
 (i) Mdaduwa : _____
 (ii) Kutamba : _____

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Daima alfajiri na mapema
 Hunipitia na jembe na kotama
 Katika njia iendayo Kondeni
 Kama walivyofanya babuze zamani;
 Nimuonapo huwa anatabasamu
 Kama mtu aliye na hamu
 Kushika mpini na kuto ~~kw~~ jasho
 Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
 Videge vya anga vinavyotumbuiza
 Utadhani huwa vimemngojea
 Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
 Pia pepo baridi kumpepea
 Rihi ya maua zikimtetea
 Nao umande kumbusu miguuni;

Na miti yote hujipinda migogo
 Kumpapasa, kumtoa matongo;
 Na yeye kundelea kwa furaha
 Kuliko ye yote ninayemjua
 Akichekelea ha ha ha ha ha

3GR CLUSTER**MTIHANI WA PAMOJA WA
MUHULA WA KWANZA 2019****KIDATO CHA NNE****KISWAHILI KARATASI YA KWANZA (102/1)****INSHA**

Andika barua kwa mhariri wa gazeti ukilalamikia hali ya watu nchini kwetu kuhamia mataifa ya nje kwa wingi.

1. Andika kuhusu umuhimu wa vijana katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

2. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.

Usitukane wakunga na uzazi ungalipo

3. Tunga kisa kitakachokamilika kwa kauli ifuatayo:

“...niliipapia ile bilauri ya maji kwa pupa. Sikuwa na uhakika kuwa kiu yangu ingekatika. Nikapiga mafunda mawili, matatu. Baada ya kugumia bilauri yote, ndipo nilipotambua kuwa kweli maji ni uhai.”

MTIHANI WA PAMOJA WA 3GR MUHULA WA KWANZA 2019**KIDATO CHA NNE 2019****KISWAHILI – LUGHA****102/2****KARATASI 2****LUGHA**

1. **UFAHAMU**

(ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili ya mahuluki ni kuilewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vile vile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na. matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vagingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!” Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadarnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima.” Hata Marekani na Ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama Vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka. Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya ‘ mkereketwa wa Uafrika akachanganua.

Demokrasia ya Afrika basi imefuataa mkondo huu wa umwagikaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutaruta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati. Hali hil imesababisha maafa makubwa, uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimpenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa ainati, uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali. Huku mataifa mengi Ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyininge kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali ‘ Tutaendelea vipi na tunadhulimiwa na kaka wakubwa’. Siasa ya demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ultima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi

ambayo hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora, uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii uliosisiwa na Jean Jacques Rousseau.

Maswali

- a) Binadamu amechanganyika kwa njia ipi) (Alama 2)
- b) Ni vipi Demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa (Alama 2)
- c) Kwa nini inasemekana kuwa ‘Demokrasia ni mchezo wa mizengwe? (Alama 2)
- d) Ni athari gani hutokana na kinyang’anyiro cha Demokrasia? (Alama 4)
- e) “Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi-hewa wa wanasiasa” Eleza. (Alama 2)
- f) Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yaliviyotumika katika taarifa. (Alama 3)
- i) Mafahali
Wanatupikia majungu
Ukarabati

2. UFUPISHO

(ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata

Wakaazi wengi wa maeneo ya kitajiri miji yetu hawajui uswapo chini ya utawala wa machifu. Huenda wakasalia katika hali hii ya kutojua hadi wanapokosa kulipa ujira wa watumishi wao wa nyumbani halafu maskini mwajiriwa huyu anaripoti kwa chifu, kwa kuwa ni hali yake. Chifu ni uzi muhimu katika vazi la kijamii. Bila hawa maafisa, jamii kama tunavyoijua ingeporomoka. Wakati mwingine hawaungwi mkono. Mfano mzuri ni kukataliwa kwa katiba kielelezo cha Wako, Novembe 2005, wakati wa kura ya maoni. Kwa sababu jukumu la chifu au kibadala chake halikudhihirishwa wazi wazi katika kielelezo, wengi walikataa stakabadhi hiyo, wakihofia sasa hawataweza kufikia mtawala wao kushughulikia malalamishi yao.

Nimeishi mtaa wa Nairobi West miaka mingi na kuhudhuria kamati nyingi za lokesheni, chini ya uwenye kiti wa chifu akisaidiwa na naibu na wazee. Mikutano, pia inahudhuriwa na madiwani, inspeka wa askari tawala na wawakilishi wengi na washia dau katika lokesheni. Takribani kila swali linalogusia maslahi ya jamii linajadiliwa na kuchunguzwa na maazimio kupitishwa. Mada muhimu wakati wa mikutano hii ni usalama, taa za barabarani, ulanguzi wa mihadarati hasa karibu na taasisi za elimu, kudumisha usafi wa vyoo vya umma, kudumisha usalama kupitia kwa raia na swala nyeti la vioski.

Kazi ngumu ya chifu ni kuwazia kila kju. Kwa mfano, mwenye kioski ni sharti apate mkate wa kila siku na sehemu ya biashara yake iliyoko ni muhimu. Ikiwa kioski kitajengwa na kukiuka sheria za baraza la jiji au ikiwa wizi usiofahamika na utumizi wa dawa za kulevyta unatokea kufuatia kukua kwa idadi ya vioski katika eneo, shinikizo zinaelekezwa kukuwa kwa wenye vioski. Chifu lazima azingatie shinikizo za umma hatari za kiusalama na hofu za wenye vioski kabla ya kufanya uamuza ikiwa mijengo hiyo ibomolewe.

Tatizo jingine ni watoto wa barabarani. Makao ya kuwakimu ni machache kama walivyo wahudumu wa kijamii, suluhu ni nini? Tuwatupe katika ukumbi wa kijamii, ambao watahepa pindi *tu*, wapatapo fürsa ndogo au wapelekwe huduma kwa vijana wa Taifa, ambapo wachache wanawenza kutunzwa kwa wakati mmoja. Ili kufaulu kwa wengine, sharti wawe katika vituo vya urekebishaji tabia za matumizi ya dawa za kulevyta. Tuwakabidhi polisi kwa sababu wanaranda au tujaribu kuungana na vituo vya urekebishaji tabia kuhakikisha hawatarudi barabarani.

Mazingira ya lokesheni pia huibuka katika ajenda. Hali ya barabara, juhudzi za kusafisha mazingira, wizi wa maji na umeme, usafiri wa umma, uchafuzi wa mazingira, hewa na kelele, hii inatokea kupitia malalamishi ya watu wanaoishi karibu na mabaa na uzingativu wa saa ya biashara

hujadiliwa kila mara. Chifu ni sharti afahamu sheria na kanuni zinazotawala hali hizo, halafu ajadili na wahusika kabla ya kutoa mwelekeo. Usawa na uwazi katika kugawa fedha za Hazina ya maendeleo ya maeneo Bunge, pia hujadiliwa.

Katika maswala haya mengine, chifu ndiye aliye nyanjani. Anawajibikia jamii na wakubwa wake na hatarajii shukrani au kutambuliwa kwa kazi njema aliyofanya. Isipokuwa hukashifiwa anapofeli. Watu wengine wana taswira ya Chifu kama mtu kwenye jukwa, kofia yake. na kifimbo kinachompa mamlaka ya kuhutubia baraza, Kajubo tyji zaidi ya hivyo. Kwa mujibu wa kitabu cha mafunzo ya machifu na Naibu wao (Januari 2004), wajibu wa chifu ni kuwakilisha sera na mipango ya serikali kwa wananchi. Chifu ni ajenti wa “mabadiliko” mwenye wajibu Wa kuhamasisha watu katika maendeleo. Anajishughulisha na kujuu ni nani maskini katika lokesheni, mkoaa, mgonjwa asiyeweza kupata tiba na kupanga jinsi mhasiriwa atakavyopelekwa hospitali kama anavyoweza. Ni sharti ashughulikie ugomvi wa kinyumbani, uhalifu wa watoto, dhuluma za watoto, agawe chakula na mavazi kwa wahitaji na kuhukumu kesi ndogo za wizi na uharibifu. Chifu hutatua kesi za kisheria kwa wasioweza kumudu wakili. Wakati wananchi wanapohisi mbunge wao hafikiliki na hawana imani na polisi, chifu ndiye suluhisho.

Lakini kuna machifu wachache ambao hawafanyi kazi yao vyema. Kwa ufupi, chifu ni mkusanyiko wa kushngaza; mfalme katika himaya yake, pasta, baba msikivu, wanasaikolojia, mtunga sheria na mdumisha sheria, balozi mchaguzi, mama, mlumbi na askari asiyechelewa. Ingawa halipwi vyema, anafanya kazi bila tarakilishi, na aghalabu hujilipia gharama ya kodi ya afisi yake kutoka mfuko wake. Kwa sababu ni mtumishi wa *umma*, tunataraji afanye kazi mufti. Hiyo haimaanishi tusishukuru kwa kazi njema aliyofanya. Serikali inaweza kufanya hivi kwa kuimarisha hali yake ya kazi, mazingira yake ya kikazi, na kuhakikisha yana tarakilishi, anapata mafunzo ya uongozi na usimamizi. Wananchi sharti washukuru watu hawa kwa kujitolea sabili.

Maswali

- a) Fupisha aya nne za kwanza (Maneno 60) (Alama 6, mtiriko,1)
Matayarisho
Jibu
- b) Kwa maneno kati ya 80-90 fupisha ~~aya~~ ya ya tano hadi ya mwisho. (Alama 8, mtiririko 2)
Matayarisho
Jibu
- 3. **MATUMIZI YA LUGHA** (ALAMA 40)
 - a) i) Taja sauti mbili ~~ambazo~~ ni vikwamizo vya ufizi(Alama 1)
ii) Taja sifa mbili ~~bainifu~~ za vokali /u/ (Alama 2)
 - b) Yakinisha sentensi hii.
Simba asiponguruma wanyama wote hawababaiki. (Alama 2)
 - c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo uliyopewa.
Mbwa ambaye aliripotiwa kuwa ameibwa amepatikana katika bwawa la maji.
(Anza: Katika bwawa.....) (Alama 2)
 - d) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia njia ya matawi (Alama 4)
Mwanafunzi stadi amenunua kitabu kizuri.
 - e) Ukizingatia neno lililo katika mabano, andika sentensi hii katika hali ya kutotendeka.
i) Daraja hili(vuka) wakati wa mvua (Alama 2)
 - f) Andika katika ukubwa wingi (Alama 2)
Mtoto mjeuri akiletwa atarejeshwa kwao.
 - g) Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 2)
“Tutawatembelea wazazi wetu leo jioni” Leo alimwambia Asha.
 - h) Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi ____ingine (Alama 2)
 - i) dau
 - ii) urembo

- | | Kiswahili |
|---|---------------|
| i) Bainisha yambwa katika sentensi hii.
Mbunge wa Mtundo Kaskazini atawajengea wanakijiji josho kisha aghurie Nairobi. | (Alama 2) |
| j) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo.
i) Nafsi viambata
ii) Visisitizi | (Alama 2) |
| k) Fafanua maana ya sauti mwambatano. | (Alama 2) |
| i) Andika mfano wa sauti mwambatano. | (alama 1) |
| l) Tunga sentensi ya neno moja yenyе visehemu vifuatavyo vya sarufi. (Alama 3)
i) Kiambishi kiwakilishi cha kiima
ii) Kiambishi kiwakilishi cha wakati uliopo
iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendewa/mtendewa
iv) Shina la kitenzi
v) Kiambishi cha kauli ya kutendesha
v) Kauli ya kutenda | |
| m) Fafanua miundo miwili ya ngeli ya LI-YA | (Alama 2) |
| n) Akifisha
sikukuu ya madaaraka nilikwenda eldama ravine kumwona yohana akasema atakuja kuniona | (Alama 3) |
| o) Eleza tofauti za kimaana baina ya sentenzi hizi.
i) Jambazi kutoka dukani aliiba
ii) Kutoka dukani jambazi aliiba.
iii) Aliibia jambazi kutoka dukani.
ii) Jambazi aliiba kutoka dukani. | (Alama 4) |
| p) Unda nomino mbilimbili kutokana na mizizi ifuatayo.
i) -f-
ii) -l- | (Alama 2) |
| 4. ISIMU JAMII | (ALAMA |
| 10) | |
| a) Mbali na mtazamo unaoshikilia kuwa Kiswahili ni kibantu, taja mingine miwili. | (Alama 2) |
| b) Huku ukitoa mifano, thibitisha kuwa kiswahili ni kibantu. | (Alama 8) |

**KIDATO CHA NNE
MTIHANI WA PAMOJA WA3GR YEAR 2019
KISWAHILI
102/3**

- SEHEMU A. SWALI LA LAZIMA RIWAYA: CHOZI LA HERI**
1. "Lakini itakuwaje historical injustice,nawe Ridhaa,hapo ulipo sicho kitovu chako?"
 a. Eleza muktadha wa dondo.
 b. Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumika kwenye dondo hili.
 c. Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya.
 d. Ni mambo gani yaliyo wakumba wale ambao sio wa kitovu kinachorejelewa.
- SEHEMU B HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**
2. "Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto. Rudi,rudi kwa Mola wako."
 a) Eleza muktadha wa dondo hili.
 b) Fafanua sifa za msemewa.
 c) Tambua tamathali ya usemi iliyotumika hapo juu.
 d) Ni kwa nini msemewa anatakikana kurudi kwa Mola wake?
- AU
3. Huku ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatumaliza, fafanua maudhui ya ukiujaji wa haki.
- SEHEMU C. TAMTHILIA: KIGOGO**
4. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka....."
 a) Weka dondo hili katika muktadha wake.

Kiswahili

- b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi? (alama 8)
 c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu. (alama8)

AU

5. Tamthilia ya ‘Kigogo’ ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika.Thibitisha.(alama 20)

SEHEMU D: USHAIRI.

6. Lisome shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yaliyoulizwa.

WENYE VYAO WATUBANA

1. Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani.
Kwa sasa kilo va dona, bei mia ishirini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
2. Washindana matajiri -kwa bei siyo utani,
Na pigo kwa mafakiri tunao hali ya chini,
Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
Wakubwa tuteteeni,wenye vyao watubana
3. Limekuwa kubwa zogo, hakuendeki madukani.
Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
Huo mkubwa mzigo , watulemaza kichwani,
Wakubwa tuteteeni ,wenye vyao watubana.
4. Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni
Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
Wakubwa tuteteeni ,wenye vyao watubana.
5. Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini.
Wachuuzi hawacheki , zimewatoka huzuni,
Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
Wakubwa tuteteeni , wenye vyao watubana.
6. Maisha yetu viumbe ,yamekuwa hilakini,
Vvenye vyao kila pembe ,wametukaa shingoni,
Nyama ya mbuzi na ng’ombe, sasa hali maskini,
Wakubwa tuteteeni wenve vyao watubana.
7. Maji vamezidi unga, kwa lodi wadarajani,
Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,
Mvao wake wa kanga,ni shilingi elifeni
Wakubwa tuteteeni,wenye vvaao watubana.

Maswali;

- a) Fafanua toni ya shairi hili. (alama2)
 - b) Nini dhamira ya nafsi neni ? (alama2)
 - c) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (alama4)
 - d) Fafanua kwa kutoa mfano mbinu moja aliyotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya arudhi katika shairi hili. (alama2)
 - e) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia. (alama4)
 - i) Vipande
 - ii) Vina
 - f) Taja kwa kutoa mifano katika shairi hili hadhira tatu lengwa. (alama6)
- SEHEMU E : FASIH SIMULIZI**
7. (a) (i) Ngano ni nini? (alama1)
 - (ii) Eleza tofauti iliyoko kati ya visasili na visakale. (alama2)
 - (iii) Fafanua umuhimu wa ulumbi katika jamii. (alama5)

Downloaded for free at www.EasyKCEPapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

COMPLIANT I**FORM FOUR END OF TERM TWO EXAM 2019**

102/1

KISWAHILI

Karatasi 1

(Insha)

1. Wewe ni mwanahabari katika shirika la Tangaza. Andika mahojiano kati yako na waziri wa Kilimo nchini kuhusu athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabili tatizo hili. (alama 20)
2. Ufisadi umekita mizizi nchini Kenya. Jadili madhara yake huku ukipendekeza suluhi. (alama 20)
3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali : **Mchelea mwana kulia, hulia yeye.** (alama 20)
4. Andika insha itakayomalizia kwa :
.... walipofungua mlango huo hatimaye wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. (alama 20)

COMPLIANT I

102/2

KISWAHILI

Karatasi 2

1. UFAHAMU**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulangazi wa dawa za kulevyta.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyakazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwangi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masorovaya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambaao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwininge hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambaao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambaao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii.

Ufisadi **umekita** mizizi na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenyewe bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelizwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambaa hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

Maswali

- a) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. (alama 4)
- b) Kulingana na kifungu ulichosoma, ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? (alama 2)
- c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? (alama 3)
- d) Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini ? (alama 2)
- e) Toa msamiati mwingine wenyewe maana sawa na rushwa. (alama 1)
- f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumiwa kifunguni:
 - i) shamiri
 - ii) waliohasiriwa
 - iii) wakilia ngoa

2. MUHTASARI (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa.

Taifa la Kenya limekuwa na tatizo la njaa kwa muda mrefu na hili ni tatizo ambalo hutokea mwaka baada ya mwaka. Kuna sababu kadhaa ambazo zimelifanya tatizo hili likithiri. Wananchi wengi hutegema ukulima kujipatia pato pamoja na chakula. Jambo hili limekuwa shida kubwa kwa vile kilimo hutegemea mvua isiyotabirika. Watabiri wa hali ya hewa huwashauri wakulima wapande mbegu zitakazohimili jua lakini mvua nayo inakuwa nydingi na kuharibu mimea.

Bidhaa za ukulima kama mbegu za kupanda, mbolea, dawa za kunyunyizia n.k, zimekuwa ghali. Kuna sehemu kubwa ya ardhi ambayo ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo. Mazao yanayotolewa shambani hayahifadhiwi vizuri. Mengine yanaharibikia shambani na mengine yanavamiwa na wadudu kiasi kwamba hayawezi kutumika.

Tatizo lingine ni vita vya kikabila. Kabilia tofauti zinapopigana, watu huhama na kuacha mashamba ilhali wengine huchoma maghala ya chakula. Wafanyabiashara pamoja na serikali huwanunulia wakulima mazao yao kwa bei ya chini sana mpaka wanakosa shauku ya kuyashughulikia mashamba yao. Siku hizi wakulima hawashughuliki tena kuzuia mmomonyoko wa udongo. Hivvo mvua inaponyesha rotuba yote inachukuliwa. Serikali haina sera mwafaka za kukabiliana na njaa. Hii ndiyo sababu sehemu zingine kama Turkana zimekabiliwa na njaa kwa muda mrefu.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa ikiwa wakulima wataelimishwa juu ya mbinu bora za ukulima. Pia wakulima waishio katika sehemu ambazo hazina mvua ya kutosha wapewe mbegu ambazo zitahimili kiangazi. Ukulima wa kunyunuzia mimea maji unafaa kuzingatiwa. Mazao yanayotolewa shambani yahifadhiwe vizuri kwa kuwekwa dawa za kuwaaua wadudu.

Sehemu kubwa za ardhi ambazo hazitumiwi zitolewe kwa kilimo. Ni muhimu wakulima waelimishwe kuhusu jinsi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na umuhimu wake. Wakulima wanunuliwe mazao yao kwa bei nafuu ili wajibidiishe katika kazi yao. Serikali inafaa iwe na sera mwafaka ili iweze kutatua tatizo hilo ambalo limekuwa ni janga kuu.

- a) Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 70) (alama 8)
Nakala chafu
Nakala safi
- b) Fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 60) (alama 7)
Nakala chafu
Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

- a) Eleza tofauti kati ya sauti
 i) | d |
 ii) | t |
- b) Andika maneno yenyne miundo ifuatayo: (alama 2)
 i) KKKI
 ii) ll
- c) Andikakatikaumoja. (alama 2)
 Machaka haya hayazai maua meusi
- d) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (alama 2)
 Dada aliinama na akasimama ndani ya nyumba.
- e) Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii: (alama 2)
 Ijapokuwa ni mgonjwa tutamwandalia karamu leo.
- f) Bainisha matumizi ya ‘ki’ katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Kitoto hiki kilinichezea kijinga.
- g) Tumia neno ‘mle’ kwenye sentensi kama : (alama 3)
 i) kivumishi
 ii) kiwakilishi
 iii) kielezi
- h) Andika katika ukubwa. (alama 2)
 Kiti kilichokuwa kimebebwaa na mvulana kilivunjika.
- i) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
 Atieno alijengewa nyumba na mamake kwa matofali.
- j) Changanua sentensi hii kwa kutumia mtindo wa jedwali. (alama 4)
 Wanafunzi wageni waliofika shulenii mapema walibeba vitabu vingi ajabu.
- k) Eleza maana ya dhana ya chagizo kisha uonyeshe kwa kupigia mstari chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
 Mkuliwa hodari zaidi atatuzwa kwa bidii yake.
- l) Kwa kutoa mifano katika sentensi, onyesha matumizi mawili ya kistari kifupi. (alama 2)
- m) Andika katika usemi halisi. (alama 3)
 Mwalimu aliwasitisizia wanafunzi kuwa kulikuwa na umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hilo lingeongeza siku zao duniani.
- n) Tunga sentensi sahihi ukitumia hali ya ‘a’ isiyodhahirika. (alama 2)
- o) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
 Wazazi walikuwa wangali harusini.
- p) Tumia o-rejeshi badala ya amba. (alama 2)
 Wachezaji ambao huchenza kwa bidii ndio ambao hufaulu maishani.
- q) Nyambua kitenzi ‘ja’ katika kauli ya kutendewa. (alama 1)
- r) Nimenunua dawa ili iwamalize wadudu wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani. (alama 2)
 Aanza: Wadudu

4. ISIMUJAMII

“Anachukua mpira, kisingino anataliza, kengeuka, kulia, kushoto, hesabu wa kwanza tesa wa pili, baki peke yake na goalkeeper.

- a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)
- b) Fafanua sifa za sajili hii. (alama 8)

COMPLIANT I**102/3****KISWAHILI****Karatasi 3****SEHEMU A : USHAIRI****1. Soma shairi lifuatato kwa makini kisha ujibu maswali.**

Niokoa Muokozi, uniondolee mashaka
 Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
 Nimekithiri simanzi, ni katika kuudhika
 Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
 Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
 Naomba hisikitika, na mikono hiinua
 Mtenda ndiwe Moliwa, nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe Moliwa, we ndiwe Mola wa anga
 Mazito kuyaondoa, pamoja na kuyatenga
 Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunga
 Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Muwanga nikundulia, nipate toka kizani
 Na huzuni n'ondolea, itoke mwangu moyoni
 Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani
 Nitendea we Manani, nipate niyatakayo

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
 Nili katika dunia, kwa afia na uzima
 Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
 Nifurahike mtima, nipate niyatakayo

- a) Shairi hili ni bahari gani ? Eleza. (alama 2)
- b) Taja madhumini ya shairi hili. (alama 3)
- c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
- d) Thibitisha namna uhuru wa kishairi unaibuka katika shairi. (alama 4)
- e) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari. (alama 4)
- f) Toa maana ya :
 - i) Nimedhikika
 - ii) Muwanga nikundulia
 - iii) Nifurahike mtima
 (alama 3)

SEHEMU B : RIWAYA**Assumpta K. Matei : Chozi la heri****Jibu swali la 2 au la 3****2. "Vipi, binadamu anavyowenza kuyazoa maji yaliyomwagika?"**

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)
- c) Jadili sifa tatu za msemaji. (alama 3)
- d) Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya. (alama 11)

Au**3. Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika riwaya ya Chozi la heri.**

(alama 20)

SEHEMU C : TAMTHILIA**Pauline Kea : Kigogo****Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Ukitaka kuwafurusha ndege, kata mti. Hawa wangekuwa sasa wametuliza nafsi zao.
 a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)
 b) Tambua mbinu mbili za uandishi zilizotumika. (alama 4)
 c) Onyesha jinsi wahusika kadhaa walivyofurushwa kama ndege. (alama 12)

Au

5. Tamthilia ya Kigogo ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani Afrika. Fafanua ukirejelea tamthilia nzima. (alama 20)

SEHEMU D**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine****Jibu swali la 6 au la 7**

6. Ukierejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza. (alama 20)
 a) Mapenzi ya kifaurongo
 b) Masharti ya kisasa
 c) Ndoto ya Mashaka
 d) Mtihani wa maisha

Au**Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad**

7. "Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?"
 a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
 b) Eleza sifa za msemaji. (alama 6)
 c) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

8. a) Miviga ni nini ? (alama 2)
 b) Fafanua sifa zozote sita za miviga. (alama 12)
 c) Miviga ina majukumu yapi katika jamii ? (alama 6)

Provided for free by www.freekcsepapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

MTIHANI WA KASSU WA 2019
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA

1. Wewe ni mtangazaji wa kituo cha utangazaji cha Uzalendo. Studioni umetembelewa na mwanamke mtetezi wa haki za wanawake kuzungumzia namna mwanamke ametelekezwa katika jamii ya sasa. Andika mahojiano kuhusu mchakato huo. (Alama 20)
2. Kuna njia anuai zinazoweza kutumiwa kulitandarukia tatizo la ajira nchini. Tetea. (Alama 20)
3. Andika kisa kinachoafiki methali; **Mgagaa na upwa hali wali mkavu.** (Alama 20)
4. Tunga kisa kitakacho kamilika kwa kauli ifuatayo;
...niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka. Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi wangu, lakini kitumbua changu kilikuwa kimeingia mchanga (Alama 20)

MTIHANI WA KASSU WA 2019
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
LUGHA

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Yasemekana kuwa Shungwaya ndicho kitovu cha watu waishio Giriama katika janibu za pwani ya Kenya na wanaojulikana kwa jumla kana Wamijikenda. Yaaminika kuwa bado wakiwa Shugwaya, walimuua Mgalla mmoja mwenyeji wa Shungwaya na kitendo hicho kiliamsha hasira kali za Wagalla, hata ikawawia vigumu Wamijikenda kuishi kwa usalama pamoja na ndugu zao hao.

Hata hivyo, Wamijikenda hawakugura mara moja wala wote kwa pamoja bali walihama katika vipindi tofauti na katika makundi madogomadogo. Kila kundi lililofika Giriama lilijenga ‘kaya’ au mji wake. Kwa jumla, walihama kwa makundi tisa.

Vile vile, Wamijikenda walihama na fingo yao ambayo ilifukiwa na viongozi wao katikati ya kaya zao, palipokuwa na msitu mdogo. Hakuna ajuaye hasa mahali ilipofukiwa ila wazee hao waliopenda kufanya baraza mahali hapo.

Mnamo mwaka wa 1870, mzee Menza na mkewe walibarikiwa kufungua kizazi kwa kupata mtoto wa kike waliyemwita Mekatilili. Walimlea vizuri na alipoanza kuzungumza, alionyesha dalili za kuwa na kipawa cha pekee. Kwanza, alipenda kujua kila kitu kilichoihusu jamii yake na pili alichukizwa sana na kiumbe aliyemdhulumu kiumbe mwenzake. Kwa mfano, aliwaoneea vipepeo imani walipoliwa na ndege. Tena alizipenda sana mila na desturi za watu wa jamii yake – Wamijikenda.

Siku moja, baada ya Mekatilili kufikia utu uzima, mama yake alimwita chemba akamwambia, “Mwanangu sasa umeshabalehe, nami ningependa kuwaona wajukuu wangu kabla sijawafuata wazee waliotangulia. Waonaje tukkuoza? Mimi na baba yako tumepata mume ambaye ni kufu yako kabisa.”

“Ninaelewa, maana hizi ni desturi zetu, lakini ningefurahi zaidi kama mngeniruhusu nijichagulie mume ninayempenda.” Binti alimjibu mamaye.

“Mnazi na uwe mrefu, huyumba kufuata upepo.” Mama akajibu. Tangu hapo binti akawa hana la kujibu ila kukubali.

Siku ya harusi, watu wengi walihudhuria na wakastarehe kwa tembo la mnazi ambalo lilikuwa limetengenezewa kwa wingi. Jioni hiyo, mekatilili alichukuliwa kwa mumewe Masendeni, karibu na mto Sabaki. Ikawa hangeonana na wazazi wake kila siku kama ingalivyokuwa mapenzi yake. Wakati huu kote nchini Kenya kulikuwa kumejaaa wagoni, wengi wao wakiwa walowezi na watawala wa kibeberu. Walikuwa wameanzisha mashamba ya mikonge, kahawa na chai. Walihitaji watu wa kupalilia mashamba yao hayo. Hata hivyo Waafrika hawakuwa na haja ya kulima wala pesa. Hata walipolima, ni kwa minajili ya kubadilishana mazao na kula. Iliwabidi Wazungu kutumia mizungu ili kuwashurutisha Waafrika kuwalimia. Baadhi ya mikakati waliyobuni ni kuwateka nyara watu barobaro na kutoza kodi. Ni katika harakati kama hizo ambapo mumewe Mekatilili alitekwa, asirudi tena kwake. Wakati uo huo, wazazi wa Mekatilili waliaga dunia.

Mambo haya yalimpa mekatilili msukumo. Baada ya muda wa kuomboleza kuisha, alijiunga na wazee wapigania ukombozi, mmoja wao akiwa Wanje, kakaye mume. Aliwaunganisha wanawake na kuwashimiza wasiige mila na desturi za kizungu. Aliwahutubia wanaume na kuwakumbusha kuwa ilikuwa lazima wailinde nchi yao. Siku moja alishikwa kwa kuwalisha watu kiapo. Alipelekwa bara, Kisii, mbali kabisa na kwao, Masharibi mwa Kenya na akatiwa kizuizini pamoja na Wanje. Hata hivyo, walifaulu kutoroka na kwa muda wa siku ayami walipitia kwenye mabonde na milima, misitu na nyika hadi wakarudi Giriama.

Mabeberu walikasirika sana. Hata hivyo, walikuwa wamechelewa. Katika safari yao kurudi Giriama, walifaulu kuhubiria wengi dhidi ya mgeni. Vita vyta ukombozi vilikuwa vimeshika.

Maswali

1. Ni kwa nini Wagirama wanajulikana kama Wamijikenda? (al.1)
2. Ni maafa gani yaliyompata Mekatilili katika maisha yake? (al.4)
3. Ni hali gani inayotawala katika makala haya. (al.2)
4. Taja masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika Makala haya. (al.2)
5. Wazungu walitumia mbinu gani ili kuwashurutisha watu kuwafanya kazi mashambani mwao. (al.2)
6. Andika maneno mengine yeney maana sawa na;
 - i) Kugura..... (al.1)
 - ii) Kubalehe..... (al.1)
7. Eleza maana ya;
 - i) Mnazi na uwe mrefu huyumba kufuata upepo (al.1)
 - ii) Kitovu cha watu waishio Giriama (al.1)

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kiswahili tunasema ni lugha yetu kwa sababu ndiyo lugha ya Kiafrika inayoongewa katika nchi nyingi Barani Afrika. Ni lugha yetu kwa sababu ni lugha asilia mojawapo za Afrika. Siyo lugha iliyoletwa na watu wa nchi za nje kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Uzuri wa Kiswahili sasa ni kuwa kimeenea kote Afrika Mashariki na Kati.

Wenyeji asilia waliokuwa wakiongea lugha hii tangu awali ni Waswahili. Waswahili hawa hata leo wako na wanaendelea kuitumia lugha hii kama lugha yao ya mama, kama vile Wakikuyu watumiavyo Kikuyu, Wakamba, Kikamba na Wadigo lugha ya Kidigo. Makao yao Waswahili tangu jadi yanapatikana kaunti ya Pwani. Makao yao yameanzia upande wa Kaskazini Mashariki ya Kenya, na wanapakana na nchi ya Somalia huko. Wameenea katika upwa huo wa Pwani, ikiwamo Lamu, Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Visiwa vya Ngazija na kuendelea.

Lugha ya Kiswahili ina lajaja nyingi kulingana na sehemu wanamoishi. Kwa mfano, Waswahili wa Lamu huongea lajaja ya Kiswahili inayoitwa Kiamu. Waswahili wa Mombasa huongea lajaja ya Kimvita. Pemba wanaongea Kipemba, Ngazija lajaja ya Kingazija, Unguja lajaja ya Kiunguja na kadhalika. Kutokana na lajaja hizi na nyinginezo za Kiswahili ambazo hazikutajwa hapo, wataalamu wa lugha walitokea na Kiswahili sanifu. Hiki Kiswahili sanifu ndicho kitumiwacho katika mafunzo ya shule, uandishi wa vitabu na mawasiliano ya kiserikali na kibiashara.

Nchini Kenya, kwa muda mrefu Kiswahili hakikuthaminiwa kama Lugha ya Kiingereza. Sababu mojawapo ni kuwa Kiswahili hakikufanya somo la lazima katika rasimu za shule, wala kutahiniwa katika shule za msingi. Hata katika shule za upili, katika kufunzwa na kutahiniwa hakikupewa umuhimu wowote. Kwa ajili hii wanafunzi wengi waliacha kujifunza Kiswahili kama somo. Hali hiyo ilifanya Kiswahili kuonekana kama lugha inayoongewa na wale watu wasio na kisomo ama elimu nyingi. Kwa ajili ya fikira hizi, watu wengi wamekuwa wakikichukia, kukidunisha na kujaribu kuongea Kiingereza kila nafasi inapojoitekeza.

Miaka michache iliyopita, Kiswahili kilianza kutiliwa mkazo katika shughuli zote nchini Kenya. Kwa upande wa msimamo wa nchi lugha hii ilionekana yenye manufaa katika kuleta umoja na kuwaunganisha wananchi wote. Jambo hili ni muhimu kwa maendeleo ya nchi iwayo yote. Umoja huleta maelewano na undugu. Hali hizi mbili zinapokuwapo, amani husambaa nchini mote.

Tukitazama mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili kimepewa nafasi sawa katika ratiba za shule kama lugha ya Kiingereza. Kiswahili kinatahiniwa kama somo muhimu kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili. Kinyume na enzi za zamani, siku hizi mwanafunzi anayesoma Kiswahili, hata asipofaulu vizuri katika lugha ya Kingereza ana nafasi sawa ya kupata kazi kama wengine.

Maswali

- a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 80. (alama 7)
Matayarisho
Jibu
- b) Eleza vile Kiswahili hakikuthaminiwa na namna hali hii inavyobadilika. (alama 8)
Matayarisho
Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

- (a) Toa **maelezo** ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. (alama 2)
 - i) /p/.
 - ii) /ch/.
 - iii) /m/
 - iv) /r/
- (b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. (alama 1)
- (c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi shirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. (alama 3)
- (d) Tumia neno **mji** kama **kielezi cha mfanano**. (alama 1)
- (e) Onyesha **namna tatu** za kutumia kiambishi “ji” katika **sentensi moja**, kisha ueleze **matumizi** husika. (alama 3)
- (f) Ziweke nomino hizi katika **ngeli** zake. (alama 2)
 - i) waya
 - ii) Kilembwe
- (g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya **aina** gani kisha uonyeshe **miundo** yake. (alama 4)
 - (i) Kikapu kilichofumwa juzi kitauzwa marikiti.

- (ii) Wenzetu walikuwa wakijinaki kabla ya dimba.
- (h) Eleza **maana mbili** za sentensi: Zainabu alisema atakusaidia. **(alama 2)**
- (i) Onyesha **majuku** ya mofimu katika neno: awaliaye **(alama 3)**
- (j) **Andika kinyume:** Aliangika picha ukutani baada ya sherehe. **(alama 2)**
- (k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kutumia kiambishi ku. **(alama 2)**
- i) Tuma
 - ii) Pinda
- (l) Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. **(alama 2)**
- (m) Andika kwa usemi wa taarifa: “Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu”, mpishi alalamika. **(alama 2)**
- (n) Tumia **visanduku** kuchanganua sentensi ifuatayo: Alipotuona alitupuuza, lakini sisi tulimsalimia. **(alama 4)**
- (o) Tumia vitate vya jua, toa na baka katika sentensi **tatu tofauti**. **(alama 3)**
- (p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka.
- (i) Ameanguka matopeni.
 - (ii) Mlango ulibishwa
- (q) Tofautisha sentensi. **(alama 2)**
- (i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.
 - (ii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

4. ISIMU JAMII (Alama 10)

Maswali

- a) “..... unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa”
- i) Bainisha sajili ya mazungumzo haya. **(al.1)**
 - ii) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. **(al.4)**
- b) Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa. **(al.5)**

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

SWALI LA LAZIMA

CHOZI LA HERI – A MATEI

“Maisha yangu yalijaa ~~shubiri~~ tangu utotonii.”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(al. 4)**
- b) Kwa kutolea mfano, bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika kauli hii. **(al.2)**
- c) Jadili athari za vita katika jumuia ya Chozi la Heri **(al. 14)**

TAMTHILIA – KIGOGO - P – KEYA

Jibu swali 2 au 3

2. Siwezi mimi, siwezi, sitaki kuwa gurudumu la akiba hujayaacha hayo?

- a) Eleza muktadha wa dondoo **(al.4)**
- b) Eleza sifa nne za msemaji wa kauli hii **(al.4)**
- c) Tambua matumizi 12 ya jazanda katika tamthilia **(al. 12)**

AU

3. Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulamu kuna gharama yake. Ukirolelea tamthilia ya Kigogo, ipatie nguvu kauli hii. **(al. 20)**

HADITHI FUPI – TUMBO LISILOSHIBA – ALFA C / DUMU K.

Jibu swali 4 au 5

Nizikeni papa hapa – Ken Walibora

4. “Ndugu yangu tahadhari na hawa.....”
- a) Eleza muktadha wa dondoo **(al.4)**

- | | |
|--|---------------------|
| b) Eleza sifa za msemewa | Kiswahili
(al.4) |
| c) Taja na ufanue maudhui sita katika hadithi hii | (al.12) |
| AU | |
| 5. a) Tulipokutana Tena – Alfa Chokocho
Jadili jinsi maudhui ya umaskini yalivyoshughulikiwa katika hadithi ya ‘Tulipokutana Tena’. | (al. 10) |
| Mame Bakari | |
| b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na change moto nyingi. Tetea. | (al. 10) |

USHAIRI

jIbu swali 6 au 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng’oo! Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yejote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyew!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mweyewe!

Maswali

- a) Eleza dhamira ya shairi hili
- b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake.
- c) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi.
- d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari/tutumbi
- e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili
- f) Bainisha toni ya shairi hili
- g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi
 - i) mstahiki
 - ii) hupuliki

SHAIRI**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nikiwa na njaa na matambara mwilini

Nimehudumika kama hayawani

Kupigwa na kutukanwa

Kimya kama kupita kwa shetani

Nafasi ya kupumzika hakuna

 Ya kulala hakuna

 Ya kuwaza hakuna

Basi kwani hili kufanyika

Ni kosa gani lilotendeka

Liloniletea adhabu hii isomalizika?

Ewe mwewe urukaye juu angani

Wajua lililomo mwangu moyoni

Niambie pale mipunga inapopepea

Ikatema miale ya juu

Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?

Je nadhari hujitokeza usoni

Ikielekea huku kizuizini?

Mpenzi mama, nitarudi nyumbani

Nitarudi hata kama ni kifoni

Hata kama maiti yangu imekatikakatika

 Vipande elfu, elfu kumi

 Nitarudi nyumbani

Nikipenya kwenye ukuta huu

Nikipitia mwingine kama shetani

Nitarudi mpenzi mama...

Hata kama kifoni.

Maswali

- a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.1)
- b) Tambua nafsineni katika shairi hili (al.2)
- c) Eleza toni katika shairi hili (al.2)
- d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (al.4)
- e) Fafanua dhamira katika shairi hili (al 2)
- f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (al 2)
- g) Taja na ufanue sifa mbili za mshairi (al 2)
- h) Fafanua mbinu 3 za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (al 3)
- i) Eleza maana ya maneno yafuatoyo kama yaliviyotumiwa katika shairi hili (al 2)
 - i) Hayawani
 - ii) Nadhari

FASIHI SIMULIZI

- a) Maudhui na Fani ya maigizo hutegemea mwigizaji. Thibitisha kwa hoja tano. (al. 5)
- b) Taja aina mbili za miviga (al. 2)

**KIGUMO
JARIBIO LA JULAI 2019 KIDATO CHA NNE.
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
KIDATO CHA NNE
JULAI /AGOSTI 2019**

1. Lazima

Wewe ni mionganini mwa wanahabari wanaomhoji Inspekte Jenerali wa Polisi katika ofisi yake. Andika mahojiano yenu juu ya hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha viwango vyaa usalama nchini.

2. Jadili umuhimu wa michezo kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya.
3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali hii.
Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno haya: ... ilinichukua muda mrefu mno kuyaamini yaliyonifika.

**KIGUMO
KISWAHILI
LUGHA
JARIBIO LA JULAI 2019 KIDATO CHA NNE**

1. UFAHAMU:(Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Meli alipokivuka kizingiti cha langoo la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemeewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenyepato wastani. Akasoma kwa juhudii za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini, au kupidia somo la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijambia kwamba kwa vyovoyote vile atapambana na maisha haya mapya.

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili ya mja yeoyote aliymfahamu. Alijhisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo aliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudii zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleafaji wajitumbukizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelewa katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata mionganini mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, "wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho"! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeze katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele dasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha** na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahuisha wataalamu wa ushauri nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyadumu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahuisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda Zaidi Meli ni shughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za mziki, ukariri wa mashairi na drama. Mazungumzo yilibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji Zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shulenii.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. Aliukata kabisa uhusiano wake na marafiki waliompotosha na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

- a) “Wanafunzi wawapo shuleni hukumbana na changamoto nyingi”. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa. (alama 6)
- b) Eleza mchango wa washikadau mbalimbali katika kumsaidia Meli kupata ufanisi masomoni. (alama 4)
- c) Bainisha mbinu **tatu** za lugha ambazo msimulizi anatumia katika kuwasilisha ujumbe wake katika kifungu. (alama 3)
- d) i. Andika kisawe cha ‘**kujipurukusha**’ kwa mujibu wa taarifa (alama 1)
ii. Andika maana ya ‘**kuwatania**’ kulingana na taarifa. (alama 1)

2 UFUPISHO: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mfumo wa elimu nchini unatilia mkazo mafunzo mengine ambayo, japo yamo nje ya masomo ya kawaida, yanahusiana na kwenda sambamba na masomo hayo ya kawaida. Vyama vya wanafunzi shuleni vinachangia pakubwa kuitisha mafunzo haya ya ziada.

Vyama vya wanafunzi hutofautiana kulingana na majukumu. Mathalani, vipo vyama vya kidini, vya kitaaluma na vya michezo. Pia, kuna vyama vya kijamii kama vile Chama cha kupambana na matumizi mabaya ya dawa na vya kiuchumi kama vile chama cha Wakulima Chipukizi.

Inadhihirika kwamba vyama vya wanafunzi vina manufaa ya kuhusudiwa. Hii ndiyo sababu shuleni, kila wanafunzi anahimizwa kujiunga na angaa vyama viwili. Vyama vya wanafunzi huwasaidia kukuza vipawa na kuimarishti stadi za kujiyeza. Haya hufikiwa kuititia kwa shughuli za vyama kama vile ukariri wa mashairi mijadala, utegaji na uteguaji wa vitendawili, chemsha bongo na ulumbi. Aidha, vyama hivi huhimiza utangamano mionganii mwa wanachama kwani wao hujiona kuwa watu wenye mwelekeo mmoja. Vilevile utangamano wa kitaifa na kimataifa hujengeka.

Mwanafunzi ambaye amejiunga na vyama vya wanafunzi huweza kukabiliana na changamoto za maisha kuliko yule ambaye hajawahi kujiunga na chama chochote. Katika vyama hivi, wanafunzi hufunzana mikakati na maarifa ya kutatua matatizo na mbinu za kuepuka mitego ya ujana. Kuititia kwa ushauri wa marika kwa mfano, mwanafunzi hushauriwa kuhusu masuala kama vile uteuzi wa marafiki, kuratibu muda, kujikubali na kuwakubali wenzake.

Halikadhalika, mwanafunzi hujifunza maadili ya kijamii na kidini. Kupitia kwa vyama vya kidini na vinginevyo, yeye hujifunza kujistahi na kuwa na stahamala ya kidini, kiitikadi na kikabila. Kadhalika, majukumu ambayo mwanafunzi huenda akapewa hupalilia uwajibikaji, uaminifu na kipawa cha uongozi. Hata anapohitimu masomo yake, mwanafunzi huyu huendeleza sifa hizi.

Vijana wana nafasi kubwa katika kukabiliana na maovu ya kijamii kwani wao ndio wengi Zaidi. Kupitia kwa vyama hivi, wanafunzi wanaweza kuwahamasisha wenza dhidi ya tabia hasi kama vile kushiriki mapenzi kiholela, ulangazi wa dawa za kulevyta na kuijingiza katika burudani zisizofaa. Pia, shughuli na miradi ya vyama hivi huwawezesha wanafunzi kutumia nishati zao kwa njia ya kujinufaisha na kuepuka maovu. Kwa mfano, wanaweza kwenda kukwea milima, kufanya matembezi ya kukusanya pesa za kuwafadhili wahitaji, kuendeleza shughuli za kunadhifisha mazingira na kutembelea vituo vya mayatima na wazee.

Kushiriki katika vyama vya michezo hakumwezeshi mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli tu, bali pia huweza kuwa msingi wa kupata chanzo cha riziki baadaye. Wapo wachezaji maarufu amba walitambua na kuviendoeleza vipawa vyao kupitia kwa vyama aina hii, na hivi sasa wana uwezo wa kuyaendesha maisha yao na ya familia zao.

Ifahamike kuwa vyama vya wanafunzi vinapaswa kuwa msingi wa mshikamano na maridhiano. Visitumiwe kama vyombo vya kuwagawa wanafunzi kitabaka. Mwanafunzi hana budi kusawazisha muda anaotumia. Atenge muda wa shughuli za vyama na wa kudurusu masomo yake.

- a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 80
Matayarisho
Nakala Safi (alamu 9,1 ya utiririko)
- b) Fafanua masuala ambayo mwandisi anaibua katika aya tatu za mwisho (maneno 60). (alamu 6, 1 ya mtiririko)
Matayarisho
Nakala Safi
- 3. MATUMIZI YA LUGHA:** (Alamu 40)
 - a) Andika sauti zenyne sifa zifuatazo: (alamu 2)
 - i) nazali ya kaakaa gumu.....
 - ii) kikwamizo ghuna cha kaakaa laini.....
 - iii) irabu ya mbele, wastani.....
 - iv) kiyeyusho cha midomo.....
 - b) Bainisha silabi katika neno: wachangamshwavyo. (alamu 1)
 - c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi. Wachezaji wote watafanyiwa ukaguzi ili kupata suluhi ya matatizo hayo. (alamu 2)
 - d) Andika sentensi ifuatavyo katika umoja. Tukishiriki katika maigizo hayo vizuri tutaweza kujishindia tuzo. (alamu 2)
 - e) Andika neno **moja** lenye **vimbajengo** vifuatavyo: (alamu 2)
 - nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendesha, kauli tenda
 - f) Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: ni (alamu 2)
 - i) kitenzi
 - ii) kiwakilishi
 - g) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. (alamu 2)
 - h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. Nyundo hizo zimetupwa mbali na jumba lile. (alamu 1)
 - i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: Nomino ya wingi, kivumishi, kitenzi kishirikishi, kivumishi (alamu 2)
 - j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. Matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili yana virutubishi vingi. (alamu 1)
 - Anza kwa: Virutubishi vingi
 - k) Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mstari. Mzee atatembelea mji (alamu 1)
 - l) Akifikisha sentensi ifuatayo: basi mwanangu akasema cheusi hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia gender parity wewe waonaje (alamu 3)
 - m) Uganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati.

Kiswahili

- | | |
|--|-----------|
| Idi alijishindia tuzo. Idi alishiriki katika uhifadhi wa mazingira. | (alama 1) |
| n) Tumia ‘kwa’ katika sentensi kuonyesha: | (alama 2) |
| i) nia | |
| ii) pamoja na | |
| o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.
Upepo ulivuma tulipokuwa tukiondoka. | (alama 3) |
| p) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.
Rono alicheza gitaa akiwa kwa Kiprono. | (alama 2) |
| q) Onyesha matumizi ya ka katika sentensi ifuatayo:
Mumbi alitia embe kapuni likaiva. | (alama 1) |
| r) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea.
Mmomonyoko wa udongo ulipozuiliwa mashamba yalinawiri. | (alama 2) |
| s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya baba na papa | (alama 2) |
| t) Methali: Haraka haraka haina baraka huambiwa mtu aliye na kasi isiyofaa katika kutenda mambo. Mtu anayepuuza shida za wenzake huambiwa aje? | (alama 1) |
| u) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo:
Wale wageni walikipenda sana. | (alama 1) |
| v) Andika kihisishi cha kuitikia wito kwa mtu wa jinsia ya kike | (al 1) |
| w) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba tendo lilifanikiwa kwa sababu ya kufanikiwa kwa tendo lingine. | (alama 1) |
| x) Andika miundo miwili ya nomino katika ngeli ya KI-VI. | (alama 1) |
| y) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari. | (alama 1) |
| Zana hizi zimeundwa <u>na mafundi wenye ustadi mkubwa</u> . | |

4. ISIMU JAMII: (Alama 10)

- | | |
|---|-----------|
| a) Umepewa jukumu la kutoa ushauri nasaha(elekezi) kwa kijana mwenzako anayefikiria kujitao uhai kuhusu manufaa ya kutojitoa uhai. Fafanua sifa tano za kimtindo utakazotumia ili kufanikisha mazungumzo yako. | (alama 5) |
| b) Eleza mitindo mitano ya matumizi ya lugha katika muktadha wa bunge. | (alama 5) |

KIGUMO**102/3 KISWAHILI – Karatasi ya 3****FASIHI****JARIBIO LA JULAI 2019****SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI****1. Lazima**

”Mwanangu nakuomba uzingatie uadilifu maishani uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu...”

- | | |
|---|---------|
| i) Tambua kipera na utanbu wa tungo hili | (al. 2) |
| ii) Kwa kutumia hoja mbili eleza muundo wa kipera hiki | (al. 2) |
| iii) Fafanua sifa nane za kipera hiki | (al.8) |
| a) Eleza vikwazo vinane vya ukuaji wa fasihi simulizi. | (al.8) |

SEHEMU B: RIWAYA

Assumpata k. matei: : chozi la Heri

Jibu swalii la 2 au la 3

- | | |
|--|---------|
| 2. ”Si kufua, si kupiga deki, si kupika...almuradi kila siku na adha”
a) Eleza muktadha wa kauli hii. | (ala.4) |
| a) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. | (al.2) |
| b) Kwa kutumia hoja kumi na nne , eleza maudhui yaliyodokezwa na dondoo hili. | (al.14) |
| 3. ”Kila mara hujiuliza ikiwa watoto huwa na hadhi tofauti nje au ndani ya ndoa” | |

SEHEMU C: TAMTHILIA

P. Kea : Kigogo

Jibu swal la 4 au la 5

4. "Acha porojo zako. Kigogo hachezewi;watafuta maangamizi!"
 a) Eleza muktadha wa dondo hili (al.4)
 b) Fafanua sifa za mzungumzaji (al.6)
 c) Kwa kurejelea hoja **kumi**, thibitisha kwamba kucheza na kigogo anayerejewa ni sawa na kutafuta maangamizi (al.10)
5. "Tunahitaji kuandika historia yetu upya."
 a)Eleza sababu **kumi na mbili** kuonyesha kwa nini ilikuwa muhimu kuiandika historia ya sagamoyo upya (al.12)
 b)Onyesha mikakati inayotumiwa kuiandika upya historia ya Jumuiya ya sagamoyo (al.8)

SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swal la 6 au la 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

LONGA

Longa longea afwaji, watabusarika

Longa uwape noleji, watanusurika

Longa nenea mabubu,sema na viduko

Longa usichachawizwe, tamka maneno

Longa usitatanizwe, mbwa aso meno

Longa usidakihiizwe,kishindo cha funo

Longa yote si uasi, si tengen si noma

Longa pasi wasiwasi,ongea kalima

Longa ukuli kwa kasi, likate mtima

Longa zungumza basi, liume ja uma

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa

Longa liume wakora, kwani wezi ni wa

Longa bangu na parara, hawakuitiwa

Longa bunge si kiwara, si medani tawa

Longa ni simba marara, wanaturaruwa.

Maswali

- a) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili (al.1)
 b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivytumika kukidhi mahitaji ya kiarudhi (al.4)
 c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumika na mtunzi kwenye shairi hili. (al.4)
 d) Eleza aina **tatu** za urudiaji katika shairi (al.3)
 e) Tambua na ueleze **toni** ya shairi (al.2)
 f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivytumika katika shairi.
 i. Afwaji
 ii. Tenge
 g) Eleza umbo la shairi hili. (al.4)

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Kila nikaapo husikia tama

Na kuwazia hali inayonizunguka

Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Hujiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu jinsia ya kike
Hukaa na kujidadisi
Hujidadisi kujuua ni kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Wezangu hawanishiki mikono
Bali wanandharau kwa kuikosea utamaduni

Hukaa na kujiuliza
Iwapi raha yangu ulimwengu huu?
Iwapi jamaa nzimaa ya wanawake?
Maswali

- a) Taja sifa **mbili** za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili (al.2)
 - b) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
 - c) Kwa kutoa mifano, eleza maana ya mistari mishata (al.3)
 - d) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumika katika shairi hili (al.4)
 - e) Eleza nafsineni katika shairi hiri (al.2)
 - f) Tambua **toni** ya shairi hili (al.2)
 - g) Taja maudhui **matatu** katika shairi hili (al.3)
 - h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumiwa katika shairi (al.2)
- Madhila
Kudhalilishwa

SEHEMU E: HADITHI FUPI

A. Chokocho na D kayanda : Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine.

8.”...hamna mwendawazimu wala mahoka kati yetu, mimi nimepewa zawadi hizo”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili (al.4)
- b) Eleza sifa nne za msemaji (al.4)
- c) Hakiki nafasi ya maudhui ya busara kwa mujibu wa hadithi hii (al.12)

KIGUMO

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI KARATASI 102/1 2019

1. Hii ni insha ya mahojiano na ni utungaji wa kiuamailifu. Vipengele viwili vyta utungo wa aina hii vizingatiwe, yaani **muundo na maudhui**.

a) Muundo

- Vipengele vikuu vyta mahojiano.
- Anwani (kutokana na mada).
- Atumie mfumo wa kitamthilia.
- Mtahiniwa ndiye mhoji hivyo basi yeye ndiye atakayeuliza maswali. Inspekte Jenerali ndiye mhojiwa.
- Mahojiano yaanze kwa maamkuzi baina ya wahusika.
Mwili wa insha ubebe maudhui.

b) Maudhui (Hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha usalama nchini)

- Kuimarisha mfumo wa ‘Nyumba Kumi’ mitaani, vijiji ni nk.
- Kuongeza idadi ya askari polisi kufikia kiwango cha kimataifa cha askari mmoja kwa raia mia nne.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA MATUNGU**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari****KISWAHILI****Karatasi ya 1****INSHA****MASWALI****LAZIMA**

- (1) Andika hotuba kuhusu matatizo ya maji kijiji ni mwenu na suluhu yake utakayoitoa katika sherehe ya maji duniani.
- (2) “Ufisadi ndicho kikwazo kikubwa katika maendeleo ya uchumi wa taifa lolote.” Thibitisha.
- (3) Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali, “Jifya moja haliinjiki chungu.”
- (4) Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo:- aliyakumbuka mashauri ya mamake ambayo aliyakaidi. Machozi yalimbubujika alipojiona kadhoofika kiafya jinsi ile; mguu mmoja duniani mwine kaburini.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA MATUNGU**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari****102/2****KISWAHILI KARATASI YA 2****LUGHA****SEHEMU YA KWANZA – UFAHAMU – ALAMA 15**

Kwa wale wanaopenda kusema uongo, siku zao zinaendelea kuwa chache kila kukicha. Teknolojia na wanasaikolojia wanaendelea kuvumbua njia na mbinu mbali mbali za uongo katika uso wa ulimwengu.

Kwanza, wataalamu sasa wanasema kuwa kumwangalia mtu usoni mnazungumza moja kwa moja ni njia muhimu ya kutathmini kama mtu anasema ukweli ama la. Inasemekana kuwa majaji na mahakimu huitumia njia hii na kuamua kesi. Aidha, wapelelezi pia huitumia wanapodekua habari kutoka kwa washukiwa. Kuna chombo maalum ambacho pia husaidia kuonyesha ubongo wa mtu unavyokwenda na kuonyesha kama anasema ukweli ama la.

Sasa, wataalamu wanapendekera njia za kujua kama mtu anasema uongo ama ukweli. Kwanza, ni muhimu kuangalia jinsi mtu anayezungumza anavyotabasamu. Iwapo anatabasamu kwa njia ya kulazimishwa, basi kuna uwezekano mtu huyo anasema uongo. Mtu kama huyo ataonekana kutokuwa stadi na kama mwenye kulazimishwa kulifanya jambo, hali ambayo ni muhali katika maisha ya kawaida.

Pili, ni muhimu kuangalia mikono na mguu yake. Mtu anayesema uongo ataonekana kuwa na mikono na mguu isiyoweza kusonga kwa haraka na inayoonekana kutatizwa kila mara anapotaka kusongeza kama katika kueleza jambo. Mikono hiyo inaweza kutumika kupangusa uso, pua, ama sikio lakini haiwezi kugusa kifua kwa urahisi.

Ni muhimu kuzingatia kama anayezungumza nawe anatokwa jasho jembamba ama la. Watu wengi wanapodanganya huwa wanatokwa na jasho jekejeke. Wakati kama huu wanaosema uongo huongeza masuala mengi ambayo hukuwauiza kama njia ya kukushawishi.

Zingatia jinsi mtu anayezungumza anavyosongeza macho yake. Mtu anayedanganya hapendi kumwangalia anayemdanganya machoni moja kwa moja. Wanaosema uongo pia hupenda kupepesapepesa macho kwa haraka. Watu hupenda sana kuangalia kushoto (wakikumbuka yaliyotendeka hasa, taswira yake) na upande wa kulia (wakiunda taswira bandia) kuhusu yaliyotokea.

Ni muhimu pia kuzingatia jinsi anayesema chochote anavyoonyesha hisia zake wakati anaotumia kufanya hivyo, jambo ambalo si dhahiri mtu anapodanganya. Hisia hucheleweshwa, hubakia kwa muda mrefu kuliko kawaida, halafu zikakatizwa ghafla. Vile vile, hisia hizo huenda zisiambatane na yanayosemwa. Kwa upande wa kutabasamu, huenda hisia zinazojitokeza usoni zижийиyeshe mdomoni na si kwingine kwa mtu anayedanganya.

Wataalamu wanasema kuwa mtu anayedanganya hupigwa kumbo kukatwakatwa maini na maswali huku akitikisa kichwa kuchelea kuyajibu maswali moja kwa moja. Jibu la kweli linakuja moja kwa moja kwani liko

akilini. Maneno anayotumia na jinsi ambavyo ameyapanga ni ishara nyingine ya kuonyesha muongo. Watu waongo hutumia maneno uliyotumia kuuliza swali, hawajibu swali moja kwa moja, husema sana, hawabadiishi kiimbo na shada, na hawatumii viwakilishi na hutumia ucheshi ili kudanganya.

MASWALI

- (i) Kwa nini mwandishi anasema kuwa dunia itakuwa ngumu kwa wanaopenda kudanganya? (al.2)
- (ii) Ni kwa nini uso wa mwongo ni njia rahisi ya kushika? (al.4)
- (iii) Mbali na mtazamo wa uso, eleza sifa zingine zinazotambulisha mwongo (al.5)
- (iv) Wataalamu wanasema nini kuhusu kutumia hisia za mtu anayesema uongo? (al.2)
- (v) Eleza maana ya msamati huu kama ulivyotumika katika taarifa (al.2)
 - i) Muhalii
 - ii) Hupigwa kumbo

SEHEMU YA PILI – MUHTASARI – ALAMA 15

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema ‘maarifa ni nguvu’.

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutoptaka na uwezo wa:kuyadhibiti, kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: ‘Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani’.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenye hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wakuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenye hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawazi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyambua maarifa yenye kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa hulingana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhalii mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo hufanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa kuwa na maana kinapoweka sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno ‘mwerevu’ huweza kuwa na maana kwa kuweka katika muktadha wa ‘mjinga,’ mjanja, ‘hodari’ na kadhalika.

Maarifa hayawazi kuhifadhiwa katika nafsi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu ambazo zingehitaji maelefu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawazi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenye, ni muhalii kuyadhibiti maarifa yenye.

Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za ueneaji wa maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

MASWALI

- (a) Fafanua aya ya pili naya tatu (maneno 55 – 60) (al.5, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Nakala safi
- (b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi ya nane (maneno 100 – 110) (al.10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

SEHEMU YA TATU – MATUMIZI YA LUGHA – ALAMA 40

- a) Taja sauti ambazo ni: (al.2)
 - i. Vokali ya mbele, juu tandazwa

- ii. Kikwamizo cha kaakaa gumu
- b) Bainisha viambishi awali katika kitenzi kifuatacho: (al.2)
Hawakulivuna
- c) Tambua vitenzi katika sentensi zifuatazo: (al.2)
- i) Mwalimu amekuwa darasani
 - ii) Mtoto huyu hajawahi kuandika insha
- d) Tunga sentansi ukitumia kielezi cha namna mfanano (al.2)
- e) Eleza matumizi ya ritifaa katika sentensi ifuatayo (al.1)
Bara'bara hii ilijengwa ba'rabara
- f) Yakinisha kwa umoja (al.2)
Wabunge wasipojenga madarasa shulenii hawatatuza
- g) Tunga sentensi moja kubaini maana ya vitate hivi: (al.2)
ShabaSaba
- h) Andika kwa wingi (al.2)
- i) Ukucha uu huu utakatwa
 - ii) Kalamu iyo hiyo inaandika vizuri
- j) Tumia **hadi** katika sentensi kama kihuishi cha: (al.2)
- i) Wakati
 - ii) Mahali
- k) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo (al.2)
Hadithi iliyotambiwa watoto ni nzuri
- l) Andika kwa wingi (al.2)
Mbuzi hawa wamerarua kikapu
- m) Andika sentensi inayoafiki uchanganuzi ufuatao.
- n) Tunga sentensi yenye kirai Nomino chenye muundo wa N + V + E (al.2)
- o) Tambua vivumishi vilivyotumika katika sentensi ifuatayo; (al.2)
Maziwa yote yalinyewa na watoto wadogo
- p) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo; (al.2)
Ubovu wa kazi yao ulifichuka kabla ya kumalizika kwa mradi ule.
- q) Eleza matumizi ya kiambishi 'KU' katika sentensi ifuatayo. (al.2)
Amekulalamikia kwa nini? Omari hakuoa jana!
- r) Unda kitenzi kutokana na nomino zifuatazo; (al.2)
- a. Zawadi
 - ii) Fisadi ...
- s) Yaweke maneno haya katika ngeli zake: (al.2)
- i) Kiwavi
 - ii) Tarakilishi
- t) Neno 'chungu' lina maana – enye kutohuwa na tamu. Eleza maana zake zingine mbili. (al.2)
- u) Eleza maana ya msemo: 'pasulia mbarika!' (al.2)
- SWALI LA NNE – ISIMU JAMII – ALAMA 10**
- a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimu jamii (al.2).
- i) Lugha sanifu
 - ii) Lugha taifa
- b) Ni matatizo gani yanayokumba ukuaji wa Kiswahili nchini Kenya? (al.6)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA MATUNGU**102/3****KISWAHILI KARATASI YA 3 -
FASIHI****SEHEMU A - USHAIRI**

(1) Walo nacho hawachi

Mshangao kunitia

Moyoni wakakutia

pindi waonapo

we u chambo cha

kuvutia raslimali

huko kwenye vina

Hawachi

Kukwinamisha

Kukupindisha mgongo

Ndoana umeshika

Kuvulia yao riziki

(2) Wakakwita kwa majina

ya hadhi

ya kupembeja

ya kukwaminisha

kwamba we na wao mu

wamoja

hali zenu

kama sahani na kawa

wakakwonyesha wao

nawe

mwachumia jungu moja

yenu matarajio ni mamoja

watakwhidi halua

kila tunu wakakwashiria

mradi nyoyo zao zimemaizi

we u nundu

ya kukamulia mafuta

we u ndovu

wa mti kugonga

makoma kuangusha

wafaidi wao.

(3) Mabepari wana mambo

ukiwa yao makasia

ya kulientesha dau lao

majini lielee

miamba kulepusha

Watakusifu

Watakuchajiisha

mbele utunge

machoyo yenyeye ari

huku wanakufunga nira

ja fahali

mali kuwazalishia

Provided for free by www.freekcsepapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

huku kipato wakupimia
kwa kibaba
usipate kukidhi haja
usipate kujamini
kuwategemea uzidi.

- (4) Hawa ni wa kuajabiwa
Watakupa yao kazi
Mpangilio wa kazi
wakukabidhi wao
na malengo wakupe
La! Hawakupi!
Wanakuhusisha
katika kuyavyaza
na muda wa kuyafikia
nao mwaafikiana
ati kuna makubaliano bayana
ambayo ubatizo wayo ni
kandarasi ya utendakazi.
Ela we nao mnajua
ndo kigezo cha kupimia
wako uwajibikaji
wako mchango chunguni
yako thamani
na usidhani una hiari ya
kuamua tapofika
Watakusukuma
Kufikia yao shabaha
bila kuwazia
ujira wanokupa.
Watakuhimiza
kutumia chako kipawa
kuikoza nundu yao mafuta
Viumbe hawa!
Mabepari – waajiri.

MASWALI

- a) Eleza mikakati sita inayotumiwa na waajiri kujikuza kiuchumi. (ala6)
- b) Bainisha tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (ala3)
- c) Huku ukitoa mifano, bainisha aina mbili za uhuru wa kishairi alizotumia mshairi (ala2)
- d) Andika mifano miwili ya mistari mishata katika shairi hili (ala2)
- e) Bainisha nafsi neni katika shairi hili (ala1)
- f) Fafanua toni ya shairi hili (ala2)
- g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (ala4)

SEHEMU B – HADITHI FUPI – TUMBO LISIOSHIBA

2. ‘Mwanamke bado ana kilio.’ Jadili kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo (ala20)
(a) Mama Bakari

- (ii) Ndoto ya Mashaka
- (iii) Mwalimu Mustaafuli

AU

3. Jamii zimekiuka haki kwa namna mbali mbali. Jadili kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote nne (ala20)

SEHEMU C – TAMTHILIA – KIGOGO

4. “Ukitaka kuongoza Sagamoyo lazima uwe na ngozi ngumu” (al. 4)
a) Adhiria muktadha wa dondo hili

Downloaded for free by www.freekcsepapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

Kiswahili

- b) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo (al. 10)
 c) Jadili jinsi ubinafsi ulivyoathiri uongozi wa Sagamoyo (al. 6)
- AU**
5. “Sudi hatanikosesha usingizi, laiti angalijua salamu zinazomsubiri”
 a) Kwa kurejelea tamthilia eleza namna wahusika wengine watano walivyosubiriwa na salamu (ala10)
 b) Eleza namna mwandishi amefanikisha matumizi ya taswira katika tamthilia ya Kigogo (al. 10)

SEHEMU YA D – RIWAYA – CHOZI LA HERI

6. Mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri amekomaa katika matumizi ya kisengere nyuma. Eleza (ala20)
AU
7. “Haikuwa ibra hata kuuziwa kipande cha ardhi ambacho tayari kilikuwa kimeuzwa na mtu akapewa hatimiliki bandia.”
 a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala4)
 b) Eleza sifa zozote sita za msemaji (ala6)
 c) Tambua na ueleze maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili (ala10)

SEHEMU YA E – FASIH SIMULIZI

- I) Tofautisha vipera vifuatavyo (ala6)
 a. Pembejezi na bembelezi
 b. Misimu na misimbo
 c. Mighani na maghani
 b) Soma utungo ufuataao kisha ujibu maswali
 Ndimi Mwimo mdumishaji ukoopi
 Ndimi ndovu mtetemeshaji ardhi
 Aliyepigana vita, ukoo kuauni
 Ziliporindima zangu nyayo
 Adui alinywea, mafahali na mitamba akatukabidhi
 Kwenye misitu sikua na kifani
 Paa na hata visungura
 Vilijikabidhi kwangu
 Kwa kuinusa tu mata
 Nani aliywahi
 Ngomani kunipiku?
 Makoo hawakunisifu, wakalilia nikaha?
 Kwenye nyanja za michuano
 Nani angedhubutu, ndaro kunipigia?
 Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi, hata kabla hatujavaana?

MASWALI

- a) Hii ni aina ya sifo? Eleza (ala1)
 b) Taja aina ya sifa inayoendelezwaa na utungo huu (ala1)
 c) Bainisha shughuli mbili mbili zinazoendelezwaa na jamii hii
 i. Za kiuchumi (ala2)
 ii. Za kijamii (ala2)
 d) Eleza mambo manne yanayoweza kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu (ala4)
 c) Ushairi simulizi ulijikita katika matukio gani katika jamii? (ala4)

MERU SOUTH
102/1
KISWAHILI KARATASI YA KWANZA
INSHA
KIDATO CHA NNE
JULAI/AGOSTI 2019

INSHA PAPER 1
KIDATO CHA NNE

1. Wewe ni mwanahabari wa gazeti la Tomoko Leo. Umemtembelea Mkuu wa Idara ya kupambana na ufisadi Bwana Ridhaa ili kumhoji kuhusu sababu za watu kushiriki ufisadi na suluhihi. Andika mahojiano yenu.
2. Andika insha kuhusu mambo yanayoathiri utaifa au umoja na utangamano katika nchi ya Kenya.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.
Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:
... Nilipiga darubini kuhusu mawaidha niliyopewa ya mama yangu. Machozi yalinitirika njia mbilimbili. Utabiri wa mama ulikuwa umetimu.

MERUU SOUTH
102/2
KISWAHILI
KIDATO CHA NNE
JULAI/AGOSTI 2019

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI – 2019
UFAHAMU (ALAMA 20)

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali

Inasemekana kuwa uongozi hutoka kwa Maulana. Siku hizi, kauli hii inaonekana kinyume na inapingwa vikali na mahuluki wengi. Hali hii imetokana na ukweli kuwa viongozi wengi wamekuwa katili. Wengi wao hutekeleza maovu bila kujali wala kubali. Kiongozi yeoyote Yule anayedai kuwa mwema hana budi kuwa **mwongofu** na wa kuaminika; anafaa kuwa kielelezo kwa wafuasi wake. Hili lisipotendeka **vurumai** huzuka mionganoni mwa watu.

Kiongozi bora sharti awe mnyenyeketu. Mtu mwenye mashauo si kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii huwahudumia watu kwa moyo wake wote. Jambo hili huwfanya watu waridhike. Watu wengi hawapendi viongozi wanaojipigia debe kila wakati. Viongozi kama hawa huwachosha na hata kuwachusha wafuasi wao. Matokeo ya haya yote huwa ni majuto kwa raia huku wakijuliza kilichowafanya wawachague.

Maadili ni sifa nyingine inayomtambulisha kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii hafai kujihusisha na vitendo vya kikatili kama matumizi ya mabavu, mauaji na hata ufisadi. Anafaa kuwajibika kazini na kuwa tayari kuyasikiliza malalamishi ya watu anaohudumia. Inamlazimu kiongozi bora kuwaheshimu wananchi bila kuzingatia vyeo vyao; asidharau maoni yao kuhusu jinsi ya kuuboresha uongozi wake.

Pia, kiongozi bora anastahili kuwa na huruma. Hii inamaanisha kuwa anafaa kuwa tayari kuwaonea **kite** wananchi wanaotatizika maishani. Anafaa kubuni mikakati ya **kuwaauni** watu kama hawa. Hali hii huwfanya watu waongeze imani yao kwa kiongozi kama huyu. Ikiwa kiongozi atajitia hamnazo anapofahamishwa kuhusu

masaibu ya wananchi, watu watatamani siku ya kumtoa mamlakani ama kwa kupiga kura au kumwomba Jalali ahitimishe uongozi wake haraka iwezekanavyo.

Utetezi wa kazi za wanyonge ni sifa nyingine muruwa ya kiongozi bora. Kiongozi kama huyu anapaswa kuwa tayari kuhakikisha kuwa sheria inafuatwa katika himaya yake. Hali hii huwfanya wanajamii kupata haki zao bila **kubughudhiwa**. Wale wasiopata haki wanazostahili wanastahili kuchunguwa maslahi na kiongozi kama huyu.

Hakuna mtu anayestahili kuitwa kiongozi bora kama si mpenda amani. Kiongozi anayepalilia rabsha katika jamii hafaulu hata kidogo kuitwa kiongozi bora. Ni wajibu wa kiongozi kusuluhisha ugomvi wowote uliomo mionganii mwa wanajamii. Jambo hili huifanya kunawiri na kuzagaa kote kote.

Wanajamii wakiishi katika mazingira yenye amani huweza kutekeleza shughuli zao bila hofu wala kindubwendumbwe.

Kiongozi bora anastahili kujitenga na ubaguzi kama ardhi na mbingu. Ni ukweli usiopingika kuwa baadhi ya viongozi huwabagua wananchi kwa misingi ya kitabaka, kijinsia na kikabila. Ni muhimu kwa kiongozi yeoyote Yule kuhakikisha kuwa kuna umoja wa wananchi katika jamii. Hii ni kutokana na ukweli kuwa jifya moja haliwezi kuinjika chungu. Astahili kuhubiri umoja katika hatamu ya uongozi wake. Nao wananchi humkumbuka daina dawamu.

Uwajibikaji ni kitambulishi kingine cha kiongozi aali. Kiongozi bora anafaa kuwajibiki kazini. Kiongozi anayestahili ni Yule ambaye anatekeleza majukumu yake kikamilifu. Suala la upigaji zohali ni muhalii kwa kiongozi wa aina hii. Ni mtu anayefanya kazi kimhangi ili kuboresha maisha yake naya wateja wake.

Kiongozi yeoyote asiyehu na hulka tulizzungumzia huishia kuwa hasimu wa watu. Viongozi wote wanastahili kuyapa kipaumbele maslahi ya umma. Hawafai kuwa wabinafisi. Ni watu wenye utu, maarifa, waongofu na wenye bidii. Wananchi wana wajibu wa kuwachagua viongozi wanaofaa bila kupofushwa na ahadi za uongo.

Maswali

- (a) Kwa nini kauli kuwa, ‘uongozi hutoka kwa maulana’, yaonekana kinaya na kipingwa na watu wengi. (ala.1)
- (b) Eleza kiini cha watu wengi kuchukia viongozi wanaojisifu kila wakati. (ala.2)
- © Eleza matokeo ya kiongozi kuwasaidia wananchi wanaotatizika maishani. (ala.1)
- (d) Taja misingi mitatu inayotumiwa na baadhi ya viongozi kuwabagua wananchi. (ala.3)
- (e) Eleza maoni ya mwandishi kuhusu jukumu la wananchi kuhakikisha kuwa uongozi bora umedumu. (ala.1)
- (f) Taja vitambulishi vine vya kiongozi bora. (ala.4)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyotumika katika kifungu. (ala.3)
 - (i) Mwongo
 - (ii) Kuwauni
 - (iii) Kite

2. UFUPISHO

Ni dhahiri shahiri kwamba **uharamia** umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki.

Taarifa za uharamia zimejawala vyombo vya habari, kiasi kwamba haipii siku bila kuripotiwa visa vipyta vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia wan chi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kuatiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dar –es salaam mnamo Agosti 7,1998 na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwagine, ukosefu wa tawala-wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umasikini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na ‘kinyume mbele’. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudini za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaraansa kunaelekea kuzipiga jeki juhudini za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wan chi kunachipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu wa ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeza ustawi wa uchumi.

Dosari hii inaelekeea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya millennia yanayositiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhalii kwa utali kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudini za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mmmwambao zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati kabambe na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa. Maswali

1. Fupishaaya mbili za kwanza kwa maneno 70. (alama 8,1 ya mtiririko)

MATAYARISHO

JIBU

- (b) Onyesha jinsi ambavyo Kenya imeathiriwa na uharamia na namna hali hii inatia hofu. Maneno 60. (alama 7,1 ya mtiririko)

MATAYARISHO

JIBU

SEHEMU YA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- (a) Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 2)
 (i) King'ong'o cha mdomo:-----
 (ii) Irabu ya mbele kati:-----
 (iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini:-----
 (iv) Kikwamizo sighuna cha menoni:-----
- (b) Dhihirisha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama 2)
 (i) itwa
 (ii) Mchwa
- © Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiakifishi (alama 2)
 Vifungo
- (d) Andika sentensi ukitumia: (alama 2)
 (i) Kihusishi cha ulinganisho
 (ii) Kihisishi cha furaha
- (e) Tunga sentensi ya neno moja iliyo na muundo ufuatao. (alama 2)
 (i) Nafsi
 (ii) Mzizi
 (iii) kauli
 (iv) Kirejeshi
- (f) Eleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
 (i) Chakula chochote kitaliwa na watoto.
 (ii) Chakula chote kitaliwa na watoto.
- (g) Kwa kutunga sentensi mwafaka onyesha aina tatu za yambwa. (alama 3)
- (h) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 3)
 "Tutamtia mbaroni mhalifu huyo sasa hivi" Askari akasema.
- (i) Ainisha matumizi ya kiambishi "ji" katika sentensi (alama 3)
 Jibwa hilo liliweza kujinusuru kutokana na hasira za mkimbajaji.
- (j) Changanya kwa Jedwali. (alama 4)
 Otii ambaye hucheza mpira ni kijana mkali.
- (k) Tofautisha vitate vifuatavyo kwa kuvitungia sentensi moja. (alama 2)
 (i) Hawara:-----
 (ii) Hawala:-----
- (L) Bumba ni kwa nyuki-----ni kwa samaki na-----

- Kiswahili (alama 2)
- ni kwa siafu.
- (m) Andika methali inayojumuisha ujumbe ufuataao.** Hata mtaalamu huhitaji kutafuta msaada wa wataalamu wenzake. (alama 1)
- (n) Unda kitenzi kutokana na nomino zifuatazo.** (alama 2)
- (i)Aina:-----
(ii)Moto-----
- (O) Onyesha matumizi ya ‘kwa’ katika sentensi.** (alama 2)
- (i)Kwao kunawaka moto.
(ii) Magaidi walitoroka kwa kasi.
- (P) Nyambua katika kauli kwenye mabano.** (alama 2)
- (i)Tua (tendama)
(ii) Pwa (tendeka)
- (q) Badilisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu.** (alama 2)
- Mama huwapikia watoto chakula.
- (r) Tumia neno ‘kesho’ kutungia sentensi kama:** (alama 2)
- (i)Nomino
(ii) kielezi:-----

SEHEMU D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)

Lugha ya magazeti husheheni upekee wa aina fulani. Eleza sifa za lugha hii kisha uleze upekee huu hukusudia nini?

MERU SOUTH

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WAPILI – KIDATO CHA NNE

KISWAHILI –KARATASI YA 3 (FASIHI) MUDA: SAA 2 ½

SEHEMU A(SWALI LA LAZIMA)

A: USHAIRI

Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali

1.

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
 Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
 Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
 Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
 Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenyе dini, wamtioo wahabu
 Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
 Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
 Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
 Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
 Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
 Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
 Cha wenyе raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. (alama 1)
- b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 2)
- c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivytumika katika shairi. (alama 2)
- d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama 4)
- e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
- f) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
- g) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
- h) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 2)
- i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumika katika shairi. (alama 2)
 - (i) Malofa:
 - (ii) Udubu:

SEHEMU YA B: RIWAYA: CHOZI LA HERI – ASSUMPTA K. MATEI

Jibu swalı la 2 au la 3

2. “Lakini itakuaje historical injustice, nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?
 - (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
 - (b) Taja na utpe mifano ya mbinu za sanaa zilizotumika katika dondo hili. (alama 4)
 - (c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 2)
 - (d) Ni mambo gani yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho. (alama 10)
3. Uozo wa maadili ya jamii umekithiri katika Riwaya ya Chozi la heri, Fafanua ukweli wa usemi huu. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA: KIGOGO – PAULINE KEA

Jibu swalı la 4 au la 5

4. “Asante ya punda kweli ni mateke. Sikujua ungekuja kunihangaisha.....”
 - (a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (alama 4)
 - (b) Onyesha jinsi msemewa anamhangaisha msemaji. (alama 2)
 - (c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha ukweli wa methali “Asante ya punda ni mateke. (alama 14)
5. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya Kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi. (alama 20)
 - (a) Jazanda
 - (b) Majazi

SEHEMU D; HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE.

6. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya ‘Tumbo Lisiloshiba na hadithi Nyingine’, jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

TATHMINI YA PAMOJA –KAUNTI NDOGO**YA KIRINYAGA MASHARIKI****KISWAHILI – KARATASI YA 1 – 102/1****INSHA****JULAI 2019 – MUDA: SAA: 1 $\frac{3}{4}$** **1. Lazima**

Wewe ni mhariri wa gazeti la Mzalendo. Andika tahariri kuhusu athari za mitandao ya kijamii kwa wanafunzi wa shule nchini Kenya.

2. Unywaji wa pombe haramu una madhara mengi.

Fafanua.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Nazi mbovu harabu ya nzima.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa kauli ifuatayo:

Nilipigwa na butwaa nilipomwona, sikujua nifurahi au nihuzunike....

TATHMINI YA PAMOJA –KAUNTI NDOGO YA KIRINYAGA MASHARIKI**KISWAHILI – KARATASI YA 2 – 102/2****LUGHA****JULAI 2019 – MUDA: SAA: 2 $\frac{1}{2}$** **1. SEHEMU A: UFAHAMU (Alama. 15)*****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

“Asubuhi moja alinipata ndani ya afisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu, Bi. Tamasha, alisikiliza kadhia yangu kwa makini. Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi.

‘Unaweza kuanza masomo katika darasa la pili. Nitamwomba mzazi mmojaakupe hifadhi,’ alisema Bi. Tamasha. Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha yangu katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Bwana Tenge na mkewe, Kimai, walinchukua kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajua je na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkafahamiana na kunguni wake? Ninayowaambia ni asilimia ndogo mino ya niliyoyaona. Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hichohicho kimoja; ndicho cha malazi, ndicho cha mapokezi, ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvunguni mwa kitanda cha wazazi.

“Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka *danguro* wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za *kisaikolojia* nilizozipata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigomkubwa kwa wahisani wangu. Si kwamba waja hawa walinibagua, la! Kusema hivyo kutakuwa kuwapaka *mashizi* bure. Hata hivyo nilihisi kwamba nimepata mbavu za kufanya angaa kibarua kidogo, na kuwatua wawili hawa mzigo wa kuninunulia sare na madaftari.

“Nilianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kufanya kazi kabla ya kwenda shulenii saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipitia huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwingine kwa marafiki wanfu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipoufanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

“Wakati huo Bwana Tenge alikuwa ameisha kupewa uhamisho, akaenda kufanya kazi katika shamba lingine. Ndivyo wafanyakazi hawa; kuhamishwa kila uchao bila mtu kuwazia kwamba wana watoto wanaoenda shule, na kwamba kuhamahama huku kunawavurugia masomo wana hawa.”

Maswali

- i) Eleza namna wazazi wanavyoweza kuchangia katika kuzorotesha maadili ya watoto katika jamii. (alama 2)
- ii) Onyesha namna haki za watoto zilivyokiukwa katika kifungu. (alama 3)
- iii) Wafanyakazi wa kima kidogo hupitia dhiki zipi kulingana na kifungu? (alama 3)
- iv) Eleza sifa **tatu** za mkewe Tenge – Kimai. (alama 3)

Kiswahili

- v) Eleza namna ndoa inavyosawiriwa katika kifungu. (alama 2)
 vi) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)
 (a) Danguro
 (b) Kisaikolojia

2. SEHEMU B: UFUPISHO (Alama 15)***Soma kifungu kisha ujibu maswali.***

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha. Kuna mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu, na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti. Wakati katiba ilipopitishwa mwaka wa 2010, Wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuvi ungewatatalia matatizo ambayo walikuwa wakipitia katika tawala zilizotangulia, hasa katika maeneo yaliyotengwa kimaendeleo.

Miaka tisa baadaye, kuna mafanikio ambayo yamepatikana ila hatua

kubwa zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha maisha ya aina raia kama mianya inayotumiwa kufuja pesa za umma itazibwa. Wizi huu unaojumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingi hupeanwa kwa jamaa na marafiki wao, ni sharti ukomeshwe mara moja.

Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuvi ilhali ukweli ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee. Changamoto za ugatuvi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo huu wa uongozi kushawishi wananchi na hata wahisani wasishughulike kuchangia katika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka walizopewa kwa manufaa ya raia. Tume ya maadili ya kupamban ana ujisadi (EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka, kwa kushukiwa kufuji mali za umma. Tungependa asasi zote zinazohusika na masuala ya kupambana na uhalifu, pamoja na wadau wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasifumbie macho maovu yanayotendwa katika kaunti zetu.

Nchi hii inatawalwa kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeoyote anayekiuka sheria anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka aliyoshikilia. Ni kuitia adhabu kali za kisheria pekee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee, watakuwa wametoa nafasi ya ufuaji kwa viongozi wapya kila miaka mitano.

(Kutoka gazeti la Taifa Leo)

- (a) Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za kwanza kwa maneno 80. (alama 8, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

- (b) Fupisha aya **mbili** za mwisho kwa maneno 70. (alama 7, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

3. SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

(Alama 40)

- (a) Andika sifa **mbili** za sauti zifuatazo. (ala. 2)

i) /e/
 ii) /ch/

- (b) Unda maneno yenyе muundo ufuatao wa sauti. (ala. 2)

i) KIKIKI
 ii) IKKI

- (c) Onyesha shadda inapowekwa katika maneno yafuatayo: (ala. 1)

i) Mwanafunzi
 ii) Alhamisi

- (d) Tunga sentensi **moja moja** kuonyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo: (ala. 2)

i) Vifungo
 ii) Kibainishi

- (e) Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? (ala. 2)

i) Changu
 ii) Manowari

- (f) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa.

(ala. 2)

Ndege hao wana manyoya mengi

	Kiswahili
(g) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo: <i>Mliyempika</i>	(ala. 3)
(h) Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari. <i>Msichana yule alizungumza kitausi.</i>	(ala. 1)
(i) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. <i>Ingawa alitia bidii masomoni, alifeli mtihani.</i>	(ala. 2)
(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali/vijisanduku. <i>Mvua kubwa inayonyesha itasababisha mafuriko.</i>	(ala. 3)
(k) Andika upya sentensi ifuatayo ukianzia na yambwa tendewa. <i>Kirwa dimjengea mama huyo nyumba kwa matofali.</i>	(ala. 2)
(l) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali ya kuendelea. <i>Walimu wanafunza.</i>	(ala. 2)
(m) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi. <i>Muliwa alimwambia Farida kuwa angewatembelea wazazi wao siku hiyo jioni.</i>	(ala. 2)
(n) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno ‘hema’	(ala. 2)
(o) Amrishaa katika nafsi ya <u>tatu wingi</u> . <i>Lala</i>	(ala. 1)
(p) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia vinyume vyta maneno yaliyopigiwa mstari. <i>Mama alijitwika kikapu mgongoni baada ya kuinjika chungu mekonii.</i>	(ala. 2)
(q) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari. <i>Mhadhara huo tata ultolewa jana jioni.</i>	(ala. 2)
(r) Tunga sentensi moja itakayodhihirisha matumizi matatu ya ‘na’	(ala. 3)
(s) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa mabanoni.	(ala. 2)
i) Paka (<i>tendata</i>)	
ii) Choma (<i>tendua</i>)	
(t) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya tafsida.	(ala. 2)
i) <i>Mama huyo alizaa mtoto msichana.</i>	
ii) <i>Mtoto ameenda kukojoa.</i>	
4. SEHEMU D: ISIMUJAMII (Alama 10)	
<i>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.</i>	
Kibiko: Hujambo dada Cheupe?	
Cheupe: (<i>Akikoho</i>) Sijambo ndugu Kibiko	
Kibiko: Unaendelea namna gani?	
Cheupe: <i>Niko poa</i> isipokuwa maumivu kidogo ya <i>chest</i> .	
Kibiko: Usijali nitakupa <i>pain relievers</i> utakuwa sawa.	
Cheupe: Asante sana, nashukuru.	
<u>Maswali</u>	
a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya.	(ala. 2)
b) Taja na ueleze sifa za lugha inayotumika katika mazungumzo haya.	(ala. 8)

TATHMINI YA PAMOJA –KAUNTI NDOGO YA KIRINYAGA MASHARIKI**KISWAHILI – KARATASI YA 3 – 102/3****FASIH****JULAI 2019 – MUDA: SAA: 2½****SEHEMU A: RIWAYA****Assumpta K. Matei: Chozi la Heri****1. Lazima**

Riwaya ya Chozi la Heri inayasawiri matatizo ya wanajamii. Jadili.

(al. 20)

SEHEMU B: TAMTHILIA**P. Kea: Kigogo***Jibu swalii la 2 au la 3***2. "Huku ni Sagamoyo, naomba kukumbusha kuwa serikali na katiba ni mambo mawili tofauti kabisa."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(al. 4)

b) Eleza sifa **tatu** za mzungumzaji.

(al. 3)

c) Fafanua umuhimu wa mzungumziwa.

(al. 3)

d) Onyesha ukweli wa kauli katika dondoo hili.

(al. 10)

3. a) Onyesha namna maudhui ya elimu yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya Kigogo.

(al. 10)

b) Eleza mbinu ambazo jamii ya Sagamoyo ilitumia kupambana na
uongozi mbaya wa Majoka.

(al. 10)

SEHEMU C: HADITHI FUPI**A. Chokocho na D. Kayanda:** *Tumbo lisiloshiba na Hadithi nyingine**Jibu swalii la 4 au la 5.***Alifa Chokocho:** "Masharti ya Kisasa"**4. "Kweli mwalimu mkuu ana kazi nyingi na nyingine lazima aende usiku/usiku**

kuzipunguza. Lakini leo ni leo"

(al. 4)

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(al. 4)

b) Taja na utolee mfano mbinu zozote **mbili** za lugha katika dondoo hili.

(al. 4)

c) Eleza matukio yoyote **sita** yaliyotokea baada ya kauli hii.

(al. 12)

5. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo eleza namna unyanyasaji umeshughulikiwa.

a) Tumbo lisiloshiba

(al. 4)

b) Shibe inatumaliza

(al. 4)

c) Mame Bakari

(al. 4)

d) Kidege

(al. 4)

e) Tulipokutana tena

(al. 4)

SEHEMU D: USHAIRI*Jibu swalii la 6 ay la 7.***6. Angawa mdogo, dagaa, amekomaa**

Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa

Kalia kinaya, dagaa, ~~h~~ondoaa njaa

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa

Na sio mzigo, kijana, bado wafaa

Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa

Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa

Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, hajambaa

Kuliko vigogo, dagaa, hajambaa

Hapati kipigo, dagaa, hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa

Sihofu magego, kijana, nawe wafaa

Kazana kidogo, kijana, kugaaga

Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al. 2)
 b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili. (al. 4)
 c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (al. 3)
 d) Tambua bahari katika shairi hili kwa kutegemea: (al. 3)
 i) Vipande vya mishororo
 ii) Mpangilio wa vina
 iii) Idadi ya mishororo
 e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (al. 4)
 f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi. (al. 2)
 g) Eleza toni ya shairi hili. (al. 2)

7.

Eti

Mimi niondoke hapa
 Niondoke hapa kwangu
 Nimesaki, licha ya risasi
 Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
 Siondoki
 Siondoki siondoki
 Niondoke hapa kwangu!
 Kwa mateke hata na mikuki
 Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
 Siondoki
 Mimi ni pahame!
 Niondoke hapa kwangu!
 Fujo na ghasia zikizuka
 Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
 Siondoki
 Kwangu siondoki
 Niondoke hapa kwangu!
 Nawaje; waje wanaokuja
 Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
 Siondoki
 Ng'oo hapa kwangu!
 Katizame chini mti ule!
 Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
 Nende wapi?
 Si hapa kitovu changu
 Niondoke hapa kwangu
 Wangawa na vijikaratasi
 Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu

**GATUNDU SOUTH
KISWAHILI KARATASI YA 102/1
INSHA**

1. LAZIMA

- Ukiwa mhariri wa gazeti la Tazama Mbele andika tahariri itakayochapishwa katika gazeti hilo ukipinga suala la mikopo inayochukuliwa na serikali kutoka kwa mataifa ya kigeni na mashirika mengine ya kifedha.
2. Michezo ya kamari ipigwe marufuku. Jadili.
 3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo;
Bendera hufuata upopo.
 4. Tunga kisa kinachoanza kwa kauli ifuatayo;
Baba hata mimi nimeliwazia jambo hili kwa muda. Hata hivyo, moyo wangu umekuwa yabis. Hisia zangu zimekufa ganzi

**GATUNDU SOUTH
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI 2019
KIDATO CHA NNE**

1. UFAHAMU

Vitabu vingi vya hadithi za watoto vilivyowahi kuandikwa katika lugha ya Kiswahili kufikia sasa vinaweza tu kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa darasa la nne hadi la nane na hivyo basi, kuacha ombwe pale panapostahili kuwekwa msingi imara – shule ya chekechea hadi darasa la tatu. Utafiti uliowahi kufanywa na wanaismusaikolojia unathibitisha kwamba, uwezo wa mwanafunzi wa kujifunza lugha ya pili huwa katika kiwango cha juu awapo na umri mdogo na kwamba, uwezo huo huanza kupungua kadiri umri unavyoongezeka na kufikia kipindi maalum (critical period) ambacho hukisiwa kubisha katika umri wa kubaleghe au kuvunja ungo.

Hivyo basi, ili kustawisha hulka ya usomaji ya kudumu, waandishi wa fasihi ya watoto wanapaswa kujifahamisha mengi kuhusu ukuaji wa watoto hao wadogo na mikakati ambayo huitumia katika kujifunza lugha ya pili.

Aidha, wanapaswa kuyafahamu yale yanaypwapendeza na kuwachocha katika kusoma ili kuyajumuisha katika vitabu vyao vya hadithi. Mambo haya yatatimia iwapo waandishi hao watakuwa na mafunzo ya kimsingi katika taaluma ya isimusaikolojia.

Wanafunzi katika viwango tofauti wana mikakati tofauti ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Kufikiria kwamba wanafunzi wa madarasa ya chini (darasa la kwanza, pili na tatu), wanaweza kuitumia mikakati sawa na ile ambayo hutumiwa na wenzao wa madarasa ya juu kujifunza Kiswahili si sahihi.

Watoto wadogo hujufunza mambo mengi kwa kukariri, kuigiza, kuiga, kufuutilia hadithi kwa picha mionganii mwa mbinu nyingine. Ili kufanikiwa katika kuwaandikia, sharti mikakati hiyo ya ujifunzaji izingatiwe.

Ufundu mkubwa unahitajika sit u katika kuziunda sentensi zao, bali pia katika kuifinyanga sarufi. Sentensi zenyewe ziwe fupi, zenyeye sarufi na msamati sahihi, zilizorudiwarudiwa ili kuzifanya zinate akilini na kuendelezwa kwa mtindo wa nyombo au mashairi mepesi.

Watoto wadogo huvitiwa sana na nyimbo na mashairi mepesi na hujifunza kwa urahisi kupitia kwayo. Msururu wa vitabu vya 'Someni kwa Furaha' uliotimiwa katika miaka ya themanini na mwanzomwanzo wa miaka ya tisini, ni mfano wa vitabu vilivyotekeleza dhima muhimu sana katika kuumua na kuchochea hamu ya wanafunzi kupenda kukisoma Kiswahili.

Vitabu vilitumia mbinu mbalimbali zilizoweza kuyateka mawazo ya wanafuzi katika viwango tofauti. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya vibonzo, mashairi na nyimbo za chekechea zenyne maudhui ambayo watoto wangeweza kujinasibisha nayo. Baadhi ya nyimbo hizo zilihimiza umuhimu wa kusomea katika mazingira safi, ushirikiano katika shughuli mbalimbali naumuhi muhi wa kuyachangamkia masomo. Mfano mzuri ni huu wimbo unapatikana katika kimojawapo cha vitabu katika msururu huo: chawa chawa mchafu, petu ni pakavu. Kata nyika utosini, kata nywele kwa mashine. Kichwa safi kama nini? Chawa chawa mchafu petu ni pakavu.

Mbinu nyingine iliyotumiwa sana katika vitabu hivyo ni matumizi ya picha na vibonzo. Vitabu vya watoto vinapaswa kuwa na picha nyingi au vibonzo vingi kuliko maandshi. Picha na vibonzo vyenyeviwe na rangi kwa sababu watoto huvutiwa sana na rangi.

Waandishi wa fasihi ya watoto katika Kiingereza wamefanikiwa pakubwa katika kukumbatia mbinu hii, na hivyo, basi, kuyakidhi mahitaji ya rika tulilotaja kwa kuandika vitabu ambavyo vimechangia kwa akali kubwa katika kustawisha hulka ya usomaji bado ingali changamoto kubwa kwani huanza kuwekewa msingi katika darasa le nne.

Kiini hasa cha kuendelea kuwepo kwa mielekeo hasi na matokeo mabaya katika somo la Kiswahili ni kule kukosekana kwa vitabu faafu vya hadithi za watoto madarasa ya chini vinavyoweza kusaidia katika kujenga hulka ya usomaji mapema iwezekanavyo.

Ombwe hilo linaweza kufidiwa tu iwapo waandishi wataibuka na vitabu ambavyo *Over 7000 Subscribers* vitayakidhi mahitaji ya watoto hao wadogo na kuwapa ari ya kikipenda Kiswahili kuanzia umri wa chini.

1. Kipe kifungu anwani mwafaka. (alama 1)
2. Ni katika umri gani mwanafunzi hujifunza lugha ya pili kwa urahisi. (alama 1)
3. Waandishi wa vitabu vya watoto watastawisha usomaji wa kudumu kwa njia gani? (alama 4)
4. Taja dhana potovu kuhusiana na ujifunzaji lugha kwa watoto. (alama 2).
5. Onyesha njia ambazo kwazo watoto hujifunza lugha kwa wepesi. (alama 3)
6. Vitabu vya watoto vinapendekezwa viwe na sifa gani? (alama 2)
7. Eleza maana ya msamiati huu kulingana na muktadha wa matumizi. (alama 2)
 - i) Ombwe
 - ii) Kufidiwa

2. Ufupisho

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Katiba mpya imeipa lugha ya Kiswahili hadhi nyingine kuifanya kuwa lugha rasmi kando na kuwa ni lugha ya taifa. Mabadiliko haya muhimu yana changamoto kadhaa.

Kwanza kabisa lugha ya Kiswahili sasa itashindania nafasi sawa na ile ya Kiingereza katika shughuli za kikazi. Swala hapa linahusu majukumu ambayo lugha hizi zitatekeleza. Je, lugha hizi zitatumiwa mtawalia katika shughuli za kikazi au zitatengewa majukumu maalum?

Lugha ya Kiswahili itachukua nafsi ipi? Kiingereza kitaachiwa nani tukizingatia kuwa kwa muda mrefu lugha ya Kiingereza ndio imekuwa lugha tawala katika mazingira haya? Je, wananchi wataweza kufanya maombi kwa lugha ya Kiswahili kando na kuendesha mawasiliano ya kiofisi kwa lugha hii? Kwa kifupi ili kusitokee mgongano wa matumizi ya lugha hizi mbili, ni muhimu sana kwa watunga-sera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili katika mazingira ya kikazi.

Changamoto nyingine na muhimu ni kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya. Kwanza, wananchi wanafaa wafahamishwe kuhusu haki yao ya kutumia lugha hii katika mazingira ya kazi. Si ajabu kuwa wao hawana habari kuhusu mabadiliko haya ya kisera. Watumishi wa umma nao wanastahili kupewa mafunzo maalumu kuhusu mbinu za mawasiliano katika Kiswahili ili waendeshe shughuli zao vizuri.

Kwa upande mwingine, vyuo vikuu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zinastahili kutoa kozi ya lazima katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiungu nazo ili kuwaandaa kwa mahitaji haya mapya ya kikatiba.

Kadhalika, serikali inastahili kuwaandaa wataalamu zaidi wa lugha ya Kiswahili ambao watahusika katika kuwafunza wanaohusika na utekelezaji sera.

Kuna haja pia ya wataalamu wa lugha kuandika vitabu zaidi kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vitatoa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za mawasiliano. Shughuli hii iambatane na ile ya kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha nyingine kwa ile ya Kiswahili.

Kwa muda mrefu sasa, kumekua na tatizo la mitazamo hasi mionganoni mwa wananchi kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wananchi wamekuwa na sababu zao za kutoitumia lugha hii wakishikilia kuwa lugha yenyewe ni ngumu.

Aidha, wananchi wengine wamekuwa na uzoefu wa kuzungumza lugha ya Kiingereza au lugha nyingine za kigeni huku, wakitoa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili, waipende na kuilewa vizuri.

Ni muhimu kufanywe kila juhudi kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia Kiswahili sanifu ili wasije wakakivuruga kwa kukiendeleza visivyo au kwa kukiharibu kwa kijilugha cha sheng au kwa lugha za kienyeji.

Vilevile, ni muhimu wananchi watambue kuwa nchi yetu ya Kenya ndiyo kitovu cha lugha hii na hivyo basi, wafanye kila juhudi kuitumia ipasavyo ili tusionekane kuwa watumwa katika lugha yetu asili. Tunahitaji viongozi vielezo nchini ambao wanazungumza Kiswahili sanifu kwa madoido na ufasaha sio tu katika ulingo, bali pia katika Nyanja nyingine za maisha.

Kwa hivyo, viongozi wetu wajiepushe na matumizi ya Kiswahili chapwa ili wananchi wahimizike kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Ingekuwa hata bora ikiwa wangepewa kipaumbele katika kupokea mafunzo kabambe katika lugha hii. Pengine tungejifunza mengi kutoka nchi jirani ya Tanzania ambayo kwa kiasi kikubwa, ilifafulu kuramisha Kiswahili na kuleta umoja wa kitaifa.

- a. Fafanua changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi. Maneno 70 alama 6, moja ya mtiririko. Matayarisho.....
Jibu.....
- b. Mwandishi ametoa mapendekezo kuhusu namna ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini. Yafafanue. (maneno 80(alama 7, 1 ya mtiririko)
Matayarisho.....
Jibu.....

3. Matumizi ya lugha

- a. Eleza sifa mbilimbili za vitamkwa vifuatavyo.
 - i) /ng'/
 - ii) /l/
 - iii) /e/
- b. Andika maneno yenye miundo ifuatayo ya silabi na upigie mstari.
 - i) KKKI -
 - ii) IK -
 - iii) KKI -
 - iv) I -
- c. Tia shadda katika maneno yafuatayo. (alama 1)
 - i) Mji
 - ii) Karatasi
- d. Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya ngeli zifuatazo. (alama 2)
 - i) I-I
 - ii) U-YA
- e. Yakinsha kwa wingi. (alama 1)
 - Mwalimu hakumwadhibu mwanafunzi.
- f. Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 1)
 - Mtoto analala
- g. Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno. (alama 2)
- h. Ainisha mofimu katika neno. (alama 3)
 - Lilililimia
- i. Changanua kwa kutumia jedwali.

	Kiswahili	
j.	Wale wakubwa waliohitajika mkutanoni wamekosa kufika.	(alama 4)
j.	Ainisha kiima na shamirisho katika sentensi ifuatayo.	(alama 3)
	Mtahiniwa huyo alimletea mamake mkufu wa dhahabu.	
k.	Andika katika usemi wa taarifa.	(alama 2)
	"Hilo jicho la paka mweupe leo ni marufuku kwangu," Alisema Bwana Ridhaa.	
l.	Tunga sentensi yenyе muundo ufuataa.	
	Nomino ya jamii, kirai kihuishi, kitenzi kishirikishi, kielezi cha mahali.	(alama 2)
m.	Tunga sentensi ukutumia kiambishi 'tu' kama.	(alama 2)
	i) Kiwakilishi	
	ii) Kitenzi	
n.	Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo.	(alama 2)
	Nzi hao walimvamia ng'ombe aliyejewa na kidonda.	
o.	Unganisha kwa kutumia kiunganishi cha kinyume.	(alama 1)
	Nitakununulia baiskeli	
	Sitakupeleka ziara.	
p.	Onyesha vishazi katika sentensi hii.	(alama 4)
	Ikiwa utajitahidi masomoni utafanikiwa maishani.	
q.	Onyesha aina za virai katika sentensi hii.	(alama 2)
	Mwalimu mwininge atatufundisha Kiswahili kando ya mti.	
r.	Andika maana mbili za sentensi ifuatayo.	(alama 2)
	Rehema aliletewa buibui na mtoto wake.	
s.	i. Wenye dhambi walimfanya Yesu afe msalabani. (Tumia kauli ya kutendesha.)	(alama 1)
	ii. Tunga sentensi ukutumia kitenzi '-pa' katika kauli ya kutendeana.	(alama 1)
t.	Akifisha sentensi ifuatayo.	(alama 1)
	Amicus curiae ni msamiati uliovuma nchini baada ya uchaguzi mkuu mwanasiasa alisema.	
u.	Uhawinde ni kwa utajiri na majimbi ni kwa	(alama 1)

4. Isimu jamii

Benki yenye haina kitu ... CD4 count yake iko chini ... ni emergency ... tutampoteza ikikosekana.

- a. Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)
- b. Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo. (alama 8)

GATUNDU SOUTH
KISWAHILI
FASIHI 102/3

Swali la lazima

(1) CHOZI LA HERI

ASSUMPTA MATEI

'Huyu ambaye mama alimwona kuwa gae, kumbe sasa ndiye chombo cha kunivusha bahari hii ya dhiki?'

- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
- (b) Eleza sifa sita za mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 6)
- (c) Onyesha jinsi wahusika mbalimbali katika riwaya ya chozi la Heri walivyopitia 'bahari ya dhiki'. (Alama 10)

SEHEMU B

(2) TAMTHILIA

Jibu swali la 2 au 3

Kigogo – Pauline Kaya.

'Nimekuja kuwakomboa sio kuwaumbua'.

- (I) Eleza umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 8)
 - (II) Kwa kutumia hoja kumi na mbili, thibitisha kuwa mneneawa na wenzake walistahili kukombolewa. (Alama 12)
- (3) 'Acha porojo zako' Kigogo hachezewi; watafuta maangamizi!
- (I) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

- (II) Fafanua sifa sita za kigogo anayerejelea.
 (III) Eleza mbinu kumi zilizotumiwa na kigogo kuonyesha ‘hachezewi’

(Alama 6)
 (Alama 10)

SEHEMU C**HADITHI FUPI – Alifa chokocho na Dumu kayanda.****(Mtihani wa maisha)**

- ‘Leo mwalimu mkuu atajua kwamba mdharao biu hubiuka’
 (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
 (b) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika mktadha huu. (Alama 6)
 (c) Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 2)
 (d) Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii. (Alama 8)

Ndoto ya mashaka (Ali Abdulla)

- (5) Kusema kweli lakini hata mimi sikuwa na nadhari katika kumpenda msichana huyu ... Nilimpenda kufa! Lakini!
 Kwao bure tu!
 (a) Eleza mukutadha huu. (Alama 4)
 (b) Taja mtindo wa lugha uliotumika katika mukutadha huu. Alama 4
 (c) Taja sifa mbili za mzungumzaji. (Alama 2)
 (d) Onyesha maudhui ya umaskini katika hadithi fupi ya Ndoto ya mashaka.

SEHEMU YA D**USHAIRI****Jibu swali 6 au 7****(6) USHAIRI****Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alfajiri na mapema
 Hunipitia na jembe na kotama
 Katika njia iendayo kondeni
 Kama walivyofanya babuze zamani;
 Ni muonapo huwa anatabasamu
 Kama mtu aliye na kubwa hamu
 Kushika mpini na kutokwa jasho
 Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
 Videge vyta anga vinavyotumbuzza
 Utadhani huwa vimemngojea
 Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
 Pia pepo baridi kumpepea
 Rihi ya maua zikimletea
 Nao umande kumbusu miguu;
 Ni miti yote hujipinda migongo
 Kumpapasa, kumtoa matongo;
 Na yeche kuendelea kwa furaha
 Kuliko ye yote ninayemjua

Akichekelea ha ha ha ha ha ha ...
 Na mimi kubaki kujiuliza
 Kuna siri gani inayomliwaza?
 Au ni kujua au kutojua?
 Furaha ya mtu ni furaha gani
 Katika dunia inayomhini?
 Ukali wa jua wamnyima zao
 Soko la dunia lamkaba koo;
 Dini za kudhani zamsonga roho
 Ayalimia matumbo ya waroho;

Kuna jambo gani linamridhisha?
 Kama si kujua ni kutokujua
 Laiti angalijua, laiti angalijua!

- | | |
|--|------------|
| (a) Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. | (Alama 4) |
| (b) Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. | (Alama 8) |
| (c) Taja nafsineni katika shairi hili. | (Alama 1) |
| (d) Eleza toni ya shairi hili. | (Alama 1) |
| (e) Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano. | (Alama 2) |
| (f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. | (Alama 4) |

(7) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
 Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
 Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
 Ilia ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
 Msikose simile, magalachia, si gurudumu mwili.

Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
 Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
 Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
 Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
 Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
 Ilia kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
 Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

- | | |
|--|------------|
| (a) Liweke shairi hili katika bahari tatu. | (Alama 3) |
| (b) Eleza dhamira ya mshairi. | (Alama 2) |
| (c) Eleza muundo wa shairi hili. | (Alama 4) |
| (d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. | (Alama 4) |
| (e) Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. | (Alama 3) |
| (f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. | (Alama 4) |

SEHEMU D
FASIHI SIMULIZI

- | | |
|---------------------------------|-----------|
| A (i) Miviga ni nini? | (Alama 2) |
| (ii) Eleza sifa nane za miviga. | (Alama 8) |
| B (i) Ulumbi ni nini? | (Alama 2) |
| (ii) Eleza sifa nane za ulumbi | (Alama 8) |

**UASIN GISHU
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA**

LAZIMA.

1. Wewe ni katibu wa kamati ya maandalizi ya sherehe ya kuwatuza wanafunzi waliomaliza kidato cha nne. Andika ratiba kwa ajili ya shershe hiyo katika ugatuzi.
 2. Wanasiasa ndio chanzo cha migogoro katika mataifa mengi ulimwenguni . Jadili kauli hii.
 3. Andika insha itakayothibitisha methali ifuatayo””Pema usijapo pema, ukipemasi pema tena
 4. Jairo, alikuwa amelala chali barabarani wakati wa jua la utosini. Alikuwa hajitambui. Matapishi.....(endeleza)

**UASIN GISHU
102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI 2**

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Ustawi wa dola lolote lile hutegemea mseto wa nguvu, maarifa chipukizi, uchapuchapu wa barubaru, pamoja na maarifa, upevu, uvumilivu na tajriba ya wazee. Tunaweza kuumithilisha ufanisi wa nchi na jumba la ghorofa lililojengwa juu ya tegemezo: msingi huu ukiwa imara, ghorofa nyingi zaweza kuinuliwa. NayO imara ya tegemezo hutegemea vyuma imara visiviyotetereka na vifaa vinginevyo. Zaidi ya haya yote, mafundi wahusika kama vile wasanifu mjengo, wahandisi, mafundi bomba na wengineo sharti wawe na ujuzi tosha ili kufanikisha kazi inayohusika. Katika taswira hii, twaweza kuelewa ni kwa nini baadhi ya nchi zimestawi huku nyingine zikiitwa ulimwengu wa tatu. Shida za nchi hizo ni kutozistawisha taaluma ambazo ndizo msingi wa maendeleo, hivyo huwa na walakini katika utekelezaji. Matokeo yake ni kulimatiA.

Nchi nyingi humu barani mwetu zimekosa kustawi kutokana na kasoro nyingi tulizo nazo katika uimarishaji wa taaluma zetu. Sababu kuu ni kuwa, wengi wetu hukimbilia kutekeleza kazi mbalimbali hata bila ujuzi wowote kwa kazi hizo. Tabia kama hii inatokana na ukweli kuwa sisi hatujali kama tuna vipawa vyaya kufanya kazi fulani. Wengine huvunjwa moyo na walio wazingira kuwa vipawa vyao havifai. Hivyo, si ajabu kuona kijana aliye na kipawa fulani akikosa kukivuvia kwa sababu labda hata hatambui kuwa anacho.

Wengi wa wakembe wetu hukosa kuvitambua vipawa vyao, hivyo kukosa kuendeleza utaalamu unaohusiana navyo kwa kukosekana kwa **mtalaa** wa kuvichochea katika mfumo wa elimu. Mfumo wa elimu nchini Kenya kwa sasa unasisitiza wanafunzi kupita mtihani ili kuingia vyuoni. Hata hivyo, ni muhimu kuvikuza vipawa walivyo navyo vijana ili wavitumie katika siku za halafu. Vitambuliwe mapema shulenii bali si vyuoni. Kunao wanagenzi wengine ambaao, licha ya kuvitambua vipawa vyao hawavifukutii kamwe, huvipuuza na kujisukuma katika taaluma ambazo hazikuwafaa kamwe. Kunao wanagenzi wengine ambaao hutamani na kuingilia taaluma fulani, si kwa kuzipenda, bali kwa kuwa wandani wao wazishiriki. Hawajui kuwa kibaya chako si kizuri cha mwenzio. **Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa.** Kuna wengine ambaao huziandama taaluma fulani kwa kushurutishwa na wazazi au wadhamini wao. Nao vijana hukosa ukakamavu wa kujiamulia na kukubali shingo upande maamuzi hayo. Hata hivyo, kuna wale ambaao hujitosa katika taaluma hizo bila kushurutishwa ili wapate hadhi. Matokeo ni kuwa kijana huzifanya kazi hizo kwa chati wala si kwa dhati. Wengine hujipenyeza kwa taaluma fulani eti kwa kuwa wamekosa nytingine. Si ajabu basi kutokana na ukosefu wa ajira kumwona mtaalamu wa mifugo akiwa mwalimu, mwalimu akiwa dereva na tabibu akiwa mkulima hali zaraa haimudu.

Ili kupata suluhu katika jambo hili, sharti kila mmoja wetu ashiriki katika kuitambua, kuikuza, kuikomaza na kutumia taaluma ya kila kijana. Twaweza kuuiga mfano wa Wazungu wafanyakayo kwao. Wao hujitahidi kuvitambua vipawa vyta watoto wangali wachanga hali ambayo huwasaidia kuzikuza taaluma zao baadaye. Naye kijana akishajua atakachofanya, afaa kufanya utafiti ili kufikia kina cha taaluma yake.

Maswali

- | | |
|---|-----------|
| (a) Eleza sababu za watu kujishughulisha na taaluma zisizo zao. | (alama 2) |
| (b) Eleza kikwazo cha ustawi wa nchi zinazoendelea. | (alama 1) |
| (c) Taja mambo manne yanayostawisha taifa. | (alama 4) |
| (d) Taja mambo matano yanayokwamiza uendelezaji wa vipawa mionganoni mwa vijana. | (alama 5) |
| (e) Kuna tofauti gani kati ya Waafrika na Wazungu katika ukuzaji wa taaluma? | (alama 2) |
| (f) Eleza maana ya ‘Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa’. | (alama 1) |
| (g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo vilivyotumika katika ufahamu. | (alama 2) |
| (i) kulimati | |
| (ii) mtalaa | |

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma makala haya kisha ujibu maswali yafuatayo.

HAKI ZA BINADAMU

Binadamu wana mazoea ya kufikiria kuwa jinsi wafanyavyo, waongeavyo na wafikiriavyo kuhusu vitu ndivyo inavyopasa kuwa. Kama binadamu tunaamini njia yetu ndiyo sahihi, yenye mantiki na inayopasa kufuatwa na kila mtu. Msingi huu huu unakwenda kinyume na kutambua kila binadamu ana haki ya kufikiri, kusema au kuongea na kutenda mradi asikiuke haki ya mwenzake iliyo sawa na yake. Nguzo mojawapo *inayogongomelea hoja* hii ni Haki za Binadamu.

Azimio la kutangaza Haki Bia za Binadamu liliafikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Desemba, 1948. Baraza kuu hilo liliyasisitizia mataifa wanachama umuhimu wa kuyasambaza, kuenezea, na kusisitiza kusambazwa kwa azimio hilo katika shule na taasisi za kielimu. Msingi wa uhuru, haki na amani ulimwenguni ni kutambua binadamu wote wana haki sawa. Ingawa kimsingi jamii na mataifa yote ya ulimwengu yanapaswa kuthamini, kusambaza na kuhimiza umuhimu wa Haki za Binadamu zipo jamii ambazo hukiuka haki hizo. Matokeo ya ukiukaji huu yana athari hasi sana kama iliyotokea nchini Rwanda na Bosnia Herzegovina kulikotokea mauaji ya halaiki.

Azimio la Haki za Binadamu linajumuisha vipengele kadha ambavyo ni mihimili mikuu ya Azimio lenyewe. Kipengele msingi kabisa kinasisitiza kuwa kila kiumbe anazaliwa huru na ana haki na hadhi sawa na kiumbe mwingine. Ukweli wa kauli hii ulikokotezw na kauli ya mwanafalsafa maarufu Jean Jacques Rousseau aliyesema kuwa kila kiumbe huzaliwa huru lakini huwa katika pingu ulimwengu mzima. Kauli hii ilitambua ukiukaji huu wa kipengele hiki. Kipengele cha pili kinasisitiza kuwa binadamu wote wana haki za kufurahia uhuru wao pasi na kutengwa au kubeuzwa kwa misingi yoyote ile si rangi, kabilia, jinsia, lugha, dini, asilia, utajiri au chochote kile.

Vipengele vingine vinatukumbusha kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kupata ulinzi. Hamna mtu anayepaswa kuishi maisha ya utumwa au unyonge wa kutumikishwa kwa namna yoyote ile. Suala hili linasisitizwa na kipengele cha sita kinachokataza kudhalilishwa kwa watu au kutunzwa kwa namna yoyote ambayo inamfedhehesha kama kiumbe. Azimio la Haki za Binadamu linasisitiza kuwa binadamu yoyote yule ana haki ya kupata ulinzi wa kisheria. Binadamu huyo hapasi kubaguliwa na ana haki ya kupata fidia ya kisheria taraa haki zake za kimsingi zikikiukwa.

Hata hivyo sio watu wote ulimwenguni ambao wanazifurahia haki hizi za kimsingi. Zipo *lukuki za jamii* ulimwenguni ambako haki za kimsingi zinakiukwa. Katika nchi ambazo zinaongozwa na watawala wa kiimla, si ajabu kuona haki za binadamu zikikiukwa. Viongozi wa aina hiyo huwa wamegeuzwa ng'ombe wa shemere na tamaa, ubinafsi na ukatili usiojua thamani ya utu. Viongozi wa aina hii wanashahau kuwa kila binadamu ana haki ya kuishi maisha huru, asipotumikishwa wala kulanguliwa kama bidhaa.

Nchi za kiimla aghalabu huongozwa na itikadi kuwa kiongozi ndiye pekee ambaye ana uwezo wa kufikiri, kuamua na kutenda. Watu wengine wanapaswa kumfuata kisilka kama yule mbwa wa Pavlov ambaye alitokwa na mate kila kengele ilipopigwa. Viongozi wa aina hii hawachelei *kuwatenza nguvu* raia zao; kuwadhalilisha kwa namna nydingi. Viongozi wa aina hiyo huiona sheria ya nchi kama iliyowekwa kwa watu wengine bali sio wao. Msimamo huu unakwenda kinyume na kipengele cha saba cha Haki Bia za Binadamu kisemacho kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria.

Baadhi ya haki zinazokiukwa katika jamii za kimabavu ni haki ya watu kuungana, kuwaza, kushiriki katika maamuzi ya serikali, kuwa mwanachama wa jumuia waitakayo, kumiliki mali, kutembea, kuishi anakotaka, kutohukumiwa bila ya kuwako na utaratibu wa kisheria. Ni muhimu hata hivyo kujua ni muhimu kwa raia wenyewe kuijelimisha na kuzijua haki zao. Serikali inapaswa kuwa mlinzi wa sheria zenyewe. Lakini muhimu kujua pia kuwa mlinzi naye hulindwa pia.

- a) Kwa maneno kati ya 90 – 100 fafanua Haki Bia za Binadamu zilizoafikiwa na Baraza kuu la umoja wa Mataifa. (Alama 10)
- b) Kwa nini viongozi wa kiimla hukiuka haki za binadmu. (Maneno 50 -60). (Alama 5)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) Ainisha vokali zifuatazo ukizingatia mwinuko wa ulimi. (alama 1)
 - i) /o/
 - ii) /a/
- b) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi. /l/ na /r/ (alama 1)
- c) Ainisha mfumo wa sauti katika neno lifuatalo. Machweo (alama 2)
- d) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ki- ya masharti. i. Tumekosa chamcha tukala chajio. (alama 2)
- e) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. Utundu wa Mali na Shakila ulikashifiwa vikali sana. (alama 2)
- f) Yakinisha sentensi ifuatayo. Rais hakuwafuta wala kuwakaripia waliosanzua msitu wa Mat. (alama 1)
- g) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali isiyodhahirika. (alama 1)
- h) Andika kinyume cha: Kile hakikuuzwa na mnadi. (Alama 1)
- i) Tumia kauli ya kutendeka katika sentensi zifuatazo:
 - i) Wanamuziki watapata sifa kwa kuimba nyimbo za kutukuza maadili. (Alama 2)
 - ii) Eleza matumizi yoyote **matatu** ya kiambarishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi. (Alama 3)
- j) Andika katika msemo wa taarifa. Askari: Ulikuwa unaelekewa wapi uliposhambuliwa? Jirani: Nilikuwa nikienda sokoni jana. (alama 2)
- k) Tunga sentensi yenyе muundo ufuatao: RN, RT,RH (alama 2)
- l) Andika mzizi wa neno ~~liliopigwa~~ msitari katika sentensi ifuatayo. Kamba zilizotumiwa zilikuwa **ndefu**. (Alama 1)
- m) Changanua kwa njia ya mishale. Mbayuwayu na korongo ni ndege ambaeo huishi mwituni. (alama 2)
- n) Akifisha : rosa mistika ni riwaya ilioandikwa na euphrase kezilahabi mmesikia mwalimu ndolo akawaambia wanafunzi. (alama 2)
- o) Andika sentensi ifuatayo upya ukianza kwa kipozi. Mwalimu alimwandikia mwanafunzi maagizo kwa kalamu. (alama 2)
- p) Eleza miundo mitatu ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi. (alama 3)
- q) Eleza ukitoa jozi **mojamoa** ya mfano, **miundo miwili** ya nomino zilizo katika ngeli ya KI – VI. (Alama 3)
- r) Weka katika udogo. Ndizi mbivu zimebekwa ndani ya kikapu kikuukuu. (Alama 1)
- s) Jaza pengo ukitumia maneno yaliyo katika paradesi katika hali inayofaa.
 - i. Mwanafunzi mwenye _____ (buni) huwafanya _____ (elimu) wake kufurahi. (Alama 2)

- ii. Andola aliachiliwa kwa sababu ya _____ (kosa) wa _____ (shuhudia) wa _____
kutosha. (Alama 2)

4. ISIMUJAMII. (Alama 10)

- a) Eleza sababu za kufanya makosa katika mazungumzo (alama 4)
- b) Eleza mambo manne yaliyochochea kusanifisha lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 4)
- c) Taja lahaja zozote nne za lugha ya Kiswahili (alama 2)

UASIN GISHU

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

JULAI

1. LAZIMA: (HADITHI FUPI: (*TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE*)
Maisha ya wahusika katika hadithi ya Ndoto ya Mashaka yamegubikwa na mashaka mengi. Thibitisha. (alama 20)

2. TAMTHILIA: KIGOGO (PAULINE KEA)

“Do! Do! Simameni! Simameni leo kutanyesha mawe!”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondo hili. (alama 4)
- c) Dhihirisha kwa kuzingatia hoja sita jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia ya Kigogo.(alama 12)

au

3. Kwa kutolea mifano, eleza jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu ya majazi. (alama 20)

4. RIWAYA: CHOZI LA HERI (ASSUMPTA MATEI)

“Lakini Mungu sio Athumanji, huenda sadfa ikatukutanisha.”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Taja tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza. (alama 2)
- c) Eleza umuhimu wa mrejelewa wa dondo hili. (alama 14)

au

5. Elimu ndio ufunguo wa maisha. Thibitisha dai hili kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)

6. **USHAIRI**

Ni sumu, sumu hatari

Unahatarisha watoto

Kwa ndoto zako zako leweshi

Za kupanda ngazi

Ndoto moto moto ambazo

Zimejenga ukuta

Baina ya watoto

Na maneno laini

Ya ulimi wa wazazi.

Ni sumu, sumu hasiri

Unahasiri watoto

Kwa pupa yako hangaishi

Ya kuwa tajiri mtajika

Pupa pumbazi ambayo

Imezaa jangwa bahili

Badala ya chemic hemi
 Ya mazungumzo na maadili
 Bainya watoto na wazazi.

3.../

Ni sumu, sumu legezi
 Unalegeza watoto
 Kwa mazoea yako tenganishi
 Ya daima kunywa ‘moja baridi’
 Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu
 Hadi saa nane usiku
 Huku yakijenga kutofahamiana
 Bainya watoto na mzazi.

Ni sumu, sumu jeuri
 Unajeruhi watoto kwa pesa
 Kwa mapenzi yako hatari
 Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
 Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
 Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
 Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi.

Maswali

1. Andika mifano miwili ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
2. Fafanua maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
3. Fafanua umuhimu wa urudiaji katika shairi hili. (alama 4)
4. Bainisha nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi hili. (alama 2)
5. Yanayozungumziwa yanajenga ukuta kwa njia gani? (alama 4)
6. Andika ubetio wa tatu katika lugha nathari. (alama 4)

au

7. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali

Mungu naomba subira, subira nayo imani,
 Imani iliyo bora, bora hapa duniani,
 Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani,
 Hiani pamwe ukora wenye kuhni.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu,
 Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili,
 Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili,
 Thakiri kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele,
 Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele,
 Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele,
 Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato,
 Vikwatopia maole, maole kufanya mito,
 Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
 Kitoto kilo vipete, vipete vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka,
 Kutamka wazi vino, vino subira kutaka,
 Kutaka imani mno, mno nisipate wahaka,

KANDARA**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI****KIDATO CHA NNE****102/1****KISWAHILI****KARATASI YA 1****INSHA****1. LAZIMA**

- Andika wasifu wa babu yako aliyejewa mwalimu mkuu katika shule ya upili ya Tuzo .
2. Wewe ni mbunge wa eneo la Lalama. Pendekeza katika bunge la kitaifa hatua zinazoweza kuchukuliwa na serikali kuu kumwendeleza kielimu mtoto mvulana.
 3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani.
 4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
Nilipomwangalia baba yangu kisha mama yangu, nilijua kuwa jambo fulani lingetendeka.....

KANDARA**102/2****KISWAHILI****(UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMUJAMII)****MUHULA WA PILI****MUHULA WA PILI 2019****UFAHAMU****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali .**

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenyeye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inanza kupusa . Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya yaliyotosha kuitwa magenge, alishukuru kwa hali hii . Vipi angeweza kulidhibiti gari lake hili kwenye barabara iliyosakafisha nayo ikahitimu . Magurudumu haya yaliyong'ara kama upara wa shaibu aliyejukula chumvi hadi iikamwoga yangeyii uelekezi wake . Mara ngapi gari hili limetaka kumwasi barabarani . Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini . Hakujitakilifu kutaka kuyapa mji maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali - nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake .

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani . Siku mbili ziliikuwa zimepita akiwa pale kazini . Madaktari kama yeye hawakuwa wengi . Alikuwa mionganini mwa madktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa . Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha . Mshahara wao wa mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao . Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi . Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye masikio yaliyotiwa zege . Na kweli wanavyosema , mwenye macho haambiwi tazama . Basi walitazama hapa na pale wakaona penye mianya ya matumaini , nao wakaiandama .

Hadi leo hii hamna la mno liliolofanyika . Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri . Hafanyi kwa kuwa katosheka , maana pia yeye ana dukuduku . Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya ya kumsoza , maana umri nao unazidi kumla . Japo anatia na kutoa , mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu .

Daktari Tabibu waama ni mfungwa . Ametekwa na kuzuiwa katika kupenda na kuchukia mambo .

Ni kama mti uliodumaa . Anatamani barabara nzuri za lami . Anatamani mshahara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake na kutimiza majukumu yake ya kimsingi . Jana amesema na rafiki yake aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye . Ingawaje mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumdokolea hali ya maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa , yapo vilevile yaliyomtia unyonge moyoni . Upweke ndio uliomtia fukuto kuu . Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano , watu hawana muda wa kutembeleana na kujuliana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo . Eti ni kila mtu na hamsini zake . Halafu ipo changamoto ya hali ya hewa . Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafunu mtu . Ni hali tofauti na ile aliyoizoea .

Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake . Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizimo ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyumbani . Kisha punde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengine kama ye ye waliofadhilli masomo yake kupitia kwa serikali na njia ya kodi . Je , si usaliti huu . Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia iliali imemjenga hadi kuwa daktari . Na je , wafanyakazi wake wa nyumbani watakwendwa wapi . Atawaambia kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake .

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua . Alipoitazama aliionna imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji . Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini . Mwili wake ulimsaliti ingawa moyo wake ulimkumbusha kuwa lisilo budi hutendwa . Hapo ndipo alipoinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili .

“Haloo ! ‘ Sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita .

“ Haloo ! “

“Naam ! Dharura nyingine tena daktari . Unaombwa kuokoa maisha mengine tena ! “

“ Haya . Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji ,’ na pale pale akaikata ile simu .

Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga . Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji . Ulikuwa umekauka kabisa . Daktari Tabibu aliduwaa pale . Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu .

MASWALI

- (a) Eleza sababu nne zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za nje . (alama 4)
 - [b] ‘Hakuna masika yasiyokuwa na mbu . ‘ Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hali ya waliohamia ng'ambo . [alama 3]
 - [c] Fafanua athari tatu zinazoikumba nchi ya msimulizi kutokana na uhamiaji wa wataalamu . [alama 3]
 - [d] Eleza mchango wa teknologia kwa kurejelea kifungu . [alama 3]
 - [e] Eleza maana ya msamati ufuatao kulingana na taarifa . [alama 2]
- [I] kuyapa mji -----
 [ii] fukuto -----

2. UFUPISHO(ALAMA 15)

Soma makala haya kisha ujibu maswali uliyopewa.

Maadili katika familia ni muhimu katika malezi ya Watoto. Hivi ndivyo alivyoniambia mtaalamu wa masuala ya Watoto Scola Wanjiru katika hospitali ya Kaunti ya Machakos. Anasema ugomvi baina ya wazazi husababisha watoto kutokuwa na maadili bora huku baadhi yao wakijiunga na makundi ya wahuni au hata kuzikimbia familia zao.

Bi Wanjiru asema ugomvi wa familia huonekana zaidi kwa watoto ambao hupata matatizo ya kusaikolojia na hivyo kuvuruga ndoto zao za baadaye,” asema. Anasema ugomvi huwaacha Watoto na vidonda moyoni ambavyo wakati mwengine huwafanya wawe katili na hata kuamini kwamba ugomvi ni sehemu ya Maisha katika wanadamu.

Adokeza kuwa utafiti unaonyesha kwamba mara nyingi ugomvi husababishwa na ulevi wa mzazi au wazazi kutoelewana kuhusu masuala ya kifamilia. Madhara yake kwa watoto huwa ni hofu na wasiwasi na kujihisi wapweke kila mara, “ asema Bi Wanjiru. Aidha kuathirika kisaikolojia hupelekeea Watoto kujingiza kwenye vitendo viovu kama ulevi na uvutaji bangi na hata kutamani kujiu. Mtaalamu huyo asema wazazi wanafaa kuwa waangalifu kwa watoto wao ili wasivuruge ndoto zao za baadaye kwa kukosa msingi bora na malezi mema.

Utafiti umeonyesha kwamba Watoto wengi waliokimbia hufanya hivyo ili kuepuka ugumu wa maisha wazazi wanapotengana au hali waionayo nyumbani kila mara wakati wa ugomvi wa wazazi au ndugu zao,” asema Bi Wanjiru aliye pia mtafiti wa masuala ya watoto. Watoto wanaolelewa kwenye familia au wazazi wanagombana kila wakati, hukosa kutimiziwa haki zao za msingi kama vile elimu, afya, malazi, mavazi na kusikilizwa.

Bi Wanjiru anawakumbusha wazazi kutimiza wajibu wao ili watoto hao wapate malezi bora zaidi na ili waweze kutimiza ndoto zao za baadaye. Anasema tafiti mbalimbali zimeonyesha watoto wanaotoka katika familia zenye ugomvi wa mara kwa mara, hupata magonjwa mbalimbali kama kuumwa kichwa, na kuwa na mawazo wakati wote. “ Madhara ya hali hiyo kwa watoto ni kutofanya vizuri shulen, kwa sababu huwa wanawaza juu ya ugomvi uliopo nyumbani.

Kadhalika mara nyingine mfarakano na ugomvi huwfanya watoto wasipate usingizi wa kutosha na kutatizika darasani. Watoto walioathirika pia huwa wakorofi, wakaidi na wenye hasira mara kwa mara, jambo ambalo linaathiri utulivu darasani na hivyo kushindwa kutimiza malengo yao.

Ugomvi pia hufanya watoto kuwa na chuki, kuna uwezekano mkubwa kwamba ikiwa baba anapenda kuzua ugomvi mtoto wa kike atawachukia wanaume maishani mwake. Hali kadhalika, kwa upande mwingine, kama mzazi wa kike atakuwa ndiye chanzo cha ugomvi katika familia, basi mtoto wa kiume atawachukia wanawake akifananisha tabia yake na wanawake wengine.

Ugomvi husababisha watoto kuiga tabia mbaya hasa ya kupigana ambapo anaweza kufikiria kuwa njia pekee ya kusuluhisha matatizo nyumbani ni kulewa na kuanzisha malumbano, ambayo wakati mwingine husababisha vita. Utafiti wa Save the Children uliofanya 1998 ulionyesha kwamba kati ya asilimia 45 na 70 ya watoto walioshuhudia ugomvi wa familia, waliathirika kusaikolojia.

Bi Wanjiru anasema familia ambazo ugomvi ni nadra kufanya mbele ya watoto, utafiti umeonyesha kwamba watoto hao huwa na nidhamu na huafikia malengo yao maishani. Ni wajibu wa mzazi kuchukua hatua kuepusha ugomvi mbele ya watoto.

MASWALI

- a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno (85 -90) [alama 8]
[Utiririko 1]
Nakala chafu
Jibu
- b) Eleza madhara makuu kwa watoto wanaolenlewa katika jamii ambazo zina ugomvi. [Maneno 50][alama 5]
[Mtiririko 1]
Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA

- a) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. [alama 3]
Raisi alisema kuwa angesafiri kwenda Somalia siku hiyo alasiri.
- b) Andika neno lenye muundo ufuatao. [alama 2]
Kiambishi ngeli wakati ujao, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda (kiishio)
- c) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. [alama 3]
Juma alipakuliwa chakula kwa bakuli.
- d) Tumia neno mume kama kielizi katika sentensi. [alama 2]
- e) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. [alama 2]
- f) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu. [alama 1]
- g) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu/dhamira yake. [alama 1]

- Funga majani matatu matatu kwa kila fungu.
- h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. [alama 2]
- i) la - (tendeana)
 - ii) Vaa (tendwa)
- I) Onyesha matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika sentensi ifuatayo. [alama 2]
- Juma atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao.
- j) Onyesha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. [alama 2]
- Wanafunzi wale walijibu maswali kwa utaratibu.
- k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea. [alama 2]
- Mwalimu humwadhibu mwanafunzi mwenye hatia.
- l) Tenga viambishi na mzizi katika neno ‘Siji’. [alama 2]
- m) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali. [alama 4]
- Nilimwona mamba majini nilipopiga mbizi.
- n) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika kinyume. [alama 2]
- Mwanafunzi aliketi kisha akakitega kitendawili.
- o) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi. [alama 2]
- “ Ningefika mapema ningemkuta mwalimu darasani.
- Ningalifika mapema ningalimkuta mwalimu darasani.
- p) Andika visawe vya maneno haya. [alama 2]
- i) Heshima
 - ii) Ruhusa
- q) Bainisha mofimu katika neno wafiwa. [alama 2]
- v) Andika sauti zenyе sifa zifuatazo. [alama 2]
- i) Kikwamizo ghuna cha mdomo na meno.
 - ii) Irabu ya nyuma, wastani.
- s) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo-; Jua lile ni muhimu kwetu.
- ISIMU JAMII. [alama 10]**
- a) Eleza maana ya sajili ya lugha. [alama 2]
- b) Fafanua mambo manne yanayosababisha kuibuka kwa sajili tofauti. [alama 8]

KANDARA
102/3 (Fasihi)
KISWAHILI
Karatasi ya 3

SEHEMU YA A. SWALI LA LAZIMA

TUMBO LISIOSHIBA na hadithi nyingine (wahariri: A. Chokocho na D. Kayanda)

1. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, ‘Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.’ Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

SEHEMU B. TAMTHILIA: Kigogo Puline Kea

2. “Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba....kutrejeshahatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena.”
 - a. Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
 - b. Kwa kumrejelea mzungumzaji wa maneno haya, bainisha unafiki katika kauli hii. (alama 16)
3. Eleza jinsi mbinu ya taharuki ilivytumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. (alama 20)

SEHEMU D. RIWAYA.

CHOZI LA KHERI NA Assumpta Matei

4. Jadili maudhui ya ‘migogoro’ katika riwaya ya Chozi la Kheri. (al 20)
5. “ ...alinionya dhidi ya kumwambia yejote kuhusu unyama...”
 - a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)

Kiswahili

- | | |
|---|------------|
| b) Fafanua sifa nne za anayehusishwa na maneno haya. | (al 4) |
| c) Onyesha namna ukiukaji wa haki za watoto unavyotokea katika riwaya hii. | (alama 12) |
| 6. SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI | |
| a) Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi. | (alama6) |
| b) Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. | (alama6) |
| c) Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti. | (alama 2) |
| d) Tambua dhana zinazotokana na maelezo haya. | |
| i) Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla? | (alama1) |
| ii) Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani? | (alama 1) |
| iii) Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje? | (alama 1) |
| iv) Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwa | (alama 1) |
| v) Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake? | (alama 1) |
| vi) Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili. | (alama 1) |

SEHEMU YA E. USHAIRI**7. SHAIRI A****MWANA**

1. Kwani mamangu u ng'ombe, au u punda wa dobi?
 Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
 Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
 Hebu nambie
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

MAMA

2. Nong'ona mwana nong'ona, sitafute angamiyo
 Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
 Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
 Kwani kelele kunena, huyataki maishiyo?
 Hilo nakwambia.

MWANA

3. Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo
 Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo
 Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
 Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo
 Hebu nambie
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni
 Nini yako matulubu, kulima hadi jioni?
 Na jembe ukidhurubu, ukilitua guguni
 Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
 Hebu nambie
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
 Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani
 Hajali hakuthamini, wala haoni huzuni
 Mwisho wa haya ni nini, ewe mama wa imani?
 Hebu nambie

Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
 Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika
 Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
 Ukichelewa vituko, baba anakutandika
 Hebu nambie
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
 Kiishapo u mbioni, wapita kupokapoka
 Urudi nje mekoni, uanze kushughulika
 Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka
 Hebu nambie
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo

MAMA

Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
 Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
 Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
 Ninaanza kujipinda, kwa mapambano hakika
 Hilo nakwambia

MASWALI

- a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili. (alama 2)
- b) Shairi hili ni la aina gani ? Toa ithibati. (alama 2)
- c) Yataje mambo yoyote matano anayoyalalamikia mwana. (alama 5)
- d) Eleza kanuni zilizotumika kusarifu ubeti wa tatu. (alama 5)
- e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. (alama 4)
- f) Eleza maana ya maneno haya yalivytumika katika shairi hili.
 - (i) jaza (alama 1)
 - (ii) muhibu (alama 1)

AU

8. SHAIRI B

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

1. Punda kalibebe gari, gari limebebe punda
 Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda
 Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda.
 Kinyume mbele

2. Saramala ahubiri, muhunzi tiba apenda
 Mganga anaabiri, baharini anakwenda
 Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
 Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda
 Mtazame askari, akazakaza kitanda,
 Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
 Kinyume mbele

4. Apakasa daktari, ukili anaupinda
 Saveya kawa jabari, mawe anafundafunda,
 Hazini wa utajiri, mali yote aiponda,
 Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda

Fahali hawasimami, wanene waliishakonda
 Walojitia utemi, maisha yamewavunda
 Kinyume mbele

6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
 Tele haitakadari, huvia tulivyopanda
 Mipango imehajiri, la kunyooka hupinda
 Kinyume mbele

MASWALI

- | | |
|--|-----------|
| a) Mtunzi alikuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? | (alama 3) |
| b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. | (alama 4) |
| c) Eleza namna mtunzi aliyyoutumia uhuru wake. | (alama 5) |
| d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? | (alama 2) |
| e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari. | (alama 4) |
| f) Eleza toni ya shairi hili. | (alama 2) |

KANDARA

102/1

KISWAHILI

INSHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA(1)

1. Mwanafunzi azingatie muundo wa wasifu.

- i) Kichwa
- ii) Mwili – maudhui kulingana na mada.
- iii) Hitimisho – umaarufu wake na sababu za kutambulikana.

Tanbihi

- i) Maelezo yawe ya kinatharia.
- ii) Aandike kwa mpangilio na mtiririko halisi wenye maana km, jina, umri, alikozaliwa, utoto wake, familia yake, elimu, makazi kazi na tajriba yake, matendo aliyoienda, pingamizi alizokumbana nazo, ushindi. n.k.
- iii) Atumie nafsi ya tatu.
- iv) Aaandike katika wakati uliopita.

2.

- Kupiga marufuku ajira za watoto
- Kutoa msaada wa karo kwa familia zisizojiweza kifedha.
- Kuwashimiza na kuwashauri wavulana kuijunga na shule.
- Kupiga marufuku uendeshaji wa pikipiki na wavulana ambao hawajahitimu katika kidato cha nne.
- Kupanua shule za wavulana zilizoko.
- Kuwe na sheria ya kulazimisha watoto wavulana kumaliza masomo yao.
- Alama za kuijunga na shule na vyuo kusawazishwa na za wasichana.
- Kuhamasisha wazazi na jamii kuhusu umuhimu wa elimu ya mvulana.
- Elimu bila malipo kwa shule na vyuo.

Tanbihi

Mtahiniwa akadirie hoja zozote zinazooana na swali.

3.

- i) Hii ni insha ya methali.
- ii) mtahini abuni kisa kinachodhahirisha maana ifuatayo:
 Mtu kutotambua umuhimu wa mtu au kitu/kutokithamini mpaka anapokikosa kile kitu km pesa, mali, wazazi, walimu, marafiki n.k.

4. Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JESHI LA WOKOVU JIMBO LA KENYA**MAGHARIBI(SAKWETET)****102/1****KISWAHILI****KARATASI YA 1****INSHA****1. Lazima**

Andika tahiriri itakayochapishwa katika Gazeti la Matumaini la shule yenu kuhusu faida na hasara za usafiri wa piki piki nchini.

2. Pendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuimarisha utalii kama kitega uchumi nchini.

3. Tunga kisa kuthibitisha ukweli wa maana ya methali: Maji ukiyavulia nguo yaoge.

4. Malizia kwa.....tulifumukana huku nyuso zetu zikiwa na tabasamu la matumaini.

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JESHI LA WOKOVU JIMBO LA KENYA**MAGHARIBI(SAKWETET)102/1****KISWAHILI****KARATASI YA II****LUGHA****UFAHAMU (Alama 15)****Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu, kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwanda mwanamke kuwa chombo kitifu cha mwanaume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kumtumikia mwanamume, kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shunghuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi nai husudu sana, ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya jiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya ushiri na uganga. Mwanamke yeoyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa napengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati zuri kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendelea katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia

Wanawake wengi wemakiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa kutochukua hatua za utekelezaji wa maazimio yaliyoendelea kupitishwa na umoja wa mataifa mwaka hadi mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengi yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa umoja wa mataifa wa wanawake (unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya umoja wa mataifa mionganini mwa shughuli nyingine katika mkabala huu. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengine. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende.

Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake. Kwa bahati mbaya, itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja naya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

Maswali

- i) Eleza chanzo cha dhuluma kwa wanawake. (alama. 2)
- ii) Huku ukitoa mafano, fafanua hali ya dhuluma kwa wanawake kama inavyodhihirika katika makala. (alama. 4)
- iii) Eleza hatua ambazo mwanamke amechukua kujikomboa (alama. 4)
- iv) Je, jamii imechangia vipi katika kumdunisha mwanamke (alama. 2)
- v) Fafanua maana ya misemo ifuatayo; (alama. 3)
 - i) Wamekiuka misingi
 - ii) Kupitishwa kwa maazimio
 - iii) Wanaojitolea mhanga

UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Ama kwa kweli maisha ya vijana wa kisasa yanatofautiana na kuhitilafiana na yale ya wazee wao. Sio katika mavazi, mienendo, mitazamo, mawazo na mielekeo tu bali pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria. Yote haya ni vielelezo vya jinsi kizazi cha leo kinavyoishi katika ulimwengu amba ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivytangulia. Baadhi ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe.

Kwao basi, si ajabu katu kuwaona vijana wakizungumza lughu yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhihirisha bayana maungo yao badala ya kuyasitiri.

Hata hivyo watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vijana wa leo ni maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao. Upande huu umetoa rai kwamba kizazi hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia. Wanazidi kufafanua kuwa nyendo hizi za ukarimu, unyenyevu, hadhari katika kila jambo, utiifu na pia kujitegemea. Yote haya yamesahauliwa ama tuseme yamepuuzwa katika “Utamaduni wa kisasa.” Swalilinalozuka sasa ni je, tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani? Tuwapige darubini kwa kutegeMEA hali ilivyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa mujibu wa jinsi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa. Jibu la swali hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini, lisije likaegemea upande wowote. Mathalan, ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaoathirika na hivyo kubadilika daima.

Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu, sayansi, mawasiliano na hata ufundi yalivyo yageuza maisha siku hizi. Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona na hata kuzungumza kwa wenzao kutoka Uropa, Asia na Marekani bila hata kunyanya hapa kwao nyumbani. Athari ya filamu, video, vitabu, magazeti, majarida na kadhalika haikadiriki. Haya, kwa kiasi yamefanya vijana hata kupevuka kabla ya wakati wao. Isitoshe, mambo hayo yameweza kuwazuzu na kuwaaminisha ya kuwa yale wanayojifunza ni kweli.

Matokeo yamekuwa ni wao kudunisha utamaduni wao wa asili na kuupapia ule wa wageni waliowaathiri. Tulisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akili kwa kupotoshwa na kucharika na yote wanayoyapokea kutoka ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wa Waafrika. Hata hivyo, badala ya kuwakashifu wanapopotea njia ama kuwapongeza wanapotenda yale tunayoyategemea tu, ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwaongoza na kuwasaidia vijana kuwa na uwezo mkubwa wa kufanya uteuzi mwafaka katika maisha yao.

- (a) Bila kupoteza maana asilia fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 40 (Alama 6, 1 ya utiririko)
 Matayarisho
 Jibu
- (b) Fufisha aya mbili za mwisho (maneno 50) (Alama 9, 1 ya utiririko)
 Matayarisho
 Jibu
- 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**
- (a) Taja irabu mbili za nyuma kisha ueleze kwa nini huitwa hivyo. (Alama 2)
- (b) Toa mfano mmoja kwa kila mojawapo. (Alama. 2)
- i) Kipasuo _____
 ii) Kitambaza _____
- (c) Eleza maana ya, (Alama. 2)
- i) Silabi
 ii) Mofimu
- (d) Bainisha viwalikishi katika sentensi ifuatayo
 Alimpiga mwanafunzi mtundu (Alama. 2)
- (e) Eleza maana mbili za sentensi hii
 Jane alifagia chakula chote (Alama. 2)
- (f) Ainisha matumizi ya ‘na’ katika sentensi (Alama. 2)
- i) Marafiki hawa hutembeleana sana _____
 ii) Amina ni tofauti na kakake _____
- (g) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali.
 Msichana mtukutu alifukuzwa shule leo asubuhi (Alama. 4)
- (h) Tunga sentensi kwa kutumia nomino katika ngeli ya pa- ku- mu. (Alama. 1)
- (i) Tambua na ueleze aina za vielezi katika sentinsi hizi.
 i) Mama alimwamrisha mtoto wake kijeshi
 Askari hutembea makundi makundi (Alama. 2)
- (j) Andika katika hali ya udogo
 Mbwa mwenye ukali alimfukuza mtoto (Alama. 2)
- (k) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumiza ya ritifaa (Alama. 2)
- (l) Tambua aina ya vitenzi kwa kutaja majina yake
 Babu angali anasoma gazeti (Alama. 2)
- (m) Kwa kutunga sentensi moja, tofautisha vitate hivi.
 i) Ghali
 ii) Gari (Alama. 2)
- (n) Tumia ‘O’ rejeshi. (Alama. 2)
- i) Msichana ambaye huja ni mwanasheria
 Maovu ambayo aliyatenda hayasahauliki
- (o) Andika katika msemo wa taarifa; (Alama 3)
 “Tusipofanya kazi yetu kwa bidii na kujitegemea, tutabaki kuwa watumwa katika nchi yetu” Rais alisema.
- (p) Kanusha sentensi hii
 Ugonjwa huu ungalidhibitiwa mapema kifo kingaliepukwa (Alama. 2)
- (q) Tambua shamirisho kipozi, kitondo na shamirisho ala katika sentensi ifuatayo.
 Baba amemnunulia mtoto fulana nzuri iliyoshonwa kwa uzi mwekundu. (Alama.3)
- (r) Badilisha katika kauli ya kutendua.
 Tundika piche hiyo ukutani na uyabandike maandishi kitabuni. (Alama 2)
- (s) Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi (Alama 2)
- Tumeanzisha shirika ili tunyanyue hali yetu **4. ISIMU JAMII (Alama 10)**
- (a) Eleza juhudzi zozote **tano** zinazotumiwa kukiendeleza Kiswahili sanifu nchini Kenya. (Alama 5)
- (b) Eleza jinsi uwililuga unaweza kuleta athari katika lugha na mawasiliano mionganoni mwa wanajamii. (Alama. 5)

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JESHI LA WOKOVU JIMBO LA KENYA**MAGHARIBI(SAKWETET)****102/3****KISWAHILI****KARATASI YA 3****FASIHI****SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI****LAZIMA**

1. A) i)Taja aina mbili za maghani (Al.2)
 ii) Eleza matatizo ya utafiti anayoweza kukumbana nayo mwanafasihi kule nyanjani (Al.8)
- B) i) Misimu ni nini? (Al.2)
 ii)Eleza umuhimu wa misimu. (Al. 8)

SEHEMU B: Tamthilia**Kigogo : Na Pauline Kea**

2. “Fungua macho uone. Keki ya uhuru imeliwa kwingine, mwaletewa masazo”
 a) Eleza muktadha wa usemi huu. (Al. 4)
 b) Thibitisha ukweli wa kauli kuwa keki ya uhuru imeliwa kwingine. (Al.8)
 c) Eleza vizingiti vinavyomkabili mnenaji katika harakati za kusaka keki . (Al.4)
 d) Jadili jazanda zinazojitokeza katika usemi huu. (Al.4)
- AU**
3. a.) Kwa kutumia mifano nane kutoka tamthilia, onyesha jinsi viongozi hutumia mamlaka yao vibaya (Al.8)
 b.) Ukrejelea tamthilia, eleza nafasi sita chanya na nafasi sita hasi walizopewa wahusika wa kike (Al.12)

SEHEMU C: RIWAYA.**Chozi la Heri: Na Assumpta Matei**

4. “.....ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde, vitisho na matusi?”
 a) Eleza muktadha wa dondo hili. (Al.4)
 b) Taja mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika döndoo hili? (Al.2)
 c) Fafanua umuhimu tatu wa msemajii wa maneno haya katika kuendeleza ujumbe wa riwaya (Al.6)
 d) Jadili jinsi mbinu ya kinaya ilivyotumiwa na mwandishi katika riwaya hii kwa kutoa mifano nane. (Al.8)

AU

5. a) Kwa kutumia mifano kumi, dhihirisha ufaafu wa anwani “Chozi la Heri” (Al.20)

SEHEMU D: HADITHI FURI**Tumbo lisilohiba na Hadithi Nyingine: Na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda – wahariri.****SHIBE INATUMALIZA**

6. “Ndugu yangu kula kunatumaliza”
 “Kunatumaliza au tunakumaliza”
 a) Fafanua muktadha wa dondo hili. (Al.4)
 b) Jadili maana ya ndani/kitamathali katika kauli “kula tunakumaliza” (Al.10)
 c) Ukrejelea mifano sita, onyesha ni kwa namna gani kula kunawamaliza watu wa jamii hii. (Al.6)
- AU**
7. a) Kwa mujibu wa hadithi ya “Mame Bakari” ubahaimu unaotendewa mwanamke umekuwa na athari mbaya kwake. Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kutumia mifano mwafaka. (Al.10)
 b.) Huku ukitumia mifano kumi, dhihirisha kuwa masharti ya kisasa ni anwani mwafaka kwa hadithi hii. (Al. 10)

SEHEMU E: USHAIRI**8. Soma shairi lifuatatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Punda kalibeba gari, gari limebeba punda
 Mwalimu anapakari, muashi vyuma adunda
 Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda

Kinyume mbele.

SaramAla ahubiri, muhunzi tiba apenda
 Mganga anaabiri, baharini anakwenda
 Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
 Kinyume mbele.
 Wakili ana hiyari, biashara kutenda
 Mtazame askari, akaza kaza kitanda
 Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
 Kinyume mbele
 Apakasa daktari, ukili anaupinda
 Saveya kawa jabari, mawe anafundafunda
 Hazini wa utajiri, mali yote aiponda.
 Kinyume mbele

Msemi huwa hasemi , wa inda hafanyi inda.
 Fahali hawasimami, wanene walishakonda
 Waliojitia utemi, maisha yamewavunda
 Kinyume mbele.

Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
 Tele haitakadiri huvia tulivyopanda
 Mipango imehajiri, la kunyooka hupinda.
 Kinyume mbele.

MASWALI

- a) Mtunzi alikuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? Taja matatu. (Al.3)
 - b) Licha ya tarbia, taja na ueleze bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. (Al.4)
 - c) Jadili jinsi idhini ya mshairi iliviyotumiwa katika shairi hili kwa kutumia mifano minne (Al.4)
 - d) Uandike ubeti wa nne kwa lugha tutumbi (Al.4)
 - e) Eleza toni ya shairi hili. (Al.2)
 - f) Eleza maana ya maneno haya kama yaliviyotumiwa katika shairi.
- i. Inda
 - ii. Utemi
 - iii. Imehajiri.

MTIHANI WA SHULE ZA JESHILLA WOKOVU (SAKWETET) MAY 2019

Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari(K.C.S.E)

KARATASI YA I- INSHA

MWONGOZO WA KUSAHIIHISHA

a

1. Hii ni tahariri
 Vipengele viwili muhimu ni:
 - i) Sura
 - ii) Maudhui

Sura

Izingatie

1. Jina la gazeti
2. Tarehe
3. Mada
4. Maelezo kuhusu faida na hasara katika aya.
5. Jina la mhariri

Maudhui

Faida

1. Zimebuni nafasi za kazi kwa maelfu ya vijana – huzuia uhalifu.
2. Bei ni nafuu- vijana wanaweza kujimudu

- (r) Kanusha sentensi:
Bawabu huyu amekuwa akitaka kuacha kazi tangu mwaka jana.
- (s) Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo.
Adika alibebewa viazi na Amina kwa torohi. (al 3)
- (t) Andika kinyume cha sentensi:
Hamisi alimwoa Khadija akiwa amelewa (al 2)

ISIMU JAMII

1. Jadili mitazamo au nadharia tano zinazofafanua chombuko au asili ya Kiswahili. (al 5)
2. Eleza umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya taifa. (al 5)

SHULE YA UPILI YA TRIAL 1**102/3****KISWAHILI****FASIHI YA KISWAHILI****MTIHANI WA KABLA YA MWIGO 2019****TAMTHILIA****1. Kigogo**

Tamthilia ya Kigogo ni ‘kioo’ cha hali halisi ya mambo barani Afrika. Jadili. (al 20)

SHAIRI**2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nilicheza ujanani, nisikieni wendani
Nimeishi duniani, zaidi nyaka sitini
Sikufanya cha manani, kiniponye uezee ni
Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda shuleni
Waloenda darasani, sasa wako magarini
Wananipita njiani, wakinipiga honi
Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda shambani
Hakataa kutuwani, jembe liwe mikononi
Na sasa niko njaa ni, wenzangu wako shibeni
Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, haiza kwenda sokoni
Walioza juani, sasa wala vivulini
Na mimi sina thumuni, initoe mashakani
Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, ndoa sikuthamini
Waliooa yakini, niliwaona watini
Sasa niko ukongweni, bila yejote nyumbani
Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, kutwa kucha magomani
Niliharibu mapeni, ulevini danguroni
Niliufanya uhuni, bila kuola usoni
Nilichjeza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, sasa niko kilioni

Ninalala kibandani, sina mali asilani
 Sina watoto olani, wala chakula ghalani
 Nilicheza ujanani, ninalipa uezee ni

Nilicheza ujanani, sasa najuta Fulani
 Machozi tele machoni, sina wa kuniauni
 Ninamuomba Manani, amionee Imani
 Ninacheza ujanani, ninalipa uezee ni

Maswali

- (a) Eleza toni ya shairi hili. (al 2)
- (b) Fafanua umbo la shairi hili. (al 4)
- (c) Fafanua mambo matano ambayo msharri aliyapuuza akiwa kijana na namna anavyoathiriwa nayo. (al 5)
- (d) Fafanua bahari katika shairi hili. (al 3)
- (e) Andika ubeti wa sita katika lugha ya nathari. (al 4)
- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliviyotumiwa katika shairi hili. (al 2)
 - (i) Danguroni
 - (ii) kuola

AU

3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Mwili na fahamu
 zilikuwa kitandani
 Usingizini mnono

Ghafla, ikaha ndoto
 Ndoto ya kutisha
 Na kubabaisha
 Ndoto ya jasho
 Na joto kali-
 Jinamizi!

Kaumu ya watu
 Ikibeba shoka
 Panga kali
 Na misumeno inayonguruma
 Ilikuja kwa mawimbi
 Na bila huruma
 Ikajinja miti
 Na kunyunga chemichemi
 Ikiimba wimbo
 Za mashamba na mbao

Ardhi iliachwa uchi
 Kama mkazi wa kijiji
 Aliyeshambuliwa njiani
 Na kundi la majambazi

Kijinga cha juu
 Kiliunguza udongo,
 Viganja vyaa upopo

Viliufikicha kwa nguvu
 vumbi jekundu
 Lilanza kupaa angani
 Kama wimbo wa matanga
 Katika kijiji ambacho
 Kinatawaliwa na kipindipindu

Mvua ilikuja kwa hasira
 Kwa kucha zake ndefu
 Ililujumu ardhi
 Na kuacha majeraha
 Yatiririka damu
 Polepole, ardhi nzima
 Illegeuka bahari
 Siyo ya maji ya chumvi
 Siyo ya mikamba na sulisuli
 Bali mawimbi makuu
 Ya machanga na vumbi

Povu lilirushwa
 Na kutua juu ya mawe
 Tanzu za miti
 Na nywele
 Mvua ilipokuja tena
 Katika mashamba
 Pojo na mbaazi
 Zilikwama njiani
 Ya maisha

Katika kijiji
 Ng'ombe, kondoo na mbuzi
 Walibadilika sura
 Na kuwa mafupa
 Yanayojisukuma njiani
 Kama makobe makongwe

Kama abiria
 Katika dau
 Katika bahari ya kusi
 Binadamu, wanyama
 Mimeea, wadudu na ndege
 Walitingishwattingishwa
 Na kusukwasukwa
 Na bahari ya mashaka

Wingu la huzuni
 Lilifunika vijiji
 Kama wingu la anga
 Likifunika vilima

Mazizini na njiani
 Waliangkiana magombe
 Kama majani makavu
 Yakiangushwa na upepo
 Majira ya mpukutiko

Provided for free by www.freekcsepapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

Katika nyua za kijiji
 Machozzi yalibubujika
 Kama maji maasi
 Kutoka mifereji iliyopasuka

Walizikwa watoto
 Na wazee
 Na hatimaye samba
 Ambao kabla ya janga
 Walingara kwa afya

Kupitia ukungu mwekundu
 Sauti ya kejeli
 Ilisikika, ikiimba

Ndimi jangwa
 Niogopewa na mvua
 Ndimi jangwa
 Ninyongaye mito
 Ndimi jangwa
 Ninyimaye mayai, maziwa na nyama
 Ndimi jangwa
 Nihiniye mboga, nafaka na matunda
 Ndimi jangwa
 Mtawala weni!

Maswali

- (a) Hili ni shairi gani? Dhihirisha. (al 2)
- (b) Huku ukitoa mifano kwenye shairi hili, eleza sifa mbili za mashairi ya aina hii. (al 2)
- (c) Mshairi anazungumzia nini katika shairi hili? (al 1)
- (d) Fafanua athari ya anachokizingumzia mshairi katika shairi hili. (al 6)
- (e) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza taswira mbalimbali katika shairi. (al 4)
- (f) Huku ukitoa mifano kwenye shairi, onyesha matumizi ya mishata katika shairi. (al 2)
- (g) Huku ukitoa mifano mwafaka, taja tamathali mbili zilizotumiwa katika shairi. (al 2)
- (h) Eleza maana ya kauli ifuatayo; Mazizini na njiani yaliangukianan magombe. (al 1)

RIWAYA

Chozi la Heri

- 4. Anwani “Chozi la Heri” inaadiki riwaya hii. Thibitisha. (al 20)
AU
- 5. “Ni kweli, mama ana haki ya kusamehewa kwani hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika.”
 (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (al 4)
 (b) Jadili umuhimu wa mzungumzaji katika riwaya hii. (al 6)
 (c) Fafanua maudhui ya ukatili kama yaliyvosawiriwa katika riwaya ya Chozi la Heri. (al 10)

HADITHI FUPI

Tumbo Lisilosiba na Hadithi Nyingine

- 6. Ndoto ya Mashaka (Ali Abdulla Ali)
 Jadili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya ‘ndoto ya Mashaka’. (al 20)
AU

7. Mtihani wa Maisha (Eunice Kimaliro)

- “Nimeuza ng’ombe wangapi kwa ajili ya kisomo chako kumbe wewe ni mbumbumbu huna kumbukumbu?”
- (a) Andika muktadha wa dondo hili. (al 4)
 - (b) Kwa kurejelea hadithi hii, onyesha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari. (al 4)
 - (c) Bainisha matumizi ya kinaya katika hadithi hii. (al 12)

8. FASIHI SIMULIZI (al 20)

- (a) Eleza maana ya ‘malumbano ya utani’. (al 1)
(b) Jadili sifa tano za malumbano ya utani. (al 5)
(c) Bembelezi ni nyimbo za kuwabembeleza watoto ili walale au kunyamaza wanapolia. Fafanua aina nyingine kumi za nyimbo. (al 10)
(d) Nyimbo zina hasara gani katika jamii? (al 4)

Provided for free by www.freekcsepastpapers.com - Trusted and Used by Over 7000 Subscribers

MTIHANI WA PAMOJA WA JIMBO LA KIANGILIKANA LA NAMBALLE-2019**KISWAHILI 102/1****Karatasi ya 1****INSHA****MASWALI****LAZIMA**

1. Wewe kama rais umekerwa na kukithiri kwa ujisadi katika wizara mbalimbali. Andikia arifa mawaziri wako ukiwaeleza madhara ya ujisadi na hatua utakazochukua ikiwa hawatakomeshu ujisadi katika wizara zao. (alama 20)
2. Dhuluma katika asasi ya ndoa haiathiri tu wanajamii husika nyumbani bali elimu ya watoto wao pia. Fafanua. (alama 20)
3. Andika kisa kinachoafiki methali:.... Usishindwe kupika ukasingizia jiko la moshi. (alama 20)
4. Andika insha itakayokamilika kwa maneno yafuatayo:
.....Ni jicho gani lisilolengwalengwa na chozi la mshangao na huzuni kwa kushuhudia unyama wa aina hii. Wanadamu wamesahau kuwa mtu ni utu. (alama 20)

MTIHANI WA PAMOJA WA JIMBO LA KIANGILIKANA LA NAMBALLE - 2019**KIDATO CHA NNE****102/2****KISWAHILI****Karatasi ya 2****LUGHA****1. UFAHAMU: (ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautito fauti. Njia za mawasiliano zimebadilika sana katika historia ya binadamu. Kwa mfano, zamani ingechukua siku nyingi kupitisha ujumbe baina ya watu wanaoishi sehemu mbalimbali. Siku hizi ujumbe hupitishwa katika sekunde chache katika masafa marefu.

Ugunduzi wa simu uliofanywa na Alexander Graham Bell mwaka wa 1876 ulifungua ukurasa mpia katika mawasiliano. Nchini Kenya, miaka ya sabini na themanini, ilikuwa vigumu kupata huduma za simu. Mtu alihitajika kusafiri masafa marefu ili kupata huduma hizo hasa kwa wale walioishi mashambani. Aidha kutokana na ukosefu wa huduma hizo katika sehemu nyingi, mtu alihitaji **kupiga foleni** ili ahudumiwe ama ajihudumie.

Baadaye, simu tampa zilivumbuliwa na mawasiliano yakarahisishwa. Mwanzoni, simu tampa zilikuwa vidude vikubwa ambavyo havikutoshea mifukoni. Hata hivyo, usumbufu huo ultafutiwa suluhu. Siku hizi simu tampa ni ndogo na hivyo huwa rahisi kuzibeba. Aidha, kampuni za kutoa huduma za mawasiliano na kufanya gharama ya kupiga simu kuenda chini.

Barua pia ni njia ya mawasiliano na imetumika kwa muda mrefu. Baadhi ya nchi kuliko tumiwa barua katika enzi za zamani ni Misri na Uyunani. **Matarishi** walitumwa kupeleka barua. Barua zilichukua muda mrefu kufikia aliyeandikiwa. Aidha kutokana na kwamba si watu wote waliojua kusoma na kuandika, wachache waliokuwa na maarifa hayo waliwandikia na kuwasomea. Katika enzi hizi matumizi ya barua yamepunguza kwa kiwango kikubwa na tarakilishi na simu tampa. Kwa kutumia tarakilishi unaweza kutuma barua pepe. Aidha, kwa kutumia simu tampa unaweza kutuma arafa.

Waajiri wengi hupendekeza wanaoomba kazi watume maombi yao kwa kutumia baruapepe. Njia hii huondoa uwezekano wa wanaoomba kazi kutumia ujisadi ili wapate kazi. Aidha, njia hii husaidia kutunza mazingira kwani karatasi hazitumiwi. Katika elimu tarakilishi zinatumwa shulenii kufundishia hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, kupitia tarakilishi iliyotandawizwa ama kuunganishwa kwa mtandao, watu huweza kujuliana hali na kupashania habari mbalimbali kutoka pembe zote za dunia. Changamoto katika hatua hii ni ukosefu wa nguvu za umeme hasa mashambani. Aidha, gharama ya kununua tarakilishi ni kali

mno hasa kwa mataifa yanayoendelea ikizingatiwa kuwa yana changamoto za kimsingi kama vile kutojua kusoma na kuandika, magonjwa na umaskini.

Vilevile, redio ni chombo muhimu ambacho huchangia sana katika mawasiliano. Kwa sasa, hiki ndicho chombo cha pekee kinachomilikiwa na karibu kila familia. Hali hii inachangiwa na ukweli kwamba kunazo redio ndogo ambazo hutumia betri. Chombo hiki huwapitishia matangazo na habari kuhusu yanayotendeka kutoka pande zote za ulimwengu. Redio hufahamisha, huburudisha na kuelimisha. Wizara ya Elimu imekuwa ikitumia redio kufundishia masomo mbalimbali hasa katika shule za msingi.

Nani asiyejua kuhusu runinga? Chombo hiki pia hutoa mchango mkubwa katika mawasiliano. Runinga hushirikisha hisi za kusikiliza na kuona, kwa hivyo mawasiliano yake hufanikiwa sana. Hata hivyo, ni asilimia ndogo ya watu ambao wanaweza kuimiliki kutokana na gharama yake na pia si wengi wanazo nguvu za umeme majumbani mwao.

Mwalimu ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii oyote. Ni dhahiri shahiri mwasiliano ni sehemu muhimu katika kuimarika kwa uchumi. Vile vile huwezesha watu kutangamana na kubadilishana mawazo. Binadamu si kama visiwa vinavyosimama peke yavyo. Binadamu huhitaji kutangamana na binadamu wengine katika maisha na kwa hivyo mawasiliano ni muhimu.

- a) Eleza kini cha taarifa hii. (al. 1)
- b) Toa sababu mbili za waajiri kuhimizi matumizi ya barua pepe. (al. 2)
- c) Kwa nini redio ndicho chombo kinachotegemewa zaidi katika mawasiliano. Eleza sababu nne. (al. 4)
- d) Kwa mujibu wa kifungu hiki eleza udhaifu wa tarakilishi. (al. 3)
- e) Eleza faida mbili za tarakilishi. (al. 2)
- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (al. 2)
 - i) Kupiga foleni
 - ii) Matarishi

2. UFUPISHO:(ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejeua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameellezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgongjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

- a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65
Matayarisho
Jibu (alama 10, 1 ya utiririko)
- b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho
(Maneno 30)
Matayarisho
Jibu (alama 5 utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili nya silabi moja. (al. 2)
 b) i) Eleza maana ya sauti za likwidi. (al. 1)
 ii) Toa mifano ya sauti za likwidi. (al. 1)
 c) Ainisha mofimu: Lililoliwa (al. 3)
 d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi ‘ji’. (al. 2)
 e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi katika sentensi, weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka. (al. 2)
 i) Uwele.....
 ii) Vita
- f) Tumia ‘O’ rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo. (al. 1)
 Tawi limekauka
 Tawi limeanguka
- g) Tambua vivumishi na uonyeshe ni nya aina gani. (al. 3)
 Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.
- h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa. (al. 1)
- i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii: (al. 2)
 Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.
- j) Unda nomino kutokana na kitenzi ‘Haribu’ (al. 1)
- k) Tambua aina za vitenzi katika sentensi. (al. 2)
 Hawa sio wachezaji bali wamekuwa wakichezea timu hii.
- l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi nya kulinganua. (al. 1)
- m) Eleza matumizi mawili ya ‘ka’ . Toa mifano katika sentensi. (al. 2)
- n) Andika visawe ya maneno yafuatayo (al. 2)
 i) Daawa
 ii) Ainisha
- o) Onyesha kwa kauli ulizopewa (al. 1)
 i) Ja (tendewa)
- p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa. (al. 1)
- q) Chanana sentensi hii kwa kutumia vishale. (al. 4)
 Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.
- r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al. 2)
 Oyula atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo.
- s) Eleza majukuma mawili ya chagizo huku ukitoa mifano. (al. 2)
- t) Akifisha. (al. 3)
 sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote kumbuka
- u) Andika ukubwa wa sentensi katika wingi. Nyundo imo ndani ya kibweta. (al. 1)
- 4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
- a) Eleza matatizo matano yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili. (al. 10)

MTIHANI WA PAMOJA WA JIMBO LA KIANGILIKANA LA NAMBALE**102/3****KISWAHILI YA 3.****FASIHI.****SEHEMU A : RIWAYA – LAZIMA**

1. Fafanua ufaafu wa anwani ‘Chozi la Heri’ (al. 20)

SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOZO

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!
- Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)
 - Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (al. 4)
 - Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. (al. 2)
 - Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia. (al. 10)

Au

3. Ni bayana kwamba viongozi wengi nchi zinazoendelea wamejawa na tama na ubinafsi. Thibitisha kauli hi ukirejelea tamthilia Kigogo (al. 20)

4.

SEHEMU C: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE**SHIBE INATUMALIZA**

5. “Ndugu yangu kula kunatumaliza”
“Kunatumaliza au tunakumaliza”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b) Fafanua maana kitamathali katika kauli ‘Kula tunakumaliza’ (al. 10)
c) Kwa mujibu wa hadithi hii, kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (al.6)

Au

- a) ‘MAME BAKARI’

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake, onyesha kwa mifano mwafaka. (al. 10)

- b) ‘MASHARTI YA KISASA’

“..... mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni ushabiki usio na maana.”

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi. (al. 10)

SEHEMU D : USHAIRIA**6. MWANA**

1. Kwani mamangu u ng’ombe, au u punda wa dobi ?
Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
Hebu nambie
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA

2. Nang’ona mwana nang’ona, sitafute angamiyo
Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
Kwani kelele kunena, huyataki maishayo ?
Hilo nakwambia.

MWANA

3. Sitasakamwa. Kauli, nikaumiza umiyo
Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo
Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
Baba hafanyi halali, huachi vumiliyo
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni
 Nini yako matulubu, kulima hadi jioni ?
 Na jembe ukudhurubu, ukilitua guguni
 Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
 Hebu nambie.
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
 Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani.
 Hajali hakudhamini, wala haoni huzuni.
 Mwisho wa haya ni nini ? ewew mama wa imani ?
 Hebu nambie.
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
 Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika
 Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
 Ukichelewa vituko, baba anakutandika
 Hebu nambie.
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
 Kiishapo u mbioni, wapiti kupokapoka
 Urudi nje mekonzi, uanze kushughulika
 Ukitosa kisirani, moto nyumbani wawaka
 Hebu nambie.
 Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA

Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
 Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
 Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
 Ninaanza kijipanga, kwa mapambano hakika
 Hilo nakwambia

MASWALI

- a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhaimira gani katika kutunga shairi hili (al. 2)
- b) Shairi hili ni la aina gani. Toa ithibati (al. 2)
- c) Yataje mambo yoyote matano anayolalamikia mwana (al. 5)
- d) Eleza kanuni zilizotumika kasarifu ubeti wa tatu (al. 5)
- e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi (al. 4)
- f) Eleza maana haya yaliyotumika katika shairi hili
 - i) Jaza (al. 1)
 - ii) Muhibu (al. 1)

7. SHAIRI B

Soma shairi hili kisaha ujibu maswali

1. Punda kalibebi gari, gari limebeba punda.
 Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda
 Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda
 Kinyume mbele.
2. Saramala ahubiti, muhunzi tiba apenda
 Mganga anabiri, baharini anakwenda
 Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
 Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda
Mtazame askari, akazakaza kitanda,
Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
Kinyume mbele
4. Apakasa daktari, ukili anaupinda
Seveya kawa jabari, mawe anafundafunda,
Hazini wa utajiri, mali yote aiponda,
Kinyume mbele
5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda
Fahali hawasimami, wanene walishakonda
Walojitia utemi, maisha yamewavunda
Kinyume mbele
6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
Tele haitakadiri, huvia tulivyopanda
Mipango nmehajiri, la kunyooka hupinda
Kinyume mbele

MASWALI

- a) Mtunzi aliuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? (al. 3)
- b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. (al. 4)
- c) Eleza namna mtunzi alivyotumia uhuru wake. (al. 5)
- d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? (al. 2)
- e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari (al. 4)
- f) Eleza toni ya shairi hili (al. 2)

SEHEMU E**7. FASIHI SIMULIZI**

1. Eleza vigozi vinne vya kuandika methali (al. 4)
2. Eleza fani zinazozijenga vitendawili vifuatavyo (al. 4)
 - i) Ajenga ingawa hana mikono
 - ii) Jani la mgomba laniambi habari zinazotoka ulimwenguni kotew
3. Nini tofauti kati ya misimu na lakabu ? (al. 2)
4. I) Miviga ni nini ? (al. 2)
 - ii) Fafanua hasara zozote tano za miviga
5. I) Tambua kipera cha maka yafuatayo
“ Wewe ni mbumbumbu kiasi kwamba ukiona picha yako kwenye kioo unashangaa ulimwona wapi mtu huyo”.
 - i) Ngomezi ni nini? (al. 1)

MTIHANI WA PAMOJA WA MOMALICHE AWAMU YA 2**KIDATO CHA NNE, MUHULA WA KWANZA**

102/1

KISWAHILI**KARATASI YA I****Karatasi 1**

1. Andika barua kwa mwenyekiti wa Tume ya kupambana na ufisadi ikipitia kwa katibu wa tume hio, huku ukieleza madhara ya ufisadi na jinsi ya kukabiliana na ufisadi nchini. (alama 20)
2. Kugatuliwa kwa huduma za matibabu kutoka serikali kuu kumeleta maumivu kuliko tiba kwa wananchi. Jadili (alama 20)
3. Andika kisa kinachothibitisha ukweli wa methali. (alama 20)
Pang'okapo jino pana pengo
4. Tunga kisa kinachomalizia kwa maneno yafuatayo: (alama 20)
.....kwakweli, penye nia hapakosi njia.

MOMALICHE AWAMU YA SITA, MTIHANI WA PILI

102/2

KISWAHILI**KARATASI YA PILI****SEHEMU YA A**
UFAHAMU

Ithibati ya maendeleo ya kiteknoloJia nchini Kenya tayari ipo.

Binafsi, nimeshuhudia teknolojia ya juu katika miundo ya simu na kompyuta,mifumo ya malipo ya kidijitali,mawasiliano na matumizi ya roboti yakizidi kurahisisha kazi katika sekta nyingi humu nchini.

Kila mwana uchumi atakubaliana nami kwa kuwa teknolojia ni nguzo muhimu katika kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Lakini mbona uzalishaji umepungua katika miongo michache iliyopita,katika kipindi ambapo teknolojia nyingi zilivumbuliwa? Sababu ni nini?

Nikichunguza data katika mataifa mengi ,hasa ya kiafrika,uzalishaji umepungua tangu mwanzo wa karne ishirini ya moja(21). Kumekuwa na sababu nyingi zilizochochea kushuka kwa utengenezaji wa bidhaa viwandani.

Sababu si teknolojia zenyewe bali ukosefu wa kueneza teknolojia hizo kufikia kila mwananchi kwa mfano, programu ya “my dawa” ni nzuri lakini ni wakenya wangapi wana uwezo wa kumiliki simuya kisiasa ili kufaidika na huduma zake?

Ili kila mkenya aweze kumudu bei ya simu kisasa,basi uchumi wafaa kuimarika kiasi cha kuwa na hela za ziada za kununua vifaa vya kiteknolojia.

Kila mkenya anatambua kuwa ufisadi umelemaza kila sekta ya uchumi wetu,lakini hiki si kikwazo pekee cha teknolojia kukosa kuwafikia wananchi wa matabaka ya chini.

Hali hii pia inasababisha kampuni saba zilizokuwa zimeorodheshwa katika soko la hisa la Nairobi (NSE) kuondolewa kutokana na mapato ya chini kama licha ya kutumia teknolojia kuimarisha uzalishaji.

Kudorora kwa uzalishaji kunahusiana moja kwa moja na kupanuka kwa pengo na mapato baina ya matabaka mbalimbali ya kiuchumi. Kwa mfano ,kampuni ya Safaricom inapata faida kubwa zaidi kwa sababu teknolojia yake ya M-pesa imeenea kote,huku kampuni pinzani zikiumia.

Hivyo , serikali kupitia mamlaka ya ushindani yafaa kuondoa vikwazo vinavyozua ushindani,na kuweka kanuni zinazozima ukiritimba.

Tukiachia kampuni chache umiliki wa soko husika, tutakuwa tunazuia kufurahia matunda ya teknolojia, hakuna haja ya wagonjwa kukwama mashinani eti kwa sababu hawana simu za kupata huduma za kiafya kidijitali.

Teknolojia haitakuwa na maana iwapo mamilioni ya wakulima hawana uwezo wamiliki simu yenyeye apu inayowaunganisha na soko la mazao yao pamoja na kuwaelekeza kwa maduka yenyeye dawa na mbegu za bei nafuu. Utazidi kuumia iwapo tutaachia Safaricom idhibiti soko la kutuma hela kidijitali.

Sera kuhusu teknolojia nchini zafaa kuboreshwa ili kuvumisha ubunifu na kueneza hadi mashinani.Kuna raha gani kuwa teknolojia nyingi zisizosaidia kukuwa kwa uchumi wetu? Teknolojia isiyoenea itazidi kulemaza uzalishaji tusipochukua hatua.

Maswali

- a). Yape makala uliyoyasoma anwani mwafaka. (al.1)
- b). Toa sababu za teknolojia kulemaza uzalishaji wa mali. (al. 4)
- c) . Kwa mujibu wa makala haya ni nini umuhimu wa teknolojia. (al.2)
- d) . Ni hatua ipi serikali inastahili kuchukua ili kuzuia ukiritimba (al.2)
- e). Ni nini msimamo wa mwandishi kuhusu teknolojia (al.2)
- f) . Fafanua msamiati huu kimuktadha (al.2)

Idhibati

Ukiritimba

SEHEMU YA B

Ufupisho.

Kuibuka kwa ripoti kwamba walangazi wa mihadarati huwa wanatumia washirika wao kuendesha biashara hiyo haramu kunapaswa kuzindua asasi za usalama kuimarisha mbinu zake kuikabili.

Uchunguzi wa polisi ambao umedumu kwa miaka kumi na nne umebaini kwamba washirika hao huwa majamaya na marafiki wa karibu ,ambao buhusika katika ununuzi na usambazaji wa dawa hizo bila ufahamu wa asasi za usalama. Ufichuzi huo unajiri wakati ambapo Kenya imetajwa kama mojawapo ya mataifa yanayotumika na walangazi wa kusafirishia dawa hizo kuelekea sehemu mbalimbai duniani.

Vile vile ,imeibuka kwamba wakenya wengi wamekuwa wakitumika wasafirishaji wa dawa hizo,hasa vijana.

Si mara moja tumeschia visa vya wakenya wanaotumikia vifungo gerezani katika mataifa mbali mbali wanakamatwa wakisafirisha dawa hizo, hasa katika viwanja vya ndege.

Kinaya kikuu kuwa kwamba bahadhi ya wanaokamatwa katika nchi hizo huwa wamekwepa mitego ya polisi na maafisa wa idara ya uhamiaji nchini.

Kwa haya yote umefikia wakati ambapo asasi zetu za usalama zinafaa ziimarishe mikakati ya kuwakibili walangazi hao kwani wengi wanatumia njia za kisasa kuiendesha .

Mawasiliano kati ya walangazi pia yameimarika, ikibainika kwamba huwa wanatumia vifaa vya kiteknolojia ambavyo huhakishwa kuwa asasi za usalama haziwanasi kwa urahisi.

Ni kinaya kwamba licha ya kashfa nyingi ya mihadarati kufichuliwa nchini,ni washukiwa wachache tu huwa wanakamatwa au kuhukumiwa.

Wale ambao hushtakiwa baadaye huachiliwa katika hali tatanishi,kwa kupewa dhamana ndogo wanazolipa kwa urahisi.

Katika nchi kama uchina, adhabu za walangazi wa mihadarati huwa kali,kiasi kwamba baadhi yao hupigwa risasi au hupewa vifungo nya maisha gerezani.

Swala hili ni geni nchini,kwani kuna ripoti nyngi ambazo zimetayarishwa zinazoenyeha jinsi baadhi ya viongozi wanahusika katika biashara hizo.

Kutokana na ufichuzi huo wakati sasa umefika kwa polisi ,idara ya upelelezi na asasi nyngine za usalama kushirikiana kuhakisha kwamba wahusika wote wananaswa wote wa biashara hiyo wananaswa na kukabiliwa vikali kisheria.

Hiyo ndiyo njia pekee ya kuwanusuru maelfu ya vijana waliogeuka watumwa wa matumizi ya mihadarati

Ahendera: kumi mingi.

Aziz: Haya ingia twende. Driver imeshona twende.

Maswali

a. Eleza muktadha wa mazungumzo haya

(al.4)

Maswali

a) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika ayasita za kwanza.

(maneno 40) (al.8)

b) Fafanua udhaifu wa polisi unaojitekeza katika taarifa hii

(maneno 67-70) (al.7)

SEHEMU YA C

MATUMIZI YA LUGHA (al .40)

a) Taja sauti moja ambayo ni kipasuo- kwaruzo hafifu cha kaakaa gumu

(al.1)

b) Tofautisha kati ya silabi wazi na fungo,huku ukitoa mfano mmoja mmoja

(al.2)

c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi “li”

(al.2)

d) Tunga sentensi mbili katika wingi ukitumia viunganishi vifuatavyo:

(al.4)

i) yamkini

ii) labda

e) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha maumbo matatu ya ngeli U-ZI.

(al.3)

f) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani.

(al.2)

i) Rajani alianguka mchangani pu!

ii) Maria anapenda kurandaranda ovyo

g) Hii sentensi ni aina gani? Thibitisha.

(al.2)

Atakuwa akiimba na kurukaruka leo jioni,wageni waketipo mezani.

h) Ainisha mofimu katika neno hili.

(al.4)

Aliyemchelewesha

i) Tunga sentensi mbili kwa kutumia aina mbili za virejeshi.

(al.4)

j) Iandike sentensi hii upya kwa kuanza na:kando ya barabara ...

(al.2)

Mti mrefu umeanguka kando ya barabara .

(al.2)

k) Changana sentensi hii ukitumia jedwali Ijapokuwa ye ye ni mweusi tititi, ni mrembo mno.

l) Tunga sentensi katika umoja ukitumia kuhusishi cha hali.

(al.2)

m) Andika sentensi hii kwa msemo wa taarifa:

“Enyi wanafunzi watundu ,rudini nyumbani mwenu,mje kesho asubuhi na wazazi wenu,” Mwalimu mkuu alisema kwa sauti ya juu.

(al.3)

n) Nyambua vitenzi vifuatavyo kulingana maagizo katika mabano na kisha utungie sentensi katika hali uliyonyambua .

(al.4)

a.Zoea (kutendeka)

b. Pata (kutendana)

o) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi hii .

(al.3)

Maria amelimiwa shamba lote na trekta ya oira.

p) Andika nomino moja kutokana na kitenzi hiki

(al.1)

Tatua

SEHEMU YA D**ISIMU JAMII**

Aziz: Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao Kenyatta, railways!

Shiko : Namba nane ngapi?

Aziz: Mbao ingia,blue.

Shiko: Nina hashuu.

Aziz: Blue auntie.

Shiko : sina.

Aziz: Ngia 46! Adams mbao Kenyatta railways gari bebabebe!

Ahendera :Mimi sinako ishirini.chukuako tu kumi.

Aziz: Dinga inakunywaga petrol mzee.

- b). Taja sifa sita za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya . (al.6)

MTIHANI WA PAMOJAWA MOMALICHE

102/3

KISWAHILI

Karatasiya3

FASIHII

2019

SEHEMU A: RIWAYA -CHOZI LA HERI**LAZIMA**

1. “Kwakwelinhalingumuhi”

- a) Wekadondookatikamuktadha wake. (alama4)
b) Ni haliganiyamsemewainayorejelewakwenyedondo. (alama16)

SEHEMU B: TAMTHILIA (KIGOGO)

Jibuswali la 2 au 3

2. ”Waonamiminiganda la muwa la juzi”

- a) Elezamuktadhawadondoohili (alama4)
b) Tambuambinuyauandishiiliyotumikakatikadondoohili (alama2)
c) Thibitishakuwahusikakadhaawanalinganishwanaganda la muwakatikatamthilia (alama14)

AU

3. Anwani “KIGOGO”imetumikakitashtitikumkejeliMajoka. Thibitisha (alama20)

SEHEMU C : HADITHI FUPI – TumboLisiloshibanaHadithiNyingine

Jibuswali la 4 au 5

4. Jadilijazandazaanwanikatikahadithizifuatazo

- a) ShibeInatumaliza (alama8)
b) Mtihaniwamaisha (alama6)
c) Mkubwa (alama 6)

AU

5. MAPENZI YA KIFAUURONGO

“Kutazamashulezavijijinikumwibuabingwakatikamtihaniwakitaifanikamakutarajiakupatamaziwakutokakwa kuku.”

- a. Elezamuktadhawadondoohili (alama 4)
b. Tambuambinumojayalughakwenyedondoohili. (alama 2)
c. Jadilimaudhuiyafuatayokatikahadithihii
i) Mabadiliko (alama 5)
ii) Uozo (alama 5)

iii) Shaka

SEHEMU YA D: FASIH SIMULIZI

6. a) Fafanuamchakatowauwasilishajiwavitendawili. (alama4)
 b) Linganishanaulinganuevitendawilinamethali. (alama10)
 c) Toa sababusitazakudidimiakwafasihisimulizi. (alama6)

SEHEMU YA E: USHAIRI

7. *Soma shairilifuatalokishaujibummaswali.*

Moyohaukongi:

Haidhuruuwewamwanadamu

Au wanyamamwitu.

Japomajiyamyumbishe
 Kandonimwabahari
 Kizeeutamwona
 Kwanguvuzauchawiwamoyo
 Mawimbiniakisukwasukwa
 Mithiliyajahazilililochoka
 Kwaurefuwa safari:
 Ingawaatabamizwamatumbaweni
 Na yakeserunimajikuitwaa
 Atang'ang'anakuidakajapokwashida
 Na majinikuelea
 Kama anayeyatishakuwa
 Badosihayamisuliipo.

Basiajabuusione
 Pakamaziwakunywa
 Katikauzima wake
 Au bi kizeekichwaakiyumbisha
 Kwamliowaala
 Amanyamakupaniakula
 Japojino la mwisho
 Liling'okajuzi.

Moyohaukongikwamsukunowawakati:
 Ni misuliinokonga.
 Moyo, simbawawakati.

- a) Hilinishairi la ainagani? (Alama 2)
 b) Elezamuundowashairihili. (Alama 4)
 c) Kwaninimshairianaelezakuwamoyohaukongi? (Alama 4)
 d) Tambuamishororobakikwenyeshairihili. (Alama 2)
 e) Elezambinumbilizaidhiniyamshairikwakurejeleashairihili. (Alama 2)
 f) Elezatoniyyashairihili. (Alama 2)
 g) Andikaubetiwatatuwalughatutumbi. (Alama 4)

COMPLIANT II
102/ KISWAHILI INSHA- KARATASI YA 1
JARIBIO LA PILI 2019

1. LAZIMA

Wewe ni mkaazi wa eneo ya Tushirikiane na unataka kuwania Ugavana katika Kaunti ya Mavuno. Andika tawasifu utakayowasilisha kwa raia ili waweze kukuchagua.

2. Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachoanza kwa;

Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho.....

COMPLIANT II

102/2 KISWAHILI – Karatasi Ya 2

(Lugha)Jaribio la Pili, na la Mwisho wa Muhula wa Kwanza, 2019

1. UFAHAMU : (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Zaraa ndio uti wa mgongo wa taifa la Kenya. Viwanda vingi nchini hutegemea kilimo kama malighafi yake na kuwalisha wafanyakazi. Licha ya umuhimu wa sekta hii, mkulima ambaye ndiye nguzo za zaraa anaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanavokwamiza juhudzi zake.

Mojawapo ya matatizo yanayomkabili mkulima ni ukosefu wa ushauri wa zaraa. Wataalamu wanaotarajiwa kumshauri mkulima kuhusu njia bora za kuzalisha na kuongeza pato lake ni haba ikilinganishwa na idadi ya wakulima wanaohitaji ushauri. Wachache walioko nao wanakwamizwa na mambo tofauti. Mathalani, utawapata hawaendi nyanjani ili kukutana na wakulima kwa kuwa hawana usafiri. Iwapo usafiri upo, huenda petroli ikawa ni kizungumkuti. Halikadhalika, usisahau kuwa baadhi ya wataalamu hawa ni walazadamu au mafisadi. Kuna wale wanaofika ofisini na kushinda siku nzima wakisoma gazeti huku wakijaza miraba, wakicheza bao au karata. Kuna wale nao ambao hufika ofisini wakaangika koti au sweta kitini ili waonekane kuwa bado wapo na kisha kutokomea kwenda kushughulikia mambo yao ya kibinaksi yasiyohusu ndewe wala sikio kazi waliyoajiriwa kuifanya.

Ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi nalo ni tatizo jingine linalotatiza kilimo nchini. Serikali haijaweka sera mahususi kuhusu matumizi ya ardhi. Wananchi wengi huongozwa na taratibu za utamaduni wa nasaba zao. Taratibu hizi hupendekeza ugawaji wa ardhi kwa minajili ya urithi kulingana na warithi waliopo. Si ajabu kuwa kote nchini, ardhi inayofaa kwa kilimo imekatwakatwa vipande vidogo vidogo ambavyo haviwezi kuwa na faida kwa zaraa.

Kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini ni changamoto nyingine inayokabili kilimo nchini. Ulimaji wa kile kipande cha ardhi mwaka nenda mwaka rudi, bila kukipa nafasi ya kukipumzisha, huufanya mchanga kupoteza virutubishi muhimu vinavyohitajiwa na mimea. Hili nalo huchangia kupunguza uzalishaji wa mazao. Ili kutatua tatizo hili, wakulima wengi hukimbia mbolea za kisasa ambazo badala ya kumsaidia, humwongezea madhila. Mbolea hizi zinatambulikana kuchangia uchafuzi wa mchanga na ardhi.

Mabadiliko ya hali ya anga nayo huongeza msururu wa madhila ya mkulima. Mabadiliko haya yamemfanya mkulima kushindwa kupanga wakati anaotakiwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia, kunyonyizia dawa na kadhalika. Mvua imekuwa adimu. Badala yake panakuwa na vipindi virefu vy'a kiangazi ambavyo huathiri bidii za mkulima. Maji nayo yanaendelea kupungua na wakulima wengi hawawezi kukimu mahitaji ya unyonyizaji maji mashambani.

- | | |
|---|-----------|
| (a) Andika anwani inayofaa kifungu hiki. | (alama 1) |
| (b) Huku ukirejelea kifungu, fafanua umuhimu wa kilimo hapa nchini. | (alama 2) |
| (c) Eleza changamoto tatu zinazowakabili wataalamu wa kilimo | (alama 3) |
| (d) Mbali na matatizo yanayowakumba wataalamu onyesha matatizo mengine matatu yanayokumba sekta ya zaraa. | (alama 6) |
| (e) Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. | (alama 3) |
| (i) yanayokwamiza | |
| (ii) sera | |
| (iii) adimu | |

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia haua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumking mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha walimu hasa ikizang'wa kuwa gharama ya maisha imepanda mara difu.

Hata hivyo, ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inaokana na ununuzi wa vitabu vya Kada na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama. Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanye.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwanga vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tuijilize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule na maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inavyohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hili ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo hutofautiana. Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa.

Kwa mfano, programu za kitahmini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula?

Sasa mbona fedha za ziada? Wanaotetea kupunguza kwa karo wana punguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotisha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahili wanapopata matokea mema. Hali hiyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa huduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile, hutumiwa kuwajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu maram uliozoleka katika shule nyingi ikumbukwe kuwe lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe.

Kwa marefu na mafupi yake, serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotozwa hasa katika shule za upili zinatafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangekuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwaajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo. Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinagsi.

Naamini kuwa hatua ya Waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kuijunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kuta mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yaliyopo kwa sasa.

- (a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 – 70)
(alamu 8, 1 ya mtiririko)

(b) Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 – 45) (alamu 7, 1 ya mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA(Alama 40)

- (a) Taja vigezo viwili vya kuainisha konsonanti. (alama 2)

(b) Bainisha aina za nomino zifuatazo: (alama 2)

 - i) Shetani
 - ii) Mjombake

(c) Taja ngeli za nomino zifuatazo: (alama 2)

 - i) pesa ii) vita

d) Kwa kutolea mfano, eleza maana ya vitenzi elekezi. (alama 2)

e) Tambua nyakati na hali katika sentensi zifuatazo: (alama 4)

 - i) Rais azuru eneo la Kisumu.
 - ii) Wanafunzi wanafanya mtihani.

f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa – wingi. (alama 2)
Kidole cha mkono wa kushoto wa mzee huyu kimeumizwa na mlango

g) Changanya sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa jedwali: (alama 4)
Mkongojo mrefu sana uliletwa na babu utauzwa na fundi mcheshi.

h) Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuayo: (alama 2)
Mtihani ambaao tulifanya ulikuwa mgumu sana.

i) Andika kwa msemo wa taarifa. (alama 2)
Mkutano huu utaendelea leo na kesho. Alisema mwalimu.
Mwalimu alisema kuwa mkutano huo ungeendelea siku hiyo na siku ambayo ingefuata.

j) Andika katika hali ya udogo: (alama. 2)
Mbwa mwenye ukali alimfukuza mtoto .

k) Yakinisha. (alama 2)
Hajui atokako wala aendako.

l) Tambua aina ya vitenzi. (alama. 2)
Babu angali anasoma gazeti.

m) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi: (alama. 2)

 - i) tawa ii) dawa

n) Tumia O' rejeshi. (alama. 2)

 - i) Mgeni ambaye huja ni mwanasheria.
 - ii) Mambo ambayo aliyasema hayasahauliki.

o) Tambua aina ya vitenzi katika sentesi hii. (alama. 2)
Babu angali anasoma gazeti

	Kiswahili	
l) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi.		(alama. 2)
i) tawa ii) dawa		
m) Tumia _ 'O'rejeshi.		(alama. 2)
n) Andika katika msemo wa taarifa;		
o) Kanusha sentensi hii: Mtoto huyu angalitibiwa mapema kifo kingaliepukwa.		(alama. 2)
p) Tambua shamirisho kipozi, kitondo na shamirisho ala katika sentensi ifuatayo. Sikuju aliwapikia wageni chai kwa maji ya chumvi. .		(alama.3)
q) Andika kinyume cha:		(alama.3)
i) Dhahiri		(alama.2)
ii) Kavu		
r) Andika maana tatu zinazojitokeza katika sentensi hii:		alama 3
s) Andika maana tatu zinazojitokeza katika sentensi hii: Wengine hawahitajiki.		alama 3

4. ISIMU JAMII (Alama 10)

- (a) Eleza juhudzi zozote tano zinazotumiwa kukiendeleza Kiswahili sanifu nchini Kenya. (alama 5)
 (b) Eleza jinsi uwililuga unawenza kuleta athari katika lugha na mawasiliano mionganoni mwa wanajamii. (alama. 5)

COMPLIANT II
MTIHANI WA MWISHO MUHULA WA KWANZA 2019
102/3
KISWAHLI
KARATASI YA 3
Fasihi

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

Jibu maswali yote

Nalitazama juu likichwa,

Matumaini yangu yakizama pamoja

na miale miekundu

Nalidhani lilikuwa jinamizi tu

Kwamba ulikuwa kesha n'acha

Walikuwa wameisha n'ambia

Walimwengu

Ela nilikataa katakata walosema

Nikajitia kuamini waloomba yalikuwa

Uzushi

Hadi siku hii nilopokea waraka,

Waraka ambaa ulikuwajeneza ka kuzikia

Pendo letu la miongo miwili.

- a)
- i) Hiki ni kipera gani cha fasihi simulizi? (alama 2)
 - ii) Eleza majukumu matano ya kipera hiki katika jamii. (alama 5)
- b) Eleza sifa 5 za mtambaji hodari. (alama 5)
- c) Andika sifa 5 za ngano. (alama 5)
- d) Eleza umuhimu wa fomyula ya kumalizia katika utambaji wa ngano. (alama 3)

SEHEMU YA B: RIWAYA**Asumpta Matei:Chozi La Heri**

2. ‘Lakini itakuwaje historical injustice,nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - b) Eleza tamathali mbil za lugha zilizoumika kwenye dondoo hili. (alama 4)
 - c) Fafanua sifa 3 na umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)
 - d) Taja mambo **SITA** yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho? (alama 6)

SEHEMU C: TAMTHILIA**Pauline Kea – KigogoJibuswali la 4 au la 5**

4. Siwezi nini? Naweza! Wewe ndiwe hujanipa fursa ya kukuthibitishia. Simba hageuki paka kwa kukatwa makucha.”
- a) Elezamuktadhawadondoohili (alama 4)
 - b) Eleza semi moja ambayo imetumika katika dondoo. (alama 2)
 - c) Ni nini ambacho msemaji anasema kuwa anaweza? (alama 2)
 - d) Ni vipi ambavyo msemaji amekatwa kucha? (alama 2)
 - e) Eleza sifa tano za msemewa. (alama 10)
- AU
5. Eleza mbinu alizotumia Majoka kufanikisha utawala wake. (alama 20)

SEHEMU D:-HADITHI FUPI**Alifa Chokocho:** - Masharti ya Kisasa

6. “Kweli mwalimu mkuu ana kazi nyingi na nyingine lazima aende usikuusiku kuzipunguza. Lakini leo ni leo...”
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
 - b) Eleza sifa 3 za mzungumzaji. (alama 6)
 - c) Eleza mbinu zifuatazo kama ziliviyotumiwa katika hadithi:
 - i) sadfa (alama 6)
 - ii) majazi (alama 4)

SEHEMU E: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yote

Unganambia ni mui, katu siuwati wema,
 Wewe ndiwe wangu bui, na Lousiwa ni mama,
 Neno kwamba suijui, ni kupotosha heshima,
 Siasi kutenda wema, kaandama uadui.

Wema nambiwa na ndia, hadi bandari salama,
 Hayo niliyasikia, wao wahenga wa zama,
 Penye wema tajitia, nipate taadhima,
 Siasi kutenda wema, japo munganinunia.

Ni iwe kupawa mali, ya kuhadaa mtima,

Niandame ufidhuli, nitengane nao wema,
 Hilo sitokubali, hapo waja wangasema,
 Sati kutenda wema, ujapokuwa ni ghali.

Sitomcha kabaila, nganiteuza nache wema,
 Muunganitia na jela, kisa imefanza huruma,
 Haragwe lenu talila, pamoja na yenu sima,
 Sati kutenda wema, japo tagoni talala.

Haufi mungaufisha, au hamipo karima,
 Mola atauhusha, weleleapo kuzama,
 Mimi ni huo maisha, hadi siku ya kiama,
 Sati kutenda wema, nganitia mshawasha.

Wema ingawa mchungu, tajaribu kutotema,
 Tautenda nenda zangu, niache wanaosema,
 Malipo yangu kwa Mungu, hayo, yenu si, lazima,
 Sati kutenda wema, kigharimu roho yangu.

- (a) Ukizingatia beti **nne** za mwanzo, taja mambo ambayo hata mshairi akifanyiwa hawezi kuacha kutenda mema. (alama4)
- (b) Eleza jinsi mtunzi wa shairi hili alivyotumiwa uhuru wake. (alama 4)
- (c) Mshairi alipata wapi ari ya kuzingatia wema? (alama 1)
- (d) Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 2)
- (e) Fafanua muundo wa ubeti wa pili. (alama 2)
- (f) Andika ubeti wa mwisho katika lugha ya nathari. (alama 4)
- (g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 3)
 - i) Mtima _____
 - ii) Kutotema _____
 - iii) Kigharimu roho yangu _____